KISWAHILI KARATASI 1

102/2

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho halafu ujibu maswali uliyoulizwa

Tsunami, tetemeko la ardhi baharini, iliyotokea Desemba mwaka 2004 katika bara la Asia ilikuwa na athari kubwa sana. Watu wasiopungua 170,000 walipoteza maisha yao kutokana na mawimbi yaliyotufulia na tsunami hiyo katika Bahari ya Hindi. Madhara na maafa hayo yalitanda hadi maeneo ya mbali kama upwa wa Afrika Mashariki ulio na umbali wa takribani kilometa 7,000 kutoka kitovu kikuu cha tsunami hiyo. Janga hili limeibua mjadala kuhusu madhara yanayotokana na nguvu za kimaumbile. Nguvu za kimaumbile zina uwezo wa kuzua majanga yasiyoweza kutarajiwa. Mlima wa volkeno uliotulia unaweza kuvuvumka na kutapakaza zaha ambayo inaweza kuua maelfu ya watu kama ilivyotokea huko nchini Kongo.

Majanga ya kimaumbile huweza kusababisha maafa, misiba na tanzia isiyokuwa na mshabaha. Sio rahisi kuweza kutasawari akilini kiwango cha madhara ya majanga haya hadi yanapotokea. Baadhi ya majanga ya kimaumbile ni kama vimbunga vya vumbi, zilizala, mafuriko, tufani, radi, ukame na hata moto.

Licha ya kuwa binadamu hawana uwezo wa kuzuia kutokea kwake, zipo hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa. Kwa mfano, yapo maeneo ambako kutokana na historia ni rahisi kujua ni majanga yepi ambayo huweza kutokea. Kuna maeneo ambako mafuriko hutokea kila zinaponyesha mvua za mvo. Jamii inayojikuta katika mazingira hayo inapaswa kujua ni hatua zipi za kuchukua. Mathalan ujenzi wa matuta, kuhimiza wakazi kusakini katika maeneo ya juu, kuwepo na huduma za dharura za kupambana na maradhi yanayochimbukana na ungi wa maji na kadhalika. Vivyo hivyo na ukame. Ni muhali kuweza kujua ukame utatokea lini. Hata hivyo, jamii inaweza kuchukua hatua fulani ambazo zinachangia kwenye ukame kamaukataji holela wa miti. Uchimbaji wa chemchemi ni njia nyingine inayoweza kutumiwa hasa kuhakikisha kuwa taraa ukame utazuka, watu hawataathirika kutokana na kuyakosa maji ya kutumia.

Wataalamu wameafikiana sasa kuwa baada ya tsunami iliyotokea lazima uwepo mfumo madhubuti wa kuweza kuudodosa mtikisiko wa ardhi ambao hutokea kwa muda kabla ya tetemeko lenyewe. Kwa njia hii watu wataweza kuonywa mapema na labda hasara kama iliyotokea kupunguzwa.

Maswali

(a) Toa kichwa mwafaka kwa makala haya. (Alama 2)

(b) Ni nini maana ya tsunami? (Alama 2)

(c) Ni lipi lililokuwa tokeo kuu la tsunami? (Alama 2)

(d) Eleza hatua zozote nne anazoweza kuzichukua binadamu kupambana na majanga ya kimaumbile. (Alama 4)

(e) Taja methali inayoweza kuufumbata ujumbe wa kifungu hiki. (Alama 2)

(f) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu hiki.**(Alama3)

(a) Kuvuvumka

(b) Kutasawari akilini

(c) Mvua za mvo

- **MUHTASARI (ALAMA 15)**
- **2. Soma taarifa hii ifuatayo kisha ujibu maswali**
- Kufaulu kwa lugha ya Kiswahili kutumika katika nyanja za sayansi na teknologia kunategemea sana utekelezaji wa mpango wa kwanza wa kutumia Kiswahili kufundisha elimu ya juu. Wanafunzi wakiwa weledi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kujifunza masomo ya sayansi, ufundi itawasaidia kujenga moyo wa udadisi, moyo wa kujiamini na moyo wa kutafuta maarifa ya ziada, wao wenyewe kwa kusoma vitabu mbalimbali vikiwemo vitabu vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.
-
- Moyo huu wa udadisi ndio msingi wa mtu kuwa mbunifu na mvumbuzi wa vitu mbalimbali. Wanafunzi hujenga moyo wa udadisi na kujiamini ikiwa lugha inayotumika kufundisha inaeleweka vizuri kwao. Hali hii hujidhihirisha pale wanafunzi wanapouliza maswali ya kutaka kujua zaidi kuhusu mada wanazofundishwa darasani au mambo wanayosoma wenyewe katika vitabu vya rejea. Ari hii ya udadisi miongoni mwa wanafunzi huweza kuonekana kwa kupima aina ya maswali yanayoulizwa. Kimsingi, maswali yote yanayofikirisha na yasiyohitaji jibu la wazi, la moja kwa moja, yanasaidia sana kukuza moyo wa udadisi na kujiamini.
- Kiswahili kinapaswa kuchukua dhima hii mpya ya kutumika katika nyanja za sayansi na teknolojia kwa sababu maendeleo ya jamii hupimwa kwa teknolojia ya kisasa iliyopo. Zamani ulimwengu ulionekana kuwa ni mkubwa lakini sasa hivi kwa kutumia teknolojia mpya ya mtandao wa mawasiliano, ulimwengu sasa unaonekana kuwa sawa na kijiji. Ili tusiachwe nyuma na wenzetu kimaendeleo, hatuhitaji tu kuwa watumiaji bali pia kuwa wachangiaji wa teknolojia hii mpya ya kisasa.

- Tunahitaji teknolojia hii kwa lugha ya Kiswahili ili watu wengi zaidi wasiojua kutumia lugha za kigeni (Kiingereza, Kifaransa n.k) waweze nao kujifunza teknolojia hii mpya kwa Kiswahili. Mathalani, kwa kuanzia tunahitaji teknolojia iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili yaani jinsi ya kutengeneza: *'Spellcheck'* ya Kiswahili kwa kutumia kompyuta, *'machine translation'* ya lugha ya Kiswahili na kutumia lugha nyingine muhimu duniani, mawasiliano ya mtandao kwa kutumia *barua–e* na jinsi ya kutengeneza programu mbalimbali za kompyuta kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Jamii itanufaika sana na teknolojia hii mpya ikiwa tu itakuwa imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

- **2. MASWALI**

- a) Andika anwani mwafaka kwa taarifa uliyosoma. (Maneno 5 –6)(Alama 1)

- **Matayarisho**

  - **JIbu**

b) Kwa nini Kiswahili kinafaa kuafiki mabadiliko katika nyanja za sayansi na teknolojia?

(Maneno 55 – 65) (alama 8)

Matayarisho

Jibu

c) Fupisha aya ya kwanza na ya pili.

(Maneno 50 – 60) (Alama 6)

Jibu

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) **Akifisha sentensi ifuatayo**

je utakuja kwetu siku ya alhamisi. (alama 2)

b) **Onyesha kundi Nomino (KN) na kundi Tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo**(alama 4)

(i) Filamu hiyo nzuri ilivutia

ii) Mtoto ataimba vizuri

c) **Andika sentensi zifuatazo ukizingatia maagizo uliyopewa katika mabano:-(**alama 2)

Magari yote yalitiwa vidhibiti mwendo (mazoea)

(ii) Alichora akatuzwa (ngali ya masharti)

d) **Tofautisha sentensi zifuatazo kimaana kwa kuongozwa na vivumishi vilivyopigiwa mistari:** (alama 2)

(i) Mtoto <u>mwenyewe</u> ndiye huyu

(ii) <u>Mwenye</u> mtoto ndiye huyu.

(e) **Bainisha viambishi awali na tamati katika sentensi ifuatayo** (alama 2)

Walipigiana

(f) **Tunga sentensi kwa kutumia viunganishi vifuatavyo:-** (alama 4)

Jinsi

ii) Sembuse

Kwa kuzingatia upatanishi wa Kisarufi ufaao, tunga sentensi sahihi ukitumia nomino zifuatazao. (alama 4)

Ulezi

Mate

h) **Andika sentensi hizi tena bila kutumia kirejeshi "amba''**

(i) Mtahiniwa ambaye husoma kwa bidii ndiye ambaye hufaulu mtihani wake Vizuri (alama 2)

(ii) Mtahiniwa ambaye amefaulu vizuri mtihani wake hujiunga na chuo kikuu(alama 2)

(i) Tambua aina za vielezi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo.

(i) Nilipomdai pesa zangu alinijibu kimzahazaha (alama 1)

(ii) Wanafunzi wanacheza uwanjani (alama 1)

j) **Ichanganue sentensi hii kwa njia ya vitawi**

Mama alimpikia mtoto uji kwa sufuria. (alama 4)

k) **Kwa kutumia maneno machache, eleza tofauti iliyoko katika sentensi zifuatazo.**

Alichekelewa alipofika

Alichekesha alipofika

Alichekelea alipofika (alama 3)

l) Geuza usemi huu uwe wa taarifa:

" Sikubaliani nawe unaposema mambo haya ni ya kweli". Msemaji mmoja akamwambia mwingine. (alama 2)

m) **Tunga sentensi <u>tatu</u> kulingana na maagizo haya:**

(i) Sentensi sahili (alama 1)

(ii) Sentensi ambatano (alama 1)

(iii) Sentensi ya changamano (alama 1)

n) **Tambua aina za vishazi vilivyotumika katika sentensi hizi zifuatazo**

Juma aliyecheza vizuri alituzwa vyema (alama 2)

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

4. **Yasome mazungumzo haya kisha ujibu maswali yafuatiayo**

- MPOTEVU: Nataka pande za Kaya. Hapa Mkanyageni nimejaribu kutafuta rafiki wa kufaa, nimekosa. Sasa nakaa kule mji wa Kale katika bweni la wageni.

  KUPE: Lahaula! Umeshampata mwenyeji atakayekutimizia haja zako zote

  MPOTEVU: Ni yupi huyo?

  KUPE: Kutafuniwa umeshatafuniwa; kulikobaki ni kumeza tu

  MPOTEVU: Mbona sikuelewi?

  KUPE: (Akijongeza kiti chake karibu) Basi tuyaache hayo. Kwani hasa umeletwa na shughuli gani huku kwetu?

  MPOTEVU: Oh! Ni kama kufanyafanya biashara na kutalii kidogo ili kutazama ulimwengu wa Walimwengu

  a) Mbinu ya majina iliyotumiwa yatosha kufasri mada. Jadili. (alama 3)

  b) "Lahaula! Umeshampata mwenyeji atakayekutimizia haja zako zote"
  Ni mwenyeji gani anayezungumziwa hapa? (alama 2)

  c) Hebu tegua kitendawili kilichomo:"Kutafuniwa umeshatafuniwa; kulikobaki ni kumeza tu. (alama 2)

  (d) Taja sajili ya mazungumzo haya (alama 1)

  (e) Zitaje sifa mbili za sajili hii. (alama 2)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

KARATASI YA 1

KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

a) Tsunami (Alama 2)

b) Tetemeko la ardhi linalotokea baharini (Alama 2)

c) i)Vifo vya watu wengi
ii)vifo vya watu zaidi ya 170,000 (Alama 2)

d) Zipo hatua kadha kutegemea janga linalohusika.Hoja muhimu ni;-

i) Ujenzi wa matuta

ii) Kuhimiza watu kwenye maeneo ya juu pale ambapo pana shida ya mafuriko
Kuwepo kwa huduma za dharura za kupambana na majanga yoyote yanayotokea
Uchimbaji wa chemichemi pale ambapo pana shida

Kuwepo na mfumo thabiti na kudodosa uwezekano wa kutokea kwa zilizala au tetemeko la ardhi (Zozote 4 x 1 = 4)

e) Kinga ni bora kuliko tiba / Heri Kinga kuliko tiba (Alama 2)

f) a) Kulipuka ghafla (Alama 1)

b) Kuona picha akilini / kuwazia akilini (Alama 1)

c) Mvua za mafuriko (Alama 1)

MUHTASARI

a) i) Kiswahili, Sayansi na Teknolojia

ii) Kiswahili kutumika kwenye Nyanja za Sayansi na Teknolojia

Kiswahili na Teknolojia mpya ya Mtandao wa mawasiliano

Kiswahili kielezwe Kisiyansi na kiteknolojia. Maneno (5-6)1 x 1 = 1 (Alama 1)

b) i) Kwa sababu maendeleo ya jamii hupimwa kwa teknolojia ya kisasa ilivyo

ii) Kwa sababu ya mabadiliko katika mawasiliano

Kwa sababu teknolojia mpya ya mtandao wa mawasiliano

Kwa sababu lugha zingine zimebadilika kwa kufuata sayansi na teknolojia

Kwa sababu wale wasioelewa lugha za kigeni waweza kuielewa lugha ya Kiswahili

Kwa sababu ya kuimudu lugha ya Kiswahili kwa kuifanya ioane na teknolojia ya kisasa

Kwa sababu ya kubuni vituo vya programu mbalimbali

c) i) Kiswahili kifunzwe kwa kuzingatia Sayansi na teknolojia.

ii) Wanafunzi waonyeshe uledi wao katika somo la Kiswahili

Wale wanaofunza na kunfunzwa wakithamini Kiswahili

Wahusika wote wajenge moyo wa udadisi

Wahusika wote wajenge moyo wa kujiamini

Wahusika wote wajenge moyo wa kutafuta maarifa ya ziada

Wahusika wote wawe na mazoea ya kusoma vitabu mbalimbali

MAUTMIZI YA LUGHA

½ ½ ½ ½

a) Je , utakuja kwetu siku ya Alhamisi ? ***(Alama 2)***

b) i) Filamu hiyo nzuri – KN ***(Alama 1)***

ilivutia – KT ***(Alama 1)***

ii) Mtoto – KN ***(Alama 1)***

ataimba vizuri – KT ***(Alama 1)***

c) i) Magari yote hutiwa vidhibiti mwendo ***(Alama 1)***

ii) Angalichora angalituzwa ***(Alama 1)***

Mtoto mwenyewe – kusisitiza ***(Alama 1)***

Mwenye mtoto – umilikaji ***(Alama 1)***

Viambishi awali – wali ***(Alama 1)***

Viambishi tamati – iana ***(Alama 1)***

Jinsi- Sentensi iwe na maana ya namna, hali fulani au aina

k.m Jinsi nilivyomwona sidhani kama atakuwa amepata nafuu leo. ***(Alama 2)***

Sembuse – Sentensi ionyeshe kinyume hasa pale ambapo pana ulinganishi K.M Onyango hamsaidii mzazi wake sembuse wewe usiyehusiana naye! (Alama 2)

Mtahiniwa atunge sentensi sahihi

K.M- Ulezi wa mtoto huyu ulikuwa mbaya ***(Alama 2)***

- Mate yaliyowatoka yalikuwa na viini ***(Alama 2)***


i) Mtahiniwa asomaye kwa bidii ndiye afauluye mtihani wake vizuri ***(Alama 2)***

Mtahiniwa aliyefaulu vizuri mtihani wake hujiunga na chuo kikuu ***(Alama 2)***

i) Kimzahamzaha – kielezi namna kikariri ***(Alama 1)***

Uwanjani – kielezi cha mahali ***(Alama 1)***

8 x ½ =



k) i) Sentensi ya kwanza inaeleza kuwa yeye alipofika alifurahiwa na watu au alidharauliwa

(Alama 1)

ii) Sentensi ya pili inaeleza kuwa alipofika aliwafanya watu wacheke ***(Alama 1)***

Sentensi ya tatu inaeleza kuwa alipofika alicheka kwa niaba ya mtu mwingine au alionyesha dhihaka ***(Alama 1)***

l) Msemaji mmoja alimwambia mwengine ya kuwa hakukubaliana naye aliposema kuwa mambo hayo yalikuwa ya kweli

(Alama 2)

m) i) Tuliimba ***(Alama 1)***

ii) Watu wengi walikuja na kulala kwetu ***(Alama 1)***

Mama aliyeenda sokoni ndiye aliyerudi ***(Alama 1)***

n) Juma aliyecheza vizuri – kishazi tegemezi ***(Alama 1)***

alituzwa vyema – kishazi huru

(Alama 1)

ISIMU JAMII

4. a) **MADA**:- Ulevi na anasa humpotosha mja

(Alama 1)

- Mbinu iliyotumika ni ile ya kimajazi kwa sababu inatafsiri tabia za wahusika

(Alama 1)

Mfano kupe ni jina linaloashiria mtu anayewategemea / wanyonya wengine

- Ni kwenye baa yenye vidosho walio na tabia za kuwalaghai watu kama **MPOTEVU.**

(Alama 1)

b) Mwenyeji anayezungumziwa hapa ni msemaji mwenyewe kwa jina **KUPE** ***(Alama 2)***

c) **KUPE** anamhakikishia kuwa yeye yuko tayari kuwa rafiki yake, kilichobaki ni yeye**MPOTEVU**

kumwambia tu. ***(Alama 1)***

Mazungumzo ya walevi/ wapenda raha na anasa ***(Alama2)***

i) Lugha ya kutaniana / mafumbo k.m kutafuniwa umeshatafuniwa

Lugha ya mahaba/ mapenzi k.m umeshampata mwenyeji atakayekutimizia haja zako zote

Lugha ya mishangao k.m Lahaula ! Oh! Zozote 2 x 1= 2

102/2

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

SWALI LA KWANZA –UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Teknolojia mpya ni tawi la maarifa linalohusiana na sayansi kwa upande mmoja na uhandisi (uinjinia) kwa upande mwingine. Sayansi ni elimu inayotokana na uchunguzi na majaribio katika maabara nao uhandisi ni ujuzi wa kuunda mitambo. Maarifa ya sayansi yanapotumiwa kutengeneza vitu viwandani, hali hii inakuwa teknolojia.

Zao mojawapo la teknolojia mpya ni simu tamba. Watu vijijini sasa wanawasiliana na jamaa zao walio mbali. Akina nyanya wanapopanda njugu, kupalilia migomba, kukama ngamia au kukuna nazi, wanaweza kuzunguuza na wajukuu zao walio uingereza, uchina au kwingine kule.

Hakuna mahali ambapo hapajafikwa na teknolojia mpya. Tukitembelea baadhi ya nyumba tutaona vifaaa kama vile tanuri la miale au mikrowevu ambalo linapika maharagwe yakaiva kwa dakika chache tu. Majokofu nayo yanatusaidia kuhifadhi vyakula bila kuharibika. Hata maiti na mizoga inaweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kwa ajili ya utafiti bila kuoza katika ufuo au mochari.

Kwa upande wa kilimo, teknolojia imefanya makubwa. La kustaajabisha ni mtu mmoja kulima eneo kubwa la shamba kwa trekta halafu akapanda kwa tandazi, akanyunyizia dawa kukausha magugu, akavuna na kukoboa mahindi akiwaa peke yake. Siku hizi inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu kwa sababu ya teknologia mpya.

Teknolojia hii imewezesha watu kuvumbua aina nyingi za nishati. Badala ya kutegemea umeme unaotokana na maji tu, sasa watu wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya jua kupata umeme. Kwa sababu hii, hata mababu zetu vijijini wanatazama televisheni bila shida wala wahka.

Kwa upande mwingine, teknolojia ina madhara yake. Kwa mfano, uundaji wa silaha kali unaendelea kuwaangamiza watu wengi. Mabomu ya kitonoradi yaliyoangushwa Hiroshima na Nagasaki Japan mwaka 1945 ni zao la kisayansi. Haya yaliwaua watu wengi na madhara yake bado yanadhihirika hata leo katika maumbile ya watoto wanaozaliwa na upungufu. Tena magaidi na wahalifu wa kimataifa wanatumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao za kutenda maovu. Isitoshe, inawezekana kutumia teknolojia kuagizia benki kutuma pesa nje ya nchi ya bila mwenye hazina kujua.

Wahalifu wanaweza kusikiza mawasiliano ya watu kwa simu hata ikiwa ni baina ya polisi. Kisha matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula vilivyokuzwa kutumia teknolojia mpya.

Katika usafiri, kuna gari moshi lenye kutumia stima badala ya makaa. Hili ni zao la teknolojia mpya vile vile. Ingawa mwendo wake ni wa kasi, kasi hiyo na stima huweza kusababisha ajali mbaya mno.

Ingawa madhara yapo lakini manufaa ya teknolojia ni mengi zaidi kuliko madhara yenyewe. Faida ni kuwa teknolojia hurahisisha shughuli za watu kama vile kufua na kusafiri. Pia hufanya matokeo ya shughuli kuwa bora zaidi. Kazi iliyopigwa chapa kwa kompyuta huwa safi na bora. Vile vile, vitu vinavyotengenezwa siku hizi ni vidogo na vyepesi lakini bora zaidi. Tukichukua mfano wa magari tunaona kuwa ni madogo lakini yenye muundo wa kuvutia. Tatizo tu ni ile kasi kubwa ambayo ni moja ya mambo yanayosababisha ajali nyingi.

Gharama ya vitu vinavyotengenezwa kutumia teknolojia mpya ni nafuu. Teknolojia hii inatumia malighafi ya kisasa na hivyo kuhifadhi madini yetu. Pia huunda vitu ambavyo matumizi yake yanadhuru mazingira.

Tusisahau kuwa hata hapa kwetu matekinia wa ‘jua kali’ wanapiga hatua. Wanajitahidi usiku na mchana kuunda vitu vya kutuuzia kwa gharama nafuu. Mitambo ya kusukuma maji sasa inapatikana. Vyombo vya kusafirisha mizigo, vifaa vya kunyunyizia maji, tanuri ya kuoka inayohifadhi nishati na vingine vingi, sasa vinaundwa ili kuimarisha sekta hii. Ikiimarika, Kenya inaweza kuwa nchi yenye uwezo wa viwanda.

Maswali

Eleza umuhimu wa teknolojia mpya kwa zaraa (alama 2)

“Kwa hakika uhandisi umepiga hatua.” **Thibitisha** kauli hii kulingana na taarifa. (alama 2)

Unga mkono kauli kwamba hakuna mahali ambapo hapajafikiwa na teknolojia. (alama 2)

Uvumbuzi wa teknolojia **umeisaidiaje** ulimwengu kupunguza gharama ya uzalishaji wa bidhaa? (alama 3)

Taja athari zozote mbili za kughasi za uvumbuzi. (alama 2)

Eleza jinsi uvumbuzi umeibuka na anasa ya kipekee. (alama 2)

Eleza maana za maneno haya jinsi yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

Malighafi

Matekinia

SWALI LA PILI UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali yanayofuata

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza, ubongo hunasa jambo kisha hulihifadhi. Baadaye huanzisha mfuno wa kutoa kilichohifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yoyote katika mojawapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitaji mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini) bidhaa za soya, matunda, maziwa, bidhaa za ngano, samaki pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madini haya ni mboga za kijani , dengu, mawele, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati, awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini kwa hivyo vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisichohatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa na kuhusisha jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kuvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na namna ya kukitoa.

Hali kadhalika mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa kuwa mazoezi ya kuyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na ratiba ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya haya mazoezi ya kiakili kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitanza ndimi, ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo wa kuyakumbuka mambo ni jamii iliyopiga hatua kimendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

(Ijaribu na uikarabati Isaac Ipara/ Francis waititu Uk 180 – 181)

Maswali

Kwa maneno 60 – 65, **fupisha** mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.

Matayarisho

Jibu

Fupisha aya tatu za mwisho za mwisho kwa maneno 80-90

Matayarisho

Jibu

SWALI LA TATU – MATUMIZI YA LUGHA

Konsonanti hizi zinatamkiwa wapi? (alama 3)

n ……

k ……

p ……

Tambulisha aina za vielezi vya namna katika sentensi zifuatazo (alama 2)

Nyanya hutembea kwa mkongojo

Mwalimu alimkemea kijeshi

Eleza matumizi ya kiambishi ‘ji’ katika sentensi zifuatazo

Mtoto amejikata kidole.

Yeye ni mchoraji.

Ainisha sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. (alama 5)

Wao watarudi mapema lakini mimi nitabaki.

Kanusha sentensi ifuatayo (alama 2)

Huyu ndiye nimtakaye

Bainisha virai na utaje ni vya aina gani (alama 3)

Atapona baada ya juma moja.

Alimnyemelea kwa woga

Andika sentensi zifuatazo katika hali ya udogo. (alama 2)

Chungu changu kimevunjika.

Ng’ombe wangu ana ndama mkubwa.

Andika katika kauli ya kutendeshea. (alama 1)

Kwa nini unamfanya mtoto wake kulia?

Ainisha mofimu za sentensi ifuatayo. (alama 3)

Alimlia

Badilisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe katika hali iliyopigiwa mstari. (alama 2)

Alimtia <u>hasira</u> alipotoa uamuzi huo. (kitenzi)

Kazi hii imefanywa kwa ustadi. (kielezi)

Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Sisi tunapenda mchezo wa soka," Otieno alisema

Bainisha yambwa kitondo na yambwa kipozi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

Rama aliwapikia wageni wake chakula kitamu.

Akifisha. (alama 2)

Riwaya ya siku njema imesomwa na wengi.

Andika katika ukubwa. (alama 1)

Nguo zake zimeloa maji.

Akifisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu kuleta maana tatu tofauti. (alama 3)

Mashaka akasema amempata.

Tumia 'A' unganifu katika sentens kudhihirisha matumizi ya: (alama 2)

Kivumishi

Kiwakilishi

Andika katika wingi (alama 1)

Baka lililoko kipajini linatisha.

Ni hisia zipi zinazodhihirika katika matumizi haya ya vihusishi?

Maskini! Alianguka mtihani wa kitaifa.

Mashala! Mtoto huyu ameuubwa akaumbika.

SWALI LA NNE – ISIMU JAMII

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Kijana: Mama unakwenda?

Mama: Kwenda wapi?

Kijana: Ala, wapi kwingine ila mjini?

Mama: Siendi.

Kijana: Haya basi. Dere wacha mioto! Beba mmoja, kwako! Dada njoo, usisafirie mtumba…. Nafasi ya mtu mmoja, Commercial….. usiachwe, gari ni ishirni tu…… bei ya chini kuliko mkate.

Dada: Nina ashu, utanibeba?

Kijana: Ah, dada! Ongeza dada, tayari nimekupunguzia kwa kukwambia mbao. Kawaida huwa ni finje

Dereva: Auntie anasema nini?

Kijana: Ananyonga ashuu.

Dereva: Basi mbebe sare.

Kijana: Dada dere amekulipia. Basi dere gari iko seti, stage ya kwanza jijini.

Maswali

(i) Mazungumzo haya hutokea katika muktadha gani? (alama 1)

(ii) Toa ushahidi. (alama 3)

Eleza sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu mbali na ulizotaja katika (a) (ii) hapo juu. (alama 6)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA 2
KISWAHILI 102/2

SWALI LA KWANZAUFAHAMU

- Kazi ya kulima, kupanda kupalilia na kuvuna inaweza kufanywa na mtu mmoja.
  Inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu. (2 x 1 = 2)

- Kuna mitambo ya kusukuma maji, vyombo vya kusafirisha mizigo, vifaa vya kunyunyizia maji, tanuri ya kuoka inayohifadhi nishati n.k
  Kuna gari moshi linalotumia stima badala ya makaa.
  Kuna majokofu yanayotuwezesha kuhifadhi vyakula bila kuharibika. (2 x 1 = 2)

- Nishati ya jua imewezesha watu vijijini kupata umeme.
  Kutumia simu tamba, watu walio vijijini wanaweza kuwasiliana na walio hata ng'ambo.
  Mashambani teknolojia inatumika katika kilimo, kupanda, kupalilia na kuvuna.
  (2 x 1 = 2)

- Kazi ya kulima, kupanda, kupalilia n.k inaweza kufanywa na mtu mmoja akitumia trekta.

  Mtu anaweza kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu.

  Badala ya kutumia umeme unaotokana na maji watu sasa wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya jua kupata umeme (3 x 1 = 3)

- Uundaji wa silaha k.m mabomu ya kitonoradi zinazotumiwa kuwaangamiza watu.

  Wahalifu na magaidi wa kimataifa wanatumia teknologia mpya kufanya uhalifu.

  Wahalifu wanaweza kusikiza mawasiliano ya watu kwa simu, hata baina ya polisi.

  Inawezekana kutumia teknolojia kuagizia benki kutuma pesa nje ya nchi bila mwenye hazina kujua.

  Matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula vilivyokuzwa kutumia teknolojia mpya. (2 x 1 = 2)

- Gari moshi latumia stima badala ya makaa

  Mikrowevu yaweza kupika maharagwe yakaiva kwa dakika chache.

  Majokofu yanatuwezesha kuhifadhi vyakula bila kuharibika.

  Magari sasa ni madogo na yenye muundo wa kuvutia na huenda kwa kasi. (2 x 1 = 2)

Malighafi – mali inayotumiwa kutengenezea kitu kingine. (alama 1)

Matekinia – mafundi. (alama 1)

SWALI LA PILI – UFUPISHO

- Vyakula vyenye vitamin B vyenye amino asidi na vile vyenye madini ya chuma huimarisha uwezo wa kukumbuka.

  Vyakula vyenye glukosi husaidia kuendesha viungo vya mwili na ubongo, lakini mtu anatakiwa kutahadhari, asizidishe kiwango cha sukari mwilini, kwani kinaweza kuathiri uwezo huu.

  Ni muhimu kutotumia vileo na nikotini kwani huzorotesha uwezo wa kukumbuka.

  (3 x1 = 3)

– Ni muhimu kuepuka woga na kuvurugika akili kulikozidi.

Haya huathiri uwezo wa kukumbuka.

Mtu lazima awe na ratiba ya kunyoosha viungo.

Unyooshaji wa viungo huimarisha ubongo pamoja na uwezo kukumbuka.

Haya yaandamane na michezo ya kiakili ambayo huchangia uimarishaji wa uwezo huu.

Uimarishaji wa uwezo huu ni muhimu kwa maendeleo ya jamii na unahitaji mchango wa kila mmoja.

(hoja zozote 5 x 2 = 10)

Utiririko – alama 2

Makosa

Ondoa makosa ya kisarufi hadi makosa 6 x ½ = 3

Ondoa makosa ya hoja hadi makosa 6 x ½ = 3

Ziada – maneno 10 ya kwanza ya ziada apoteze alama 1, kisha ½ alama kwa kila maneno 5 ya kufuatia.

SWALI LA TATU- MATUMIZI YA LUGHA.

(a) (i) n - menoni (1)

(ii) k - kaakaa laini (1)

(iii) p - midomoni (1)

(b) (i) Kwaa mkongojo - namna ala/ kitumizi (1)

(ii) Kijeshi - namna mfanano (1)

(c) (i) amejikata - kumrejelea mtendaji. (1)

(ii) mchoraji - mazoea ya kutenda jambo. (1)

(d)

S					
S1			U	S2	
KN	KT			KN	KT
W	T	E		W	T
Wao	watarudi	mapema	lakini	mimi	nitabaki

(alama 5)

(e) Huyu siye nimtakaye. (alama 2)

(f) (i) – baada ya juma moja – kirai elezi (alama 1)

(ii) kwa woga – kirai elezi (alama1)

(i) Kijungu changu kimevunjika (alama 1)

(ii) Kigombe changu kina kidama kikubwa. (alama 1)

(h) Kwa nini unamlizia mtoto wake

(i) A - Kiwakilishi cha nafsi ya tatu.

li - Kiwakilishi cha wakati uliopita.

m - Kiwakilishi cha mtendewa.

l - Shina la kitenzi.

i - Kiendelezi cha kauli

a - Kiishio. (6 x ½ = 3)

(j) - alimkasirisha (alama 1)

- Kistadi (alama 1)

(k) Otieno alisema kuwa wao walikuwa wanapenda mchezo wa soka. (alama 2)

(l) Wageni - kitondo (alama 1)

Chakula kitamu – kipozi (alama 1)

(m) Riwaya ya siku njema imesomwa na wengi. (alama 2)

(n) Manguo yao yameloa maji. (alama 1)

(o) (i) Mashaka akasema, “Nimempata.” (alama 1)

(ii) “Mashaka.” Akasema, “nimempata.” (alama 1)

(iii) “Mashaka?” Akasema, “Nimempata.” (alama 1)

(p) Mzigo **wa** mwenzio ni kanda la usufi (kivumishi) alama 1)

La kuvunda halina ubani. (kiwakilishi) (alama 1)

(q) **Ma**baka **ya**li**yo**ko **vi**pajini **ya**natisha. (alama 1)

(r) (i) Masikitiko / huruma. (alama 1)

(ii) Shukrani / kutosheka / kuridhika. (alama 1)

SWALI LA NNE ISIMU JAMII

(i) Lugha hii hutumika katika muktadha wa biashara ya usafiri wa umma hasa matatu. (alama 1)

(ii) Ushahidi:

dere (dereva)

nafasi ya mtu mmoja

…stage ya kwanza jijini

utanibeba?

n.k (3 x 1 = 3)

(b) - Lugha kusifia ubora wa huduma inayotolewa

- Lugha ya ushawishi
- Lugha ya chuku
- Lugha isiyo sanifu
- Lugha inalenga vijana zaidi – katika kifungu hiki utingo haelewani na mama lakini anaelewana na dada.
- Msamiati unarejelea usafiri na pesa.
- Kuchanganya ndimi n.k (6 x 1 = 6)

KISWAHILI KARATASI 3

102/2

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

SOMA MAKALA KISHA UJIBU MASWALI

Bi mwenyekiti , wataalamu wa lugha, waamuzi na washiriki waliojumuika kwenye mdahalo, mabibi na mabwana. Si vema niwapotezee wakati wenu kutetea mjadala kwa madhumuni ya kuteta tu. Sijaja hapa kupiga makelele mithili ya mbwa mdomo wazi (makofi). Nimefika hapa kuwaandalia hoja madhubuti zitokanazo na kina cha mawazo na maoni murua moyoni mwangu. Mada ya mjadala inasema kuwa Kiswahili inatosheleza matakwa yote kimawasiliano.

Bi mwenyekiti, Swali tunalopaswa kujiulizwa ni, Je, mawasiliano ni nini? Fafanuzi mbalimali zimetolewa. Aidha wavumbuzi wa kisayansi / kiteknolojia wameasisi mbinu za kisasa zinazorahihisha mawasiliano na kuufanya ulimwengu kuwa kama kijiji. Tukijikita kwenye muktadha wa mjadala huu, twaweza tukaafiki kwamba mawasiliano ni kupasha ujumbe namna unavyoeleweka na mpokezi. Hivyo ni kusema kwamba mja aweza akatumia lugha, ishara au alama kumfikishia mwenzake ujumbe uliokusudiwa. Pindi mpokezi akosapo ufahamu wa jambo linaloangaziwa, basi hapo mawasiliano yatakuwa <u>muhali.</u>

Mawasiliano huwezesha makabila mbalimbali kutangamana huku yakiendeleza biashara. Maazimio na miradi ya taifa yaweza kusambazwa kotekote kwa Kiswahili kupitia radio, magazeti na runinga. Huu ni ukweli wa wazi usiopingika. Kiswahili bila shaka, chajitosheleza kimawasiliano.

Bi mwenyekiti, niliyoyadokeza yana <u>ithibati.</u> Naomba kutajiwa muktadha wowote, si nyumbani, si ofisini, si kanisani ambamo mawasiliano kwa Kiswahili yangekwama. Duru za kuaminika zashikilia kuwa mtaalamu wa tarakilishi ulimwenguni, Bill Gates, ameunda mitambo itumiayo misamiati na lugha ya Kiswahili. Ajabu!

Bi mwenyekiti, hawa wapinzani wana upungufu mmoja, nao ni <u>yamkini</u> hawajimudu katika lugha ya Kiswahili. Wanatumia upungufu wao huo dhidi ya mjadala unaojitetea wenyewe. Mmoja wa wanenaji amejikanganya na kujipinga kwa kusema, “mwacha mila ni mtumwa.” Kauli hii inazidi kuthibitisha kuwa Kiswahili kina ukwasi wa kutosheleza mawasiliano. Wapinzani wangekuwa weledi wa Kiswahili wangegundua

kuwa usemi huu unaafikiana na mjadala (makofi). Ama kwa kweli fumbo mfumbie mjinga, mwerevu atalifumbua! Aidha uneni usisitizao kuwa “Alalaye usimwamshe, ukimwamsha utalala wewe” unao mashiko. Bi mwenyekiti, tamati nimefika nikiwasihi wenzangu wasisite kuvuka sakafu ili tuufanikishe mjadala. Asanteni.

a) Upande wa upinzani ulishikilia mada ipi? (alama 1)

b) Msemaji wa upinzani amejikanganya anapotumia msemo: “Mwacha mila ni mtumwa .” Fafanua. (alama 2)

c) Mwandishi anasema, “Alalaye usimwamshe ukimwamsha utalala wewe.” Thibitisha ukirejelea muktadha wa hotuba uliyoisoma. (alama 4)

d) Kunapatikana shangwe (makofi) zaidi ya mara moja katika taarifa. Eleza chanzo cha shangwe hizo. (alama 2)

e) Mbali na mbinu za mawasiliano zilizozungumziwa katika taarifa, zitaje mbinu nyingine za kisasa ambazo zimerahisesha mawasilano. (alama3)

f) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya msamiati huu:

Yamkini----------

Ithibati----------

Muhali----------

UFUPISHO

<u>Soma makala haya kisha ujibu maswali.</u>

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea kuwafedhehesha wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama.

Ajali za baraza barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka wakiwemo viongozi na watu mashuhuri.Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani ni pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya uchukuzi na mawasiliano.Madereva wengi hung’oa vidhibiti mwendo vilivyowekwa, hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawayapeleki magari yao kukaguliwa mara kwa mara kama inavyopaswa. Yale yanayopelekwa kwa ukaguzi, mengi hushindwa kutekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani.Fauka ya hayo, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya, kama miraa na bangi hutumiwa sana na hawa na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini Kenya

utapata kuwa barabara haziko katika hali nzuri. Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidibwi mithili ya michimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa na lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame kinachohitajika kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kupanda magari ambayo tayari yamejaa. Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inawafaa watambue ya kwamba wanajukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi kuliko ile ya kilomita themanini kwa saa iliyokubaliwa.Inafahamika kuwa maafisa wa usalama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita vya ufisadi na ajali za barabarani ni mwananchi mwenyewe ambaye atawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wakamatwe na kupelekwa kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na kuchukuliwa hatua kali, matatizo haya yataisha. Lakini kabla kufikia hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza yakukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

(a) Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya pili na tatu.
(maneno kati ya 45-50 Alama 7)

Matayarisho:-

Jibu:

(b) Bila kubadilisha maana iliyokusudia, fupisha aya mbili za mwisho.
Maneno kati ya 35-40 (alama 05)

Jibu:

Utiririko alama 3 (jumla).

3 **MATUMIZI YA LUGHA.**

a) **Onyesha kitenzi kikuu na kisaidizi katika sentensi hii.**
Nimewahi kumkumbusha makosa yake. (al 2)

b) Umepewa aina tofauti za nomino. Tunga sentensi idhihirishayo kila aina ya nomino;

(al 3)

Nomino ya wingi

Nomino ya kitenzi jina

Nomino ya kipekee

c) **Tunga sentensi kutofautisha maneno haya.** (al 2)

(i) Dhamini

(ii) Thamini

d) **Tunga sentensi kuonyesha matumzi ya viakifishi hivi.**

(i) Alama hisi (al 1)

(ii) Parandesi (Al 1)

(iii) Alama za mtajo / usemi (Al 1)

e) Andika konsonanti mbili zinazotamkiwa kwenye ufizi. (al 2)

f) Eleza maana ya msemo huu.

Maisha ya kitwea (al 2)

g) Geuza vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya kutendeana, kisha uvitungie sentensi.

(i) Ja (al 2)

Pa. (al 2)

h) Eleza maana mbili ya “La” (Al 2)

(i) Unda vitenzi viwili kutokana na kila moja ya majina

Mtukufu (Al 1)

Mchumba (Al 1)

j) Tumia – ndi- pamoja na viashiria vya ngeli kujaza pengo (Al 2)

(i) Wewe _____ ninayekufuta.

(ii) Nyingi _____ mnaoongoza.

k) Andika kinyume cha;

(i) Tandaza zulia kubwa (Al 1)

(ii)Mtweke mchukuzi mzigo huu. (Al 1)

l) Vitaje vipashio vitatu muhimu vya lugha. (Al 3)

m) Andika kwa msemo wa taarifa (Al 3)

“Lo! Umeweza kuubeba mzigo huu pekeyo?”

Mama alishangaa.

n) Tumia “O” rejeshi katika sentensi zifuatazo (al 2)

(i) Mikeka ambayo hufumwa Turkana ni madhubuti.

Uchunguzi ambao wangojewa umewadia.

o) Eleza matumizi ya “KU” katika sentensi hii.

Kucheza huku hakufai (AL 2)

p) Tofautisha nyakati (Al 2)

(i) Akimbia

(ii) Anakimbia

q) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii (Al 2)

Anamolala mna viroboto wengi.

ISIMU JAMII

Wananchi huoyee! Kiti juu!

Leo ni ile siku tuliyoingojea kwa hamu na ghamu. Imefika, haijafika? Naona nyuso zenu zinatangaza ushindi wa kiti.Naona hamjadanganywa na mpinzani wangu atembeaye na kupaka matope jina langu. Ni nani hajaona maendeleo niliyoleta hapa tangu mnichague nyinyi wenyewe? Kwa hiari yenu mlinichagua niwe mtumishi wenu nami niko chini ya nyayo zenu. Sasa huu ni wakati mwingine naomba, nawasihi, nawanyenyekea mnikabidhi tena hilo jukumu zito la kuwatumikia.

Mpinzani anawapa pesa kuwahonga, ela nasema kula kwa mpinzani wangu, lakini kura ni kwangu jamani. Kiti juu!

Maswali

A Taja muktadha wa matumizi ya lugha hii (Al 2)

B Eleza sifa za lugha hii . (Al 4)

C Jadili mbinu za lugha zilizotumika katika lugha hii . (Al 4)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA 3
KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

a) - Kiswahili hakitoshelezi mahitaji yote ya mawasiliano. (al. 1)

b) - Hakuelewa maana na matumizi ya msemo huo ambao kwa hakika uliunga mkono mjadala. (al.2)

c) - Wapinzani walikuwa na ujinga na kama wangeelimishwa , wangeibuka washindi katika mjadala. (Al.4)

d) - Matumizi bora ya lugha (mbwa mdomo wazi) (alama 1)

e) - Barua meme /pepe /mdahalishi
- Satalaiti za mawasiliano
- Simu rununu /tamba/sogevu
- Nukulishi /kipepesi (faksi) (zozote tatu) (alama 3)

f) i) Yawezekana
ii) Ushahidi
iii) Kutowezekana

(al.3)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA MUHTASARI

a) - Mambo muhimu anayozungumizia mwandishi katika aya ya pili na tatu.

Sababu ziletazo maafa barabarani ni uendeshaji kasi.

Madereva kung'oa vidhibiti mwendo

Hawarekebishi mikanda ya usalama.

Hawayapeleki magari kukaguliwa.

Hawatekelezi kanuni za ukaguzi.

Hutegemea kuhonga askari.

Madereva wa malori na trela ni walevi.

Barabara za lami kuchimbika.

Zisizokuwa na lami kuharibika zaidi.

Serikali ifanyie ukarabati. (zozote 7x1=7)

b) 1. Maafisa wa usalama ni wafisadi zaidi.

2. Huchangia kuongezeka kwa vifo barabarani.

3. Mwananchi anauwezo wa kukomesha ufisadi .

4. Anayetoa hongo na anayepokea wapelekwe kwenye kituo cha kukabiliana na ufisadi.

Waadhibiwe vikali, ufisadi utaisha.

Elimisha mwananchi kuhusu haki yake.

Izilainishe sekta zote. (zozote 5x1=5)

KUTAHINI -

Makosa ya hijai (6 x ½ =3)

Makosa ya sarufi kila kosa linapojitokeza aondolewe (½ alama)

MWONGOZO

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Nimewahi kitenzi kisaidizi ✓1 Kumkumbusha kitenzi kikuu. ✓1 (al. 2)

b) i) Alinunua Marashi maua machozi maombi *n.k* ya pemba. ✓1

ii) Kuzaliwa kwa kristo kuliwakasirisha. ✓1

iiii) Kapsabet ni mji mkuu.
Bungoma ✓1

Sudan

Karanja.

i) Dhamini – chukulia mtu ahadi ya kutimiza jambo / toa pesa mahakamani ili mshtakiwa aachiliwe. (al.1)

ii) Thamini- Tia maanani / heshimu au tia gharama au bei ya kitu. (al.1)

d) i) Lo! Siamini…….

Kumbe! Alikuwa…….

ii) Parandesi // [ ]- Hutumiwa kufungia herufi kubwa za alphabet.

Kubaimsha sauti za lugha / vitamkwa.

Mf /a/ /p/

e) - t (al.1)

d (al.1)

f) - Maisha ya upweke (al.1)

g) - Ja - jiana

- pa - peana

h) - La -kiingizi *m.f La! Siji*

- -kitenzi m.f Amekula . zozote 2 x 1 = 2

-Kivumishi cha ‘A’ unganifu *m.f Gari la kubebea*

i) - Kutukuza, tukuka tukuzana 1 x 1 = 1

- Chumbia, chumbiana 1 x 1 = 1

j) - Ndiye Al. 1)

- Ndio Al. 1)

k) i) Tandua zulia ndogo (kubwa) Al.1)

ii) Mtue mchukuzi mzigo huu.

l) - Sauti

- Silabi } zozote 3 x 1 = 3

- Neno

- Sentensi.

m) - Mama alishangaa <u>kuwa</u> alikuwa /nilikuwa ameweza /nimeweza

kuubeba mzigo huo peke yake /yangu.

n) i) Mikeka ifumwayo Turkana ni madhubuti. Al.1)

ii) Uchunguzi ungojewao umewadia. Al.1)

o) - Ku- Mwanzoni mwa nomino ngeli ya ku. Al.1)

Kukanusha kwa wakati uliopo Al.1)

p) i) Daima / kila mara. Al.1)

ii) Wakati uliopo Al.1)

q) - Anamolala mna viroboto wengi

huru tegemezi

4. Mwongozo wa isimu jamii

a) - Mwanasiasa anagombea kiti cha uwakilishi labda bungeni.

Anawaomba waashi kumpa kura zao. zozote 2 x 1 = 2

b) - Unyenyekevu

- Kuomba
- Kujisifu/Kujitapa
- Kushawishi /ahadi
- Inaendelezwa katika nafsi ya kwanza –ni zozote 4 x 1 = 4

c) - Chuku

- Tanakali ya sauti
- Takriri
- Balagha zozote 4 x 1 = 4
- Viingizi ***(kila hoja alama moja)***

KISWAHILI KARATASI 4

102/2

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

UFAHAMU

Soma Taarifa Ifuatayo Kisha Ujibu Maswali

Nidhamu kwa vijana ni jambo ambalo tangu zamani limekuwa likipigiwa makelele sana. Kwa kuwa maisha yanazidi kuwa na mabadiliko sana na vijana wanasoma na kuona mengi. Inafaa watu hawa kukanywa kila wakati, bila ya kufanya hivyo , wataharibika zaidi.

Wengine kwa uhayawani unaowapanda vichwani mwao wanaweza hata kufikiria kuwa wazazi walio nao ni ovyo na labda sio waliowazaa. Hata kama ndio waliowazaa wanadai kuwa wao hawakuomba kuzaliwa na wazazi kama hao.

Wengine huibia wazazi wao au huwatafutia wezi. Wengine huwashika wazazi wao kabali au huwatisha. Isitoshe kuna, wanaoshikana miereka na wazazi . Hakuna mzazi anayeketi na kuomba kuzaa mtoto atakayemuambua mbele ya watu kiasi hicho .

Wanapokanywa juu ya mienendo ya kutembea na marafiki wabaya, wao hufura kama andazi lililoamuliwa kwa hamira nyingi. Hawatulii na kusikiliza mawaidha ila wao hujiona bora kuliko hata wazazi wa ndugu , wamesahau kuwa damu ni nzito kuliko maji na hata iwe vipi, mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

Licha ya maovu ya wanao , wazazi mara nyingi hawana kinyongo na wanao. Mzazi hushikwa na uchungu wake wa uzazi. Hujaribu juu chini kumsaidia mwanaye dhidi ya shida yoyote. Mzazi huguna kimoyomoyo na kujisemea ndio, asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Kila siku vijana hutaka kuvutia ngozi kwao. Badala ya kutumia maneno yenye nyama ya ulimi, wao ni kufoka tu kama chungu cha pure kilichochochelewa moto mwingi.

Unyenyekevu , bidii, heshima, shukrani, usaidizi wema na kuwa waelewa hali za wazazi wao. Kuwatenda kila jambo waliwezalo kwa mioyo mikunjufu. Maneno matamu humtoa nyoka pangoni. Ukali wote unaofikiriwa upo kwa wazazi hautakuwepo tena. Suluhisho litapatikana katika kila tatizo na watu wataishi kwa amani

Vijana pia wasisahau Mungu, Dini hubadilisha nyoyo za vijana wanaoanza kuingiwa na maovu. Vijana nao wana wajibu wa kujisaka na kujikosoa . Wazazi nao hawana budi kuketi na kuona vipi wanavyoweza kuwaelewa na kuwarekebisha vijana badala ya kutoa balaghumu zao; Wawaelekeze.

Walimu nao kwa vile hawawezi kujitoa katika hali hii ya urekebishaji wa tabia. Inatakiwa washirikiane na wazazi katika kuelekeza, kuelimisha , kurekebisha na hata kupongeza vijana kwa kitendo kifaacho. Adhabu zinapotolewa, Zitolewe baada ya vijana kuyaelewa makosa yao. Adhabu zilingane na uzito wa makosa.

Watoto nao wajifunze kuyakubali makosa yao, wawe wanyenyekevu na waombe msamaha

Mwana aliyeongoa ni mfano bora wa vijana wengine. Wazazi, walimu na majirani humwonea mtoto huyo fahari. Kila anapopita watu humsemesha vizuri . Anapopata shida, kila mtu hujitolea mhanga kumsaidia. Mtoto mzuri hudumisha dhima ya wazazi katika jamii. Lakini mbaya hufanya wazazi kudharauliwa. Tabia nzuri humjenga mtu maishani.

Ni juu ya kila kijana kuujua wajibu wake. Akijitia kifua mbele ajue wazi kuwa sikio halipiti kichwa na asipoyashika anayokatazwa na wakuu atakiona kilichomkosesha kuku matiti.

Ulimwengu ni hadaa na tena ni shujaa ukicheza nao, utakuwa kama mwenda wazimu anayepiga ukutani . Si vizuri kujiponza.

MASWALI

Taja mifano minne ya matendo ya vijana wabaya kwa kuzingatia taarifa (alama 2)

Ni mambo yapi yanayosababisha utovu wa nidhamu (alama 3)

Walimu na wazazi wanahusikaje katika kurekebisha mienendo ya vijana ? Eleza (alama 3)

d) Ni masuluhisho gani yanayotolewa ili kuimarisha tabia za vijana

e) Kwa nini kuna haja ya kurekebisha hasa vijana

f. Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika habari

i) Kuvutia ngozi kwao

ii) Kumwonea fahari

iii) Kuzozana

iv) Uhayawani

v) Majaliwa

vi) Kujisaka na kujikosoa

½ x 6 = al 3

SEHEMU B UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali unayoulizwa

Nchi zinazoendelea hukubwa na matatizo mengi mathalan kama umaskini, kutokuwepo kwa miundombinu ifaayo, uongozi potofu, sera mbazo hazifai na kadhalika . Tatizo mojawapo ambalo limekuwa sugu katika mataifa mengi ni lile la mrundikano wa mahabusu . Mahabusu hawa ni wengi kutokana na sababu mbili kuu.

Kwanza , kuwepo kwa nafasi ndogo katika magereza yaliyomo katika nchi Fulani. Pili, suala la kuwepo kwa mahabusu wengi huweza kwenda sambamba na mrundikano wa kesi. Hii ina maana kuwa kesi zao hazijasikilizwa . Baadhi ya kesi huchukua muda mrefu kusikilizwa kutokana na muda mrefu wa kufanywa upelelezi na uchunguzi unaohusika hasa katika kesi za jinai.

Muda huu unaweza kuwa mrefu kutokana na uzembe wa wanaohusika na uchunguzi na upelelezi huo. Lakini zipo kesi nyingine ambazo hazihitaji uchunguzi mrefu au muda mrefu ili kukamilika . Kukawizwa kwa kesi kama hizi (na kuishia kusota magerezani kama wanaohusika) hutokana na kutokuwako kwa uwajibikaji ufaao kwa wanaopaswa kufanya uchunguzi huo. Zipo hali ambapo kosa au uhalifu unafanyika mkosaji au mtuhumiwa anakamatwa na ushahidi upo. Licha ya hali hii, si ajabu kumwona anayehusika akibakia gerezani bila kuhukumiwa . Wengine huweza kubakia huko hata kwa miaka na inaishia kuthibitishwa kuwa mtuhumiwa au mshukiwa hana hatia kabisa.

Bila shaka zipo kesi nyingine ambazo ni zenye utata. Hizi ni kesi ambazo huhitaji muda kufanyiwa uchunguzi . Hata hivyo , upo umuhimu wa kuhakikisha kwamba upelelezi na uchunguzi wa kesi za aina hii una mipaka yake pia. Ni muhimu kwa kuwa ikiwa anayehusika amecheleweshwa kwa kiasi fulani haki zake kama binadamu zitakiukwa. Kesi ambazo hazina matatizo zinapaswa kuchangamkia na kumalizwa haraka . Kesi za aina hii zingesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano na mrundikano kwenye korokoro na jela zetu.

Pana umuhimu pia wa uchunguzi kufanywa ili kuhakikisha kuwa ucheleweshaji wa kesi hautokani na sababu nyinginezo kama rushwa, kisasi utepetevu au hata uzembe . Aidha serikali inapaswa kuhakikisha wapo mahakimu na majaji wa kutosha kuweza kuzisikiliza kesi kwa wakati ufaao. Ni matumaini ya wengi kuwa wanaohusika na masuala ya sheria watautilia maanani ushauri huu na

kuharakisha kesi ambazo ziko wazi . Hata hivyo , ifahamike kuwa kuharakishwa huko hakupaswi kuwa msingi wa udhalilishwaji wa wanaohusika . Kwa vyovyote vile haki na sheria lazima zitawale matendo yetu.

MASWALI

a) Kwa maneno (45 – 50) fupisha aya ya pili na ya tatu

Alama 7

Nakala chafu (Alama 1 ya utiririko)

Nakala safi

b) Mwandishi alikuwa na ujumbe upi katika aya ya mbili za mwisho? Maneno 40. (alama 8)

(alama 7)

(alama 1 ya utiririko)

Nakala chafu

Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA C

a) Ainisha mofimu za maneno yafuatayo

i) Mtoto……

ii) Kuku ……. al 2

b) **Andika maneno haya katika hali ya udogo**

i) Kisu ……..

ii) Sabuni ……..

al 2

c) **Kanusha sentensi hizi**

(i) AKija tutaonana

ii) Ningalikuwa na uwezo ningalinunua ndege (alama 2)

d) **Weka vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeka** (Ala 3)

i) Cha……

ii) La ……

iii) Nywa ……

e) **Ainisha viambishi katika neno**

Kikulacho……..al 2

f) **Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo** Al 2

i) Sasa ……..

ii) Saza……..

g) **Changanua kwa Njia ya Mishale** al 4

Mimi sipendi watu wanaopigana

h) **Zipange nomino hizi katika ngeli zao** Al 2

i) Unga ……iii) Mkoba……

ii) Tupa ……iv) Kwake …….

i) **Bainisha aina za nomino katika sentensi zifuatazo** Al 3

i) Joshua huzungumza Kiswahili vizuri

ii) Maji mengi yamemwagika

j) **Ziandike Sentensi Hizi Kwa Wingi** **Al 2**

i) Wewe uliajiriwa juzi

ii) Ndoo hii imetoboka

k) Tambulisha viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsi viambata katika sentensi hizi al 3

i) Mimi nitakuwa seremala

ii) Akiwa rubani , ataruka kwa ndege

l) **Sahihisha sentensi zifuatazo** **AL 3**

i) Umemwona mwenye ameiba ndizi yangu?

ii) Kiatu kile kimenunuliwa ni chake

iii) Uji iliyopikwa imeiva

m) Andika katika usemi wa taarifa

" Tusipofanya kazi yetu kwa bidii na kujitegemea , tutaendelea kuwa watumwa katika nchi yetu"

Mwalimu alisema Al 2

n) **Unda vitenzi kutokana na majina haya** Al 2

i) Mtukufu ……..…….

mchumba ……

o). **Onyesha shamirisho kipozi na / au shamirisho kitondo katika sentensi zifuatazo** al 4

i) Mwalimu alitupa vitabu viwili

ii) Ann alisomewa gazeti na wanafunzi wenzake.

p) **Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya-enye na-enyewe** al 2

ISIMU JAMII D

1 a) Lugha ya taifa ni nini?

al 1

b) Eleza sifa mbili za lugha ya taifa?

al 2

C) Ni matatizo gani yanayokumba Kiswahili nchini Kenya? al 4

d) Matatizo haya yameshughulikiwa vipi? al 3

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA 4
KISWAHILI 102/2

UFAHAMU

Soma Taarifa Ifuatayo Kisha Ujibu Maswali

Nidhamu kwa vijana ni jambo ambalo tangu zamani limekuwa likipigiwa makelele sana. Kwa kuwa maisha yanazidi kuwa na mabadiliko sana na vijana wanasoma na kuona mengi. Inafaa watu hawa kukanywa kila wakati, bila ya kufanya hivyo , wataharibika zaidi.

Wengine kwa uhayawani unaowapanda vichwani mwao wanaweza hata kufikiria kuwa wazazi walio nao ni ovyo na labda sio waliowazaa. Hata kama ndio waliowazaa wanadai kuwa wao hawakuomba kuzaliwa na wazazi kama hao.

Wengine huibia wazazi wao au huwatafutia wezi. Wengine huwashika wazazi wao kabali au huwatisha. Isitoshe kuna, wanaoshikana miereka na wazazi . Hakuna mzazi anayeketi na kuomba kuzaa mtoto atakayemuambua mbele ya watu kiasi hicho .

Wanapokanywa juu ya mienendo ya kutembea na marafiki wabaya, wao hufura kama andazi lililoamuliwa kwa hamira nyingi. Hawatulii na kusikiliza mawaidha ila wao hujiona bora kuliko hata wazazi wa ndugu , wamesahau kuwa damu ni nzito kuliko maji na hata iwe vipi, mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

Licha ya maovu ya wanao , wazazi mara nyingi hawana kinyongo na wanao. Mzazi hushikwa na uchungu wake wa uzazi. Hujaribu juu chini kumsaidia mwanaye dhidi ya shida yoyote. Mzazi huguna kimoyomoyo na kujisemea ndio, asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Kila siku vijana hutaka kuvutia ngozi kwao. Badala ya kutumia maneno yenye nyama ya ulimi, wao ni kufoka tu kama chungu cha pure kilichochochelewa moto mwingi.

Unyenyekevu , bidii, heshima, shukrani, usaidizi wema na kuwa waelewa hali za wazazi wao. Kuwatenda kila jambo waliwezalo kwa mioyo mikunjufu. Maneno matamu humtoa nyoka pangoni. Ukali wote unaofikiriwa upo kwa wazazi hautakuwepo tena. Suluhisho litapatikana katika kila tatizo na watu wataishi kwa amani

Vijana pia wasisahau Mungu, Dini hubadilisha nyoyo za vijana wanaoanza kuingiwa na maovu. Vijana nao wana wajibu wa kujisaka na kujikosoa . Wazazi nao hawana budi kuketi na kuona vipi wanavyoweza kuwaelewa na kuwarekebisha vijana badala ya kutoa balaghumu zao; Wawaelekeze.

Walimu nao kwa vile hawawezi kujitoa katika hali hii ya urekebishaji wa tabia. Inatakiwa washirikiane na wazazi katika kuelekeza, kuelimisha , kurekebisha na hata kupongeza vijana kwa kitendo kifaacho. Adhabu zinapotolewa, Zitolewe baada ya vijana kuyaelewa makosa yao. Adhabu zilingane na uzito wa makosa.

Watoto nao wajifunze kuyakubali makosa yao, wawe wanyenyekevu na waombe msamaha

Mwana aliyeongoa ni mfano bora wa vijana wengine. Wazazi, walimu na majirani humwonea mtoto huyo fahari. Kila anapopita watu humsemesha vizuri . Anapopata shida, kila mtu hujitolea mhanga kumsaidia. Mtoto mzuri hudumisha dhima ya wazazi katika jamii. Lakini mbaya hufanya wazazi kudharauliwa. Tabia nzuri humjenga mtu maishani.

Ni juu ya kila kijana kuujua wajibu wake. Akijitia kifua mbele ajue wazi kuwa sikio halipiti kichwa na asipoyashika anayokatazwa na wakuu atakiona kilichomkosesha kuku matiti.

Ulimwengu ni hadaa na tena ni shujaa ukicheza nao, utakuwa kama mwenda wazimu anayepiga ukutani . Si vizuri kujiponza.

MASWALI

Taja mifano minne ya matendo ya vijana wabaya kwa kuzingatia taarifa (alama 2)

Ni mambo yapi yanayosababisha utovu wa nidhamu (alama 3)

Walimu na wazazi wanahusikaje katika kurekebisha mienendo ya vijana ? Eleza (alama 3)

d) Ni masuluhisho gani yanayotolewa ili kuimarisha tabia za vijana

e) Kwa nini kuna haja ya kurekebisha hasa vijana

f. Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika habari

i) Kuvutia ngozi kwao

ii) Kumwonea fahari

iii) Kuzozana

iv) Uhayawani

v) Majaliwa

vi) Kujisaka na kujikosoa

½ x 6 = al 3

SEHEMU B UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali unayoulizwa

Nchi zinazoendelea hukubwa na matatizo mengi mathalan kama umaskini, kutokuwepo kwa miundombinu ifaayo, uongozi potofu, sera mbazo hazifai na kadhalika . Tatizo mojawapo ambalo limekuwa sugu katika mataifa mengi ni lile la mrundikano wa mahabusu . Mahabusu hawa ni wengi kutokana na sababu mbili kuu.

Kwanza , kuwepo kwa nafasi ndogo katika magereza yaliyomo katika nchi Fulani. Pili, suala la kuwepo kwa mahabusu wengi huweza kwenda sambamba na mrundikano wa kesi. Hii ina maana kuwa kesi zao hazijasikilizwa . Baadhi ya kesi huchukua muda mrefu kusikilizwa kutokana na muda mrefu wa kufanywa upelelezi na uchunguzi unaohusika hasa katika kesi za jinai.

Muda huu unaweza kuwa mrefu kutokana na uzembe wa wanaohusika na uchunguzi na upelelezi huo. Lakini zipo kesi nyingine ambazo hazihitaji uchunguzi mrefu au muda mrefu ili kukamilika . Kukawizwa kwa kesi kama hizi (na kuishia kusota magerezani kama wanaohusika) hutokana na kutokuwako kwa uwajibikaji ufaao kwa wanaopaswa kufanya uchunguzi huo. Zipo hali ambapo kosa au uhalifu unafanyika mkosaji au mtuhumiwa anakamatwa na ushahidi upo. Licha ya hali hii, si ajabu kumwona anayehusika akibakia gerezani bila kuhukumiwa . Wengine huweza kubakia huko hata kwa miaka na inaishia kuthibitishwa kuwa mtuhumiwa au mshukiwa hana hatia kabisa.

Bila shaka zipo kesi nyingine ambazo ni zenye utata. Hizi ni kesi ambazo huhitaji muda kufanyiwa uchunguzi . Hata hivyo , upo umuhimu wa kuhakikisha kwamba upelelezi na uchunguzi wa kesi za aina hii una mipaka yake pia. Ni muhimu kwa kuwa ikiwa anayehusika amecheleweshwa kwa kiasi fulani haki zake kama binadamu zitakiukwa. Kesi ambazo hazina matatizo zinapaswa kuchangamkia na kumalizwa haraka . Kesi za aina hii zingesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano na mrundikano kwenye korokoro na jela zetu.

Pana umuhimu pia wa uchunguzi kufanywa ili kuhakikisha kuwa ucheleweshaji wa kesi hautokani na sababu nyinginezo kama rushwa, kisasi utepetevu au hata uzembe . Aidha serikali inapaswa kuhakikisha wapo mahakimu na majaji wa kutosha kuweza kuzisikiliza kesi kwa wakati ufaao. Ni matumaini ya wengi kuwa wanaohusika na masuala ya sheria watautilia maanani ushauri huu na kuharakisha kesi ambazo ziko wazi . Hata hivyo , ifahamike kuwa kuharakishwa huko hakupaswi kuwa msingi wa udhalilishwaji wa wanaohusika . Kwa vyovyote vile haki na sheria lazima zitawale matendo yetu.

MASWALI

a) Kwa maneno (45 – 50) fupisha aya ya pili na ya tatu

Alama 7

Nakala chafu (Alama 1 ya utiririko)

Nakala safi

b) Mwandishi alikuwa na ujumbe upi katika aya ya mbili za mwisho? Maneno 40. (alama 8)

(alama 7)

(alama 1 ya utiririko)

Nakala chafu

Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA C

a) Ainisha mofimu za maneno yafuatayo

i) Mtoto……

ii) Kuku ……. al 2

b) **Andika maneno haya katika hali ya udogo**

i) Kisu ……..

ii) Sabuni ……..

al 2

c) **Kanusha sentensi hizi**

(i) AKija tutaonana

ii) Ningalikuwa na uwezo ningalinunua ndege (alama 2)

d) **Weka vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeka** (Ala 3)

i) Cha……

ii) La ……

iii) Nywa ……

e) **Ainisha viambishi katika neno**

Kikulacho……..al 2

f) **Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo** Al 2

i) Sasa ……..

ii) Saza……..

g) **Changanua kwa Njia ya Mishale** al 4

Mimi sipendi watu wanaopigana

h) **Zipange nomino hizi katika ngeli zao** Al 2

i) Unga …….iii) Mkoba……

ii) Tupa ……iv) Kwake …….

i) **Bainisha aina za nomino katika sentensi zifuatazo** Al 3

i) Joshua huzungumza Kiswahili vizuri

ii) Maji mengi yamemwagika

j) **Ziandike Sentensi Hizi Kwa Wingi** **Al 2**

i) Wewe uliajiriwa juzi

ii) Ndoo hii imetoboka

k) Tambulisha viwakilishi nafsi huru na viwakilishi nafsi viambata katika sentensi hizi

al 3

i) Mimi nitakuwa seremala

ii) Akiwa rubani , ataruka kwa ndege

l) **Sahihisha sentensi zifuatazo** **AL 3**

i) Umemwona mwenye ameiba ndizi yangu?

ii) Kiatu kile kimenunuliwa ni chake

iii) Uji iliyopikwa imeiva

m) Andika katika usemi wa taarifa

“ Tusipofanya kazi yetu kwa bidii na kujitegemea , tutaendelea kuwa watumwa katika nchi yetu”

Mwalimu alisema Al 2

n) **Unda vitenzi kutokana na majina haya** Al 2

i) Mtukufu ……..…….

mchumba ……

o). **Onyesha shamirisho kipozi na / au shamirisho kitondo katika sentensi zifuatazo** al 4

i) Mwalimu alitupa vitabu viwili

ii) Ann alisomewa gazeti na wanafunzi wenzake.

p) **Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya-enye na-enyewe** al 2

ISIMU JAMII D

1 a) Lugha ya taifa ni nini?

al 1

b) Eleza sifa mbili za lugha ya taifa?

al 2

C) Ni matatizo gani yanayokumba Kiswahili nchini Kenya? al 4

d) Matatizo haya yameshughulikiwa vipi? al 3

KISWAHILI I
SEHEMU YA KWANZA

1. Chagua mojawapo ya mazao yafuatayo na ueleze uzalishaji wake tangu kutayarisha shamba hadi kuvunwa.
   (a) Mahindi
   (b) Nyanya

2. Ganga ganga za mganga humlaza mgonjwa na matumaini.

3. Siku yangu ya kwanza katika shule ya upili.

4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo:
   " … dunia kweli wakati wa sasa imefikia kilele cha maendeleo ya teknolojia."

KISWAHILI I
SEHEMU YA PILI:

UFAHAMU:
Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali:

Mwangeka Mwachoni alizaliwa mwaka wa 1930 katika tarafa ya Mwanda, Wilaya ya Taita-Taveta. Angalikuwa hai leo bila shaka angalikuwa mmoja wa watu mashuhuri wenye kuheshimiwa kwa ujasiri wao.

Mwangeka alipata taabu mno utotoni wake kwa sababu ya malezi ya shida ya wazazi wake ambao walishindwa hata kumpeleka shule. Juu ya hivyo aliweza kuinuka na kuwa kijana mahiri sana tena mkakamavu na mchanga-mfu. Alikuwa akiwatii wazazi wake na kuwaenzi. Alijitwika jukumu la kuiangalia ile milki yao ndogo waliyokuwa nayo na kuwatumikia bila kinyongo. Ustadi aliokuwa nao Mwangeka umeweka kumbukumbu ya vitendo vya ushujaa wake wakati angali ni mdogo. Wakati huo, kila siku alikuwa akichunga ng'ombe wa baba yake milimani kulikokuwa na hatari za kila namna za wanyama wa mwitu. Siku moja alipowapeleka ng'ombe wao malishoni aliwaona simba wawili katika mlima Vuma waliotaka kuwashambulia wale ng'ombe. Mwangeka alipambana nao kwa uta na mshale na akaweza kuwaua. Hapo ndipo sifa zake za ujasiri ziliposambaa Taita nzima.

Mwangeka alikuwa mtu mwenye hekima na busara nyingi na alikuwa mwenye maarifa ya mambo mengi ya ajabu. Mojawapo ya mambo aliyoyajua ni vipi kajipinga na kujihami na shari za maadni wasiweze kumwona au kumjua alipo na hali yeye amewakabili na kuwatazama. Basi alipofika umri wa miaka ishirini na tano alianza kuwa mashuhuri na sifa zake zilizagaa kila mahali. Wakati huo alikuwa amekwisha oa. Alimwoa mwanamke aitwaye Magema, bibi ambaye mwanzo wa kuolewa alionyesha hubo nyingi kwa mumewe. Lakini baada ya miaka michache alianza kubadilika hulka na kuwa na umbeya na udadisi mwingi. Kila mara alikuwa akimsaili mumewe kuhusu ushujaa wake na mengi mengine yasiyostahili kuulizwa, bali mradi aelezwe tu. Alikuwa akistaajabu kumwona mumewe akiweza kuishi msituni kwa muda wa mwezi mzima bila chakula, na vile alivyoweza kwenda kwa miguu kutoka Kasigau mpaka Mwanda, mwendo wa kilomita mia mbili, bila kuchoka. Pia, ilikuwa ikistaajabisha vile alivyoweza kupotea asionekane na maadui zake (ambao wakati huo walikuwa ni wazungu) akiwacha nyuma kivuli chake ambacho ndicho kikiwashambulia na kuwaua maadui hao.

Siku moja bibi alimbembeleza sana mumewe amweleze maarifa na miujiza atumiayo, lakini Mwangeka alikataa kabisa kumdokezea habari hiyo. Mwishowe kero lilizidi na Mwangeka hakuweza tena kumkatalia.

Aliona heri amweleze lakini alimkanya asiweze zabizabina na kumweleza mtu yeyote, kwani hiyo ilikuwa siri yake. Akitoa siri hiyo kumwambia mtu, maisha yake yatakuwa hatarini, mahasimu zake wakikipiga kivuli chake.

Mwangeka alifanya kazi kubwa katika kuupigania uhuru wa Kenya. Aliwafukuza wazungu na kuwaua wengi. Huu ndio wakati ambapo Taita, na Kenya kwa jumla, ilipomtambua Mwangeka kuwa ni kiongozi asiye na kicho, aliyejitolea maisha yake yote kwa ajili ya nchi yake. Yeye ndiye aliyekianzisha chama cha vijana wa kitaita kilichopigania usawa wa wataita. Alitembelea sehemu nyingi za Kenya na akakutana na Jemadari Dedan Kimathi, mmoja wa viongozi wa Mau Mau, wapiganaji wa vita vya uhuru. Viongozi hao wawili walizungumza na kushauriana namna ya kupambana na taabu zilizo wakabili na wakaahidiana kwamba watakuwa wakitembeleana mara kwa mara.

Huku nyuma nyumbani kwa Mwangeka mambo hayakuwa mema kama alivyofikiria. Baada ya yeye kuondoka wazungu wawili walifika na kumbembeleza mkewe awaeleze jinsi Mwangeka alivyokuwa akifanya. Kwanza mkewe alikataa kuwaeleza lakini baada ya kupewa gunia moja la mchele na shilingi kumi pamoja na kuahidiwa mambo mema kadha siku za mbele, aliwaeleza siri zake zote!

Ilikuwa usiku, tarehe 23 Machi 1966, Mwangeka alipoonekana amelala juu ya jabali kubwa, maiti, kiwiliwili chake kiasi cha maili tatu hivi kutoka kivuli chake.

(a) Kisa gani kilimfanya Mwangeka kusifiwa kwa ujasiri katika Taita? (alama 2)
(b) Eleza sifa moja ya ajabu ya Mwangeka ambayo ilikuwa ikiwakanganya maadui zake. (alama 2)
(c) Eleza mabadiliko ya tabia ya mke wa Mwangeka. (alama 3)
(d) Eleza sifa za Mwangeka zisizopungua tano. (alama 3)
(e) Wale wazungu wawili walifanya nini hata Mwangeka mwishowe akauawa?(alama 2)
(f) Mwangeka alipokufa alikuwa kijana au mzee? Toa sababu. (alama 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa namna yalivyotumika katika taarifa.(alama 6)
    (i) Mahiri: _____
    (ii) Bila kinyongo: _____
    (iii) Hulka: _____
    (iv) Mahasimu: _____
    (v) Akijitwika jukumu: _____
    (vi) Akimsaili: _____

SEHEMU YA B:
MUHTASARI:

Mzee Kondoo: Wenyeji wa kijiji cha maendeleo; mabibi na mabwana pokeeni salamu zangu na shukrani kwa kuhudhuria mkutano huu. mimi pamoja na wazee wenzangu tuliamua kwa kauli moja kuwaita nyote hapa ili kujadili maendeleo ya kijiji chetu. Jambo linalotukera sisi wazee ni kwamba hali ya kijiji chetu inazidi kuzoroteka. Kijiji chetu kiliitwa maendeleo sisi wazazi wake tulipokuwa na rai ya kuleta maendeleo. Wake kwa waume tulijifunga vibwebwe na kwa kweli juhudi zetu zilitoa matunda mema. Sasa nguvu zimeanza kutuishia; leo tupo, kesho tutakuwa hatupo. Ninyi ndio mtakaoshika usukani. Kama tunavyoona, mambo yakiendelea namna hii, watoto wenu wataishi maisha ya dhiki. Tungependa ninyi wenyewe mtueleze kwa nini kijiji maarufu cha maendeleo kinarudi nyuma badala ya

kuendelea mbele. Kila anayetaka kutoa hoja zake atapewa fursa ya kufanya hivyo. Lakini kwanza mzee mwenzangu ana machache ya kusema.

Rojo: Asante sana mzee Kondoo. Kwa upande wangu naona kwamba tumekuwa pweza kujipalia makaa na kwa mintaarafu hii, maendeleo ya kijiji chetu yakaanza kuzoroteka. Kwa ufupi, tunazaa watoto tusioweza kuwalea. Ni hivi majuzi tu tulipomkuta mtoto mmoja amezirai …

Jara: Wee! Kaa chini. Usituletee aibu hapa. Sisi ni watu wa kuheshimiwa. Ufahamu kwamba hukupewa fursa ili uanze kuchambua nyumba za wengine. Mungu mwenyewe alitoa amri kwamba watu wazae mpaka waijaze dunia.

Jilo: Mimi namwunga mkono Jara. Anayosema Rojo hayafai kuruhusiwa kuzungumzwa tena.

Mzee Kondoo: Hatukuwaita hapa mje mgombane. Rojo hajataja jina la mtu wala hajamaliza kutoa hoja zake. Endelea bwana Rojo.

Rojo: Nashukuru Mzee Kondoo. Ndugu, mimi nitatoa ule ukweli. Humu kijijini mwetu mna watoto ambao hawaendi shule. Kazi yao ni kuzurura kila mahali na kuokotaokota mali za watu. Hata huingia mashambani mwa watu wakaiba matunda, mihogo, mahindi na mazao mengine wakapeleka mijini kuuza. Mimi kitendo kama hiki nakilaani kwani ndicho kinachorudisha maendeleo ya kijiji chetu nyuma.

Uledi: Hayo usemayo ni kweli. Juzi walikuja usiku mwenyewe siko wakavunja mlango wakafagia nyumba yangu fyu! Vitendo vya vijana hawa vinadhihirisha ukosefu wa malezi bora. Mabwana na mabibi, mimi sipingi uzazi lakini yule azaaye atambue jukumu lake la kuwalea vizuri watoto hao hata kama ni ishirini: awalishe, awavishe, awatibu wawapo wagonjwa, awafunze tabia njema na kupelekwa shuleni ili wakuapo waweze kujimudu na kushirikiana nasi katika kuendeleza kijiji chetu.

Heri: Mabibi na mabwana mtaniwia radhi kwa vile ambavyo sina mke wala watoto. Hata hivyo sitasita kutoa maoni yangu. Wasemayo wenzetu ni ya kuungwa mkono. Watoto wakosao malezi bora ndio hatari katika kijiji chetu. Wakazi wa kijiji hiki wamekuwa waoga hata hawawezi kujenga maduka wakaendesha biashara zao humu.

Rojo: Mbali na uhalifu wa vijana wetu sisi watu wazima pia twafaa kulaumiwa. Kwanza tumeshindwa kutimiza wajibu wetu kwa ajili ya ulevi. Tumeshiriki ulevi hata kwamba hatudiriki makazini wala mwetu majumbani. Vipi tutadumisha nidhamu katika jamii zetu? Pia tusisahau kwamba ili kuwa na jamii ya kuimudu siku hizi hali ya maisha imepanda juu na tusipokuwa na busara yatatushinda.

Uledi: Zaidi ya hayo inatupasa tuzingatie miradi mbalimbali itakayotuletea maendeleo …

Maswali:

1. Kwa nini wazee walikereka kuona kijiji chao kikizoroteka? (maneno 15)(alama 3)
   NAKALA CHAFU
   NAKALA SAFI

2. Wanakijiji cha maendeleo wamekuwa pweza kujipalia makaa kwa vipi? (maneno 50) (alama 8)

   NAKALA CHAFU
   NAKALA SAFI

3. Uledi ana wazo gani kuhusu mpango wa uzazi? (maneno 15). (alama 2)
   NAKALA CHAFU
   NAKALA SAFI

4. Eleza mambo yanayozorotesha kijiji cha maendeleo? (maneno 50). (alama 7)
   NAKALA CHAFU
   NAKALA SAFI

3. SEHEMU YA C:
MATUMIZI YA LUGHA

(a) Andika kwa kinyume:
   (i) Nje kulikuwa kweupe. (alama 1)
   (ii) Mzizimo (alama 1)

(b) Eleza matumizi ya "po" katika sentensi hizi.
   (i) Mjomba aliniuliza "Je, sikukuambia kuwa akomeleapo mwenyeji nawe mgeni koma papo? (alama 2)
   (ii) Eleza matumizi ya "kwa" katika sentensi hii:
   Mwanariadha alijikaza kisabuni tulipomshangilia kwa nguvu. (alama 1)

(c) Akifisha sentensi zifuatazo:
   (i) lahaula sijui kama kazi hii itamalizika (alama 2)
   (ii) siku ya jumapili mwezi wa aprili mwaka huu tutaenda mombasa (alama 1)

(d) Eleza maana ya misemo hii :
   (i) Kulia ngoa. (alama 2)
   (ii) Kuwa mjango. (alama 3)

(e) Kamilisha methali hii:
   (i) Atupaye tope _____(alama 4)
   (ii) Cha mkufuu mwanafuu ha, na akila hu, _____(alama 5)

(f) Tumia kivumishi kwenye vifungo kukamilisha sentensi:
   (i) Tuleteeni ng'ombe yeyote _____ (-dogo) (alama 1)
   (ii) Ngoma _____, ndiyo iliyotakikana. (-le) (alama 1)

(g) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo uliyopewa:

(i) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ikiwa unatumia msumeno. (Anza: "Ni rahisi …)
(alama 2)

(ii) "Kuna chai?" Mtoto aliuliza. Maliza na …. Chai) (alama 2)

(iii) Tabasamu yake ilipotea haraka alipoambiwa kuwa alipatikana na hatia ya kuwa mlevi na kukosa adabu. (Anza Aliishiwa na ….)
(alama 2)

(h) Geuza sentensi zifuatazo katika <u>hali ya mazoea</u>:
(i) Mtoto unavyomlea ndivyo anavyokuwa. (alama 2)
(ii) Matunda yanayoiva ndiyo yanayotundwa. (alama 2)

(i) (a) Mke wa mwanao utamwitaje? (alama 1)
(b) Yohana na Selemani ni ndugu, pia wataitanaje? (alama 1)
(c) Msichana ambaye hajavunja ungo huitwaje? (alama 1)

(j) <u>Eleza muundo/mpangilio wa sentensi hii:</u>
Amenikasirisha (alama 3)

(k) <u>Tumia maneno haya katika sentensi.</u>
(a) Hapiki hapakui. (alama 2)
(b) Hana kazi hana bazi.

(l) <u>Tumia amba katika sentensi hii.</u>
Mtoto anayelia amepigwa na mwizi vibaya sana. (alama 1)

SEHEMU YA TATU
USHAIRI:

Soma shairi hili, kisha uyajibu maswali yanayofuata:

9. 1. Dunia yanishangaza, kwa mikiki na myujiza,
Yajaa sana kuwaza, ama nitajiumiza,
Kwa maovu kuigiza, nimejigeuza pweza,
Mola naomba ya jaza, nanuia kuwa mwema.

2. Utu uzima wangia, masoma namalizia,
Michezo yanizidia, rafiki wana udhia,
Sipati wala tulia, masomo sijafalia,
Mwenyewe najichukia, vitabu sijavishika.

3. Siku nazo zayoyoma, kesho nitasema nini?
Nitanena sikusoma, nitamdanganya nani?
Wazazi pesa wachoma, kunipeleka shuleni,
Kwa kuwa nimebaini, heri nitie bidii.

4. Mawi yamenizunguka, mungu wangu nibariki,
Kujiasa ninataka, nifanye yote ya haki,
Ningependa kuamka, utepetevu sitaki,
Nyuma sipendi kubaki, ningependa kufaulu.

5. Marafiki naeleza, kuwa nimeshachapuka,
   Habari nazieneza, wala msije kumaka,
   Ukweli ninawajuza, horomo nimeondoka,
   Uvivuni nimetoka, niondoeni kundini.

6 Panda nalipulizia, kwa wa hapa na wa kule,
   Nadhani nimesikia, mkazo natia shule,
   Ukunguni nasusia, nataka kusonga mbele,
   Sitaki zenu kelele, nidhamu naifwatile.

7. Leo nisipokazana, kesho nitakula nini?
   Nitawakidhije wana? Nitakuwa mtu duni!
   Riziki takuwa sina, nitaitwa mkunguni,
   Moto najipaliani? Heri nijikuze sasa.

8. Mtegemea cha ndugu, atakufa maskini,
   Ama atakuwa pwagu, aishie kifungoni,
   Kwa nini niote sugu, na kweli i hadharani,
   Sitajitia shimoni, nitayapenda masomo.

9. Baibai masahibu, msipende kunighasi,
   Nitavisoma vitabu, mitihani niipasi,
   Nigeuke mahabubu, na mtu aso muasi
   Hayana ya wasiwasi, yenu nyingi hayawani.

10. Jongoo nimemtupa, na mti wake pamoja,
    Sitataka tapatapa, ninaitafuta tija,
    Nyingi pigeni malapa, hatavishwa makoja,
    Kuna siku itakuja, mtakuja kuhiliki!

Maswali:

(a) Andika kichwa mwafaka kinachofaa kuelezea shairi hili. (alama 2)
(b) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu zako. (alama 2)
(c) Marafiki wa mwandishi wana tabia gani? (alama 4)
(d) Ni nini dhamira ya mtunzi? (alama 2)
(e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 5)
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi
   (i) Mikiki (ii) Kuyoyoma (iii) Mkunguni
   (iv) Panda (v) Sugu

10. <u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali :</u>

1. Ukitazama dunia, umbo lake huarifu,
   Kuwa imeandaliwa, wageni watukufu,
   Tayari kuwapokea, na mambo sufufu,
   Ndani yake yamejaa, viumbe kuwanadhifu.

2. Umbile huonyesha, namna ilivyotimu,
   Yangoja kukaribishwa, katika mastakimu,
   Yenye kila tamasha, machungu na matamu,
   Maisha yanapokwisha, huiacha inadumu.

3. Ajae ardhi hii, kutoka katika mimba,
   Mzizini au yai, au katika kitumba,
   Milki hakinai, ya mali wala mashamba,
   Mwisho wa uhai, kaburi lake jemamba.

4. Halii choyo kaburi, mtu uzima ukisha,
   La upana shubiri, urefu pima yatosha,
   Wala hadai fahari, tena hujifaharisha,
   Akiwa hai fikiri, anavyopenda tamasha.

5. Yalipo maziara, masikani ya maiti,
   Huonyesha ishara, na pengine tofauti,
   Dhaifu na bora, hawagombi hawateti,
   Wazima kila mara, Pato linawasalitia.

6. Mtu hashibi pato, hili huonyesha nini?
   Laonyesha kama pito, kuwa yumo safarini,
   Enda kuitika wito, bora usio kifani,
   Ambao kila mtoto, wa Adam hutamani.

7. Yumo katika safari, kila mwanadamu,
   Haraka au usiri, kwenda imelazimu,
   Epusha roho kahari, yake na Jahanamu,
   Iwe katika fahari, mwili ukiwa kuzimu.

Maswali:

(a) Pendekeza kichwa cha shairi hili. (alama 2)
(b) Mshairi amevitaja vitu aina ngapi vyenye uhai? Vitaje. (alama 4)
(c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 5)
(d) Eleza vina na mizani katika shairi hili. (alama 3)
(e) Eleza ujumbe wa mshororo:
"Halii choyo kaburi, mtu uzima ukishe." (alama 2)
(f) Onyesha vile uhuru wa kishairi ulivyotumiwa. (alama 4)

KISWAHILI I
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA:

1. Kila insha ina alama 20 - jumla 40.
2. Tumia mtindo ufuatao kwa kusahihisha.
   Maudhui - 5

Mtindo-	4	Tahajia -	3
Sarufi -	6		
Msamiati -	5		
	20		

MAUDHUI:
Kadiria maelezo anayotoa mwanafunzi kuhusu anwani. Angalia ikiwa ametaja hoja mwafaka na ikiwa amejibu swali; je:

1) Ametaja mada/hoja zote? - 5
2) Ametaja nusu? - 2 ½
3) Ametaja chini ya nusu? - 2
4) Hakutaja chochote - 0

Mtahini ana uhuru wa kukadiria alama kama atakavyoongozwa na majibu kutoka kwa mwanafunzi.

MTINDO:
Ni mpangilio wa insha - utangulizi, maelezo na mwisho. Ni mtiririko wa mawazo na namna mwanafunzi anavyowasilisha mawazo yake. Mtahini akadirie kulingana na jibu.

SARUFI:
Ni makosa ya sarufi ya lugha ya Kiswahili. Kila kosa litokeapo, alama (.5) huondolewa ambayo ni nusu alama. Kossa likirudiwa haliadhibiwi mara mbili. Usiondoe zaidi ya alama 6 yaani nusu 12.

MSAMATI:
Ni uafaka wa matumizi ya misamiati ya lugha. Ni uzito wa lugha ya mwanafunzi. Mtahini akadirie.

HIJAI:
Ni makosa ya uendelezaji ambayo huondolewa kutoka jumla ya alama aliyopata mwanafunzi. Usiondoe zaidi ya alama 3 yaani nusu 6.

MASWALI

1.(a) Mahindi
- Aeleze ni aina gani ya mimea, faida yake au matumizi yake kwa binadamu.
- Aeleze namna shamba linavyotakikana kutayarishwa halafu namna ya kupanda- kuongezea mbolea n.k.
- Utunzaji wa mahindi inapokuwa shambani hadi uvunaji - mitindo ya uvunaji.

(b) Nyanya - Mtindo ni huo wa hapo juu.
2,3,4 - Mtahini atasahihisha kulingana na majibu ya mwanafunzi maana majibu ni mbalimbali kulingana na chaguo la mwanafunzi.

SEHEMU YA PILI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA

Jinsi ya kutuza na kuadhibu makosa:

Ufahamu: (Muhtasari na matumizi ya lugha
Ondoa alama ½ kwa kila kosa la sarufi. Usiondoe zaidi ya nusu ya alama zote katika swali.
- Ondoa alama ½ kwa kila kosa la hijai, usiondoe zaidi ya nusu sita yaani alama tatu katika swali zima.

Kuadhibu makosa:
(i) Sarufi - adhibu makosa kumi na mbili ya sarufi. Kila kosa alama ½ 12 x ½ = 6.

(ii) - Tahajia - adhibu makosa kumi ya hijai, kila kosa alama ½ 10 x ½ = 5.
- Makosa ya hijai yanagusia mwendelezo kama paba badala ya baba.
- Kuunganisha mchezafibora - mchezaji bora.
- Kutenganisha - mwana sheria badala ya mwanasheria.

(iii) Mtiririko - pima alivyotiririsha hoja zake. Je, ni wastani? 1 ½ ju ya wastani ; 2 ½ au chini ya wastani (1). Usimpe sifuri (0) katika mtiririko.

(iv)Ikiwa mtahiniwa hakuelezea hoja kikamilifu, mpe nusu alama ya ile yote.

Mwongozo wa kusahihisha ufahamu:

(a) Jinsi alivyoweza kupambana na simba wawili waliotaka kuwashambulia ng'ombe wao katika mlima wa vuma na kuwaua.
(Maelezo kamili - alama 2)

(b) Sifa yake ya kuweza kujihami na kukikinga asionekane na maadui zake au kujulikana alikokuwa ilhali yeye angewakabili na kuwatazama. (alama 2)

(c) - Mbeleni alimpenda Mwangeka sana lakini baadaye tabia yake ikabadilika akaanza kuwa na umbeya huku akidadisi mumewe apate kujua mengi kumhusu.
- Alibadilika na kumsaliti mumewe kwa kutoboa siri kwa wazungu waliomwua Mwangeka, kwa hivyo alibadilika kutoka ile tabia yake ya kuaminiwa na mumewe kuwa mwaminifu na kuwa msaliti. (alama 5)

(d) Sifa za Mwangeka:
- Mahiri.
- Mkakamavu.
- Mchangamfu.
- Mtiifu kwa wazazi.
- Asiye na kingongo atendapo mema.
- Mwenye hekima na busara.
- Mwenye maarifa ya mambo mengi.
- Msiri.
- Mkombozi.
- Kiongozi shupavu. ***(alama ½ x 6 = 3)***

(e) Walimwendea mkewe Mwangeka na kumwuliza jinsi mumewe alivyokuwa akifanya. Alipojizuia kutoboa siri alihongwa kwa gunia moja la mchele na shilingi kumi na kuahidiwa mema siku za baadaye naye akaeleza siri ambayo ilisaidia kuuwawa kwa mumewe (Mwangeka).
(alama 2).

(f) Kijana kwa sababu alikuwa na miaka 36. Kwa hivyo mtu wa makamo mwenye nguvu. (alama 2)

(g) (i) Mahiri - mwenye ujuzi na hodari kufanya mambo, mwenye busara.
(ii) Bila kinyongo - bila chuki au uchungu.
(iii) Hulka - mwenendo au tabia.
(iv) Mahasimu - maadui.
(v) Alikitwika - alifanya wajibu huo bila kulazimishwa.
(vi) Akimsaili - Akimdadisi, akimhoji, akimwuliza - uliza maswali kwa minajili.
(alama 6)

Mwongozo wa kusahihisha muhtasari:

1. - Kilikuwa kikiongoza katika maendeleo.
   - Kulikuwa na hali ya kuzorota.
   - Hali hiyo ingeleta dhiki baadaye. (alama 1x3 = 3)

2. (1) Kuwa walevi.
   (2) Kuzaa watoto wasioweza kuwalea.
   (3) Hawafanyi kazi.
   (4) Hawawafunzi watoto tabia nzuri, wanawaletea madhara. (alama 4x2 = 8)

3. Uzazi ni mzuri lakini wazazi wazingatie wajibu wao. (alama 2)

4. kutopanga uzazi:
   - Hawafanyi kazi.
   - Hawawalei watoto wao vizuri.
   - Wao walewa.

(3 x 2 = 6 - alama moja kwa maelezo = 7)

Mwongozo wa kusahihisha: Matumizi ya lugha:

(a) (i) Ndani kulikuwa kweusi. (alama 1)
(ii) Mzizimo - ari au fukuto. (alama 1)

(b) (i) Po - wakati. (alama 1)
(ii) po - mahali. (alama 1)

(c) (i) Lahaula! Sijui kama kazi hii itamalizika? (alama 2 ½ x 4)
(ii) Siku ya Jumapili mwezi wa Aprili mwaka huu tutaenda Mombasa.
(½ x 4 alama 2)

(d) (i) Kulia ngoa - kuhusudu. (alama 2)
(ii) Kuwa mjango - kuwa kazi bure (alama 2)

(e) Kamilisha methali hii:
(i) Atupaye tope hujichafua naye. (alama 2)
(ii) Cha mkufuu mwanafuu ha, na akila hu, cha mwanafuu mkufuu hu akila ha.

(alama 2)

(f) (i) Mdogo. (alama 1)
(ii) Ile. (alama 1)

(g) (i) Ni rahisi kuukata mti wa zambarau ukitumia msumeno. (alama 2)
(ii) Mtoto aliuliza kama kulikuweko na chai. (alama 2)

(iii)Aliishiwa na tabasamu haraka alipoambiwa kuwa alipatikana na hatia ya kuwa mlevi na kukosa adabu. (alama 2)

(h) (i) Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. (alama 2)
(ii) Matunda yaivayo ndiyo yatundwayo. (alama 2)

(i) (a) Mkaza mwana.
(b) Umbu.
(c) Kigoli/kigori.

(j) A - kiambishi ; kiwakilishi; kiima (yeye_)
me - kiambishi ; kiwakilishi cha wakati (wakati timilifu).
ni - kiambishi ; kiwakilishi ; kitendewa ; (mimi)
kasir - suna la kitenzi.
Insha - kielezi cha jinsi (jinsi ya kufanya)
(½ x 5 = 2 ½) + (½ ya maelezo)

(k) (a) Mvivu mfano itapiki mzurura tu. (alama 2)
(b) Hana chochote. (alama 2)

(l) Mtoto ambaye analia amepigwa na mwizi vibaya sana. (alama 1)

SEHEMU YA TATU
USHAIRI MWONGOZO

9. **USHAIRI**:
(a) - Kujiasa na makanyo. - Zinduko. - Kujitoa uvivuni.
- Buriani n.k.
(yoyote mwafaka alama 2)

(b) (i) Tarbia - lina mistari minne katika kila ubeti.
(ii) Ukaraguni - kila ubeti una kina chenye silabi tofauti na ubeti mwingine kinyume na ukara wa mtiririko
(kutaja alama 1 ; kutoa sababu alama 1 ; alama 2)

(c) Tabia ya uvivu:
- Uzuruaji - Utovu wa nidhamu.
- Kutozingatia maisha ya baadaye. (alama 4x1 = 4)

(d)
- Kuzindua mtu anayepotoka.

- Kumuasa mtovu wa nidhamu.
- Kumshauri yeyote anayeshiriki katika utovu wa nidhamu n.k.
  (hoja moja 1x2 = 2)

(e) Nawatangazieni nyote popote mlipo kuwa natumai mmepata habari kuwa mimi sasa bidii yangu iko shuleni. Nimeamua kuongoka kinidhamu. (alama 5)

(f) (i) Mikiki - shuguli za kinguvunguvu.
(ii) Kuyoyoma - kupotea kwa haraka, kutokomea, enda bila kutazama.
(iii) Mkunguni - mvivu, mlegevu, goigoi.
(iv) Panda - tarumbeta, baragumu, parapanda.
(v) Sugu - jeuri, mwenye kichwa kikubwa, asiyejali, asiyesikia maonyo kabisa.
(jumla alama 5)

10. (a) - Maisha ya mwanadamu duniani.
- Hatima ya maisha ya mwanadamu ni kifo.
(hoja yoyote sawa - alama 2)

(b) Aina tatu:
- Wanaozaliwa - kutoka mimbani.
- Mimea - kutoka mzizi.
- Ndege na wadudu - kutoka kwenye yai au mfuko.

(c) Viumbe vyote vijazavyo dunia ikiwa ni wa kuzaliwa, mimea. Kutoka kwenye yai au mfuko hawezi kutosheka na mali akiwa hai lakini mwishowe hungia kaburini ambayo huchukua sehemu ndogo ya ardhi.

(b) - Vina vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.
- Vina vya kati na mwisho ni tofauti katika kila ubeti.
- Mizani hailingani katika mishororo ya kila ubeti ; mfano ubeti wa kwanza:
mshororo wa kwanza una mizani 16
na mishororo wa pili una mizani 15
(hoja 3x1 = 3)

(e) Maana ni kuwa kaburi i tayari kila wakati kupokea wafu na hivyo kila mwanadamu awe tajiri au maskini ajue bayana kuwa siku moja ataaga dunia na kuyaacha au kuacha mali yake yote.

(f) Uhuru wa kishairi:
(i) Inkisari - kufupisha maneno.
Mfano: jemamba - jembamba
Yangoja - yanangoja.
(ii) Mazda - kurefusha maneno
Mfano: Linawasalitia - linawasaliti.
(kutaja alama 1 kwa kila mfano kutoa mifano miwili moja kwa kila moja – alama 2 - 2x2 = 4)

KISWAHILI II
SEHEMU YA KWANZA
INSHA

Insha zote zizipungue maneno 400 kila moja. Kila insha ina alama 20.

1. Andika insha ya mazungumzo ya simu kati ya Kirubi na Ojilo.
2. Safari ni hatua.
3. Tatizo la vijana wanaorandaranda mijini haliwezi kutatuliwa. Jadili
4. Namna ya kupika Ugali.

KISWAHILI YA PILI
UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA

SEHEMU YA KWANZA - UFAHAMU

Nchi zetu za Afrika zinakumbwa sana na ukosefu wa mvua. Inasemekana ya kwamba jangwa linazidi kutanda katika bara hili, kwa hivyo ni wajibu wetu kujiandaa na kuchukua hatua kadha wa kadha ili tuweze kupambana na ukavu huu, kwani wahenga walisema, “Uwahi udongo uli maji.”

Kwa hakika ukavu huu unasambaa katika bara hili na unatutia hofu kubwa. Imekuwa sana tunategemea nchi za kigeni kutusaidia. Tukichunguza zaidi sababu kubwa ya ukosefu wa mvua ya kutosha ni ukataji wa miti. Kwa hivyo tuhakikishe kuwa tutapanda miti kwa wingi wakati wa mvua. Serikali ya Kenya inahimiza sana upandaji wa miti katika sehemu mbalimbali za nchi. Pia lazima tuhakikishe kwamba baada ya mche kupandwa, kufanywe mipango na kupatikane watu ambao wataiangalia na kuipalilia hadi itakapokuwa mkubwa. Ni wazi kwamba tumetilia mkazo wa kupanda miche lakini hatujazingatia miche hii kuangaliwa kwa kunyunyiziwa maji wakati wa ukame.

Hatua ya kuchimba visima, katika sehemu zenye ukavu ni jambo la muhimu sana, kwani maji ya visima yataweza kutumika majumbani na pia kunyunyizia mimea. Maji kwa binadamu ni kitu muhimu sana kwa sababu bila ya maji hakuna uhai. Huko Australia, visima vingi vimechimbwa katika sehemu zenye ukame kwa minajili ya kuwapatia wakazi wa sehemu hizo maji ya nyumbani, mifugo na kunyunyizia mimea.

Maji ya mvua na yale yanayochuruzika mitaroni, hukusanywa na kutumiwa kwa kunyunyizia mimea. Mashamba yanayonyunyuziwa maji ya aina hii, hunawiri na kustawi sana. Maji ya mito ambayo huchuruzika baharini, lazima tuyatumie baada ya kuiondoa chumvi ndani yake. Vile vile, tujaribu tuwezavyo kupanda mimea ambayo itatupa chakula cha kutosha ili tuweze kujitegemea badala ya kuzitegemea nchi za kigeni.

(a) Mwandishi ametumia methali “uwahi udongo uli maji” akimaanisha nini hasa?*(alama 3)*
(b) “Haitoshi tu kupanda miche na kutulia”. Kulingana na yaliyomo katika taarifa hii, ni hatua gani zingine zinazohitajika ili kufaulu katika mradi huo wa upanzi? *(alama 3)*
(c) Taja jitihada zozote mbili zinazochukuliwa na serikali ili kukabiliana na shida ya ukosefu wa mvua / maji*(alama 4)*
(d) Kwa nini maji ya baharini hayatumiwi moja kwa moja? *(alama 2)*
(e) Kwa nini nchi nyingi za bara la Afrika zinategemea nchi za kigeni? *(alama 3)*
(f) Maneno yafuatayo yametumiwa kuleta maana gani? *(alama 5)*
    (i) Kutanda_____
    (ii) Miche_____
    (iii) Kunyunyizia_____

(iv) Hunawiri_____

(v) Kustawi_____

MUHTASARI

Hapo kale mfanyi-biashara mmoja alisafiri akenda kufanya biashara katika nchi ya mbali na kwao. Baada ya kuuza bidhaa zake alifunga safari ya kurudi kwao. Alisafiri msitu na nyika hata akafika kwenye jangwa. Ilimbidi alivuke hilo jangwa.

Mfanyi biashara huyo alisafiri siku kadha jangwani. Siku hizo za kale kulikuwa hakuna magari. Mfanyi-biashara alikuwa amepanda farasi. Baada ya siku chache farasi alichoka sana akaanguka na kufa. Mfanyi-biashara sasa ikambidi asafiri kwa miguu.

Hatimaye maji aliyokuwa nayo yalikwisha yote, akawa hana hata tone la maji ya kunywa. Kiu ilimbana lakini maji yalikuwa hayapatikani jangwani kote. Ilimpasa aanze kusafiri usiku usiku, kwa sababu mchana jua lilikuwa kali sana na angalisafiri wakati huo kiu ingalimzidi.

Baada ya kusafiri siku mbili tatu katika hali hii, alijiona hawezi tena kuendelea. Alikuwa yu hoi, alishindwa hata kunyanyua mguu. Kwa bahati siku ile alipita msafiri mwingine amepanda ngamia. Alipomwona mfanyi biashara katika hali ile alisimama na kumwangalia. Mfanyi-biashara alimwomba yule msafiri maji.

Msafiri alimjibu, “Maji niliyonayo ni kiasi ya kunitosha mimi tu, siwezi kukupa.”

Mfanyi-biashara alisema, “Mimi ni tajiri sana. Milki yangu haihesabiki. Huko kwetu nina majumba na mashamba mengi. Mimi ni tajiri nikukabidhi mali hiyo yote nawe unipe hicho kiriba chako cha maji.”

Msafiri alimjibu, “Mimi sina haja ya mali iliyoko nchini kwenu mali hiyo sitaweza kuitumia nchini kwetu.”

Mfanyi-biashara aliwaza kisha akamwambia, “Hivi hapa nina kifuko kimejaa almasi na lulu. Hizi nilizinunua huko nilikotoka. Biashara ilinipatia faida nyingi sana. Je, utachukua almasi na lulu hizo zote, nawe unipe kiriba cha maji?”

Msafiri alikubali. Mfanyi-biashara alipata maji akanywa na kukata kiu yake. Maisha yake yakaokoka na kuepukana.

Maswali

(a) Eleza matatizo yaliyomkabili mfanyi-biashara katika safari yake toka mwanzo hadi mwisho wa safari. (Maneno 30 - 40) *(alama 8)*

Nakala chafu

Nakala safi

(b) Katika kila janga mfanyi-biashara alipita, kulijitokeza suluhu. Eleza jinsi hali hii inavyosawirika.
(Maneno 20 - 30) *(alama 6)*
Nakala chafu
Nakala safi

(c) Eleza kwa ufupi mambo muhimu yanayojitokeza katika mazungumzo baina ya msafiri na mfanyi-biashara. (Maneno 40) *(alama 6)*
Nakala chafu
Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA

(a) Andika sentensi ifuatayo bila kutumia "amba"
(i) Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali. *(alama 1)*
(ii) Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea. *(alama 2)*

(b) Badilisha sentensi hizi hadi usemi wa taarifa
(i) "Nitarudi tu ikiwa mtakubali kuomba msamaha." Juma alisema. *(alama 2)*
(ii) "Elezeni vile mlivyokuja hapa na namna mtakavyokwenda." Mwalimu mkuu alisema *(alama 3)*

(c) Fuata maagizo uliyopewa baada ya kila sentensi ili kujibu maswali haya.
(i) Aliogopa kumwangalia simba aliyekula mzoga. (Tumia neno 'Ogofya' bila ya kubadilisha maana ya sentensi) *(alama 2)*
(ii) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ukiwa unatumia msumeno. (Anza Ni rahisi . . .) *(alama 2)*

d) (i) Eleza maana na matumizi ya methali hii *(alama 2)*
Kila mchukuzi husifu mzigo wake
(ii) Kamilisha tashbihi hizi *(alama 2)*
.....kama mauti
Nuka kama.....

(e) (i) Kanusha sentensi hii *(alama 2)*
Tungewalaki kama tungejua watakuja
(ii) Sahihisha sentensi ifuatayo na uiweke katika wingi *(alama 2)*
Ningalifanya kazi ningekuwa tajiri

(f) Tunga sentensi nne kuonyesha matumizi na maana nne za kijineno ki

(g) Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi *(alama 4)*
(i) Bibi yule alinunua gari _____ (-pya)
(ii) Mwizi alifukuzwa na mbwa _____ (-angu)
(iii) Mti (-ingine) _____ uliangushwa badala ya ule wa kwanza.
(iv) Nyoka aliingia _____ (-le) shimoni.

(h) Unda majina mawili kutoka vitenzi hivi na utumie katika sentensi ili kubainisha maana *(alama 4)*
(i) Safiri
(ii) Zaa

(i) Akifisha kifungu hiki
Yohana na emanueli walifunga safari wakielekea mashariki kusini na hatimaye magharibi walifika huko novemba mwaka jana walipokuwa wakirudi walimkuta mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale *(alama 4)*

(j) (i) Geuza sentensi hii hadi udogo *(alama 2)*
Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi.
(ii) Eleza umuhimu wa sehemu hizi za mwili
* Figo
* Moyo

SEHEMU YA TATU
USHAIRI

9. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali

Cheo cha mtu hupanda, ukipata mke mwema,
Kula chachu na maganda, mfano kama mnyama,
Na nyumba iwe kibanda, si nzuri ya kutazama,
Utaona umewanda, moyo umekuterema.

Mke mwema ni johari, yenye furaha daima,
Awe hasa na saburi, na adili na huruma,
Hata ukiwa fakiri, hutimizi pato jema,
Utaona tajiri, maliki dunia nzima.

Mke akiwa mbishi, wa kushindana kusema,
Na majivuno na mashi, na ulimi wake pima,
Hata kama wala pishi, wali na kilo ya nyama,
Utajiona waishi, duniani huna kima.

Mke mrembo si hoja, hili nimekwisha pima,
Nimepima rejareja, kila jambo kutazama,
Kujumlisha pamoja, mambo yalivyosimama,
Nikaona kuwa tija, ndogo kuliko gharama.

Awe mwema mke wangu, nani hapendi kusema?
Wema asili ya ungu, milele una heshima,
Kuwa wema walimwengu, ni wajibu na lazima,
Wema dawa ya machungu, moyoni yanayouma.

<u>Maswali</u>

(a) Kulingana na shairi hili, mke mwema ana faida gani kwa mumewe? *(alama 3)*
(b) Mke mwema ana sifa gani? *(alama 3)*

(c) Mwandishi wa shairi hili alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili?*(alama 3)*
(d) Eleza kwa ufupi muundo wa shairi hili. *(alama 6)*
(e) Maneno yafuatayo yametumiwa katika shairi kuleta maana gani? *(alama 5*)
(i) Chachu
(ii) Johari
(iii) Saburi
(iv) Mbishi
(i) Pishi

10. Nataka nikupe chanzo, weka katika moyo,
Kishike kwa mkazo, hata kizae mazao,
Ukifanya bidiizo, kushawishi utakayo,
Utaona mfulizo, kwako yanakuja mbio

Husemwa Alexander, shujaa Macedonia,
Ambaye alishinda, karibu nzima dunia,
Alipokosa pa kwenda, tena kushambulia,
Kwa huzuni alikonda, akadiriki kulia,

Ingawa vita vigumu, yeye alivipenda,
Kwa moyo aliazimu, daima mbele kwenda,
Moyo kuitia hamu, mashaka kuyashinda,
Ndilo linalolazimu, kila mtu kutenda.

Moyo ukiulegeza, kila kitu kigumu,
Utaishi na kuoza, hupati kuonja tamu,
Lakini ukijikaza, ipasavyo mwanadamu,
Katika mwangaza, utakuwa na sehemu.

Moyo kuupa mwanzo, wa kushindwa hustawi,
Utaona mzozo, unalotaka haliwi,
Na hili ni katizo, ya faida ya uhai,
Peponi halina tuzo, na hapa ni uadui

Hili linahasiri, moyoni kulidhibiti,
Mabaya ukifikiri, yaliyo mema hupati,
Na kila wazo la heri, hukaribisha bahati,
Fikira iliyo nzuri, sawasawa na yakuti.

Maswali

(a) Kilichomfanya Alexander kufaulu katika kadhia zake ni nini hasa? *(alama 3)*
(b) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. *(alama 4)*
(c) Kuna athari gani kwa kukosa moyo wa ujasiri? *(alama 3)*
(d) Mtunzi huyu ana dosari gani kwa upande wa muundo wa shairi? *(alama 4)*
(e) ‘Kwa huzuni alikonda, akadiriki kulia.’ Ni kwa nini ilitukia hivi? *(alama 3)*
(f) Eleza maana ya maneno haya. *(alama 3)*

(i) Akadiriki
(ii) Kushawishi
(iii) Kulidhibiti

KISWAHILI II
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
SEHEMU YA KWANZA INSHA

Maudhui - 5
Mtindo - 4
Msamiati - 5
Sarufi - 6
Hijai - aondolewe alama zisizozidi 3

* Ukadiriaji wa alama hizo ni jukumu la mwalimu kwa kutegemea kazi ya mwanafunzi.

- **Maudhui**

* Yaweza kuhusu mada yoyote.
* Mwanafunzi aweza kuonyesha lengo au kiini cha mazungumzo
* Aonyeshe mawazo kadha wa kadha yanayohusu kiini cha mazungumzo

- **Mtindo**

* Atenganishe jina na maneno yake hasa aghalabu kwa kutumia koloni.
* Atumie lugha ya simu - kama vile 'Hallo' n.k.
* Atangulize mazungumzo yake kwa maamkuzi, kujitambulisha na kutaja lengo la kupiga simu.
* Aendeleze mazungumzo yake ipasavyo.
* Aitimize kazi yake na ikiwezekana amalizie maagano.

- **Msamiati**

* Atumie lugha na sajili mwafaka.

- **Sarufi**

* Kila kosa la sarufi linapojitokeza, liadhibiwe na linaporudiwa, lionyeshwe tu.
* Atangulize kazi yake kwa kueleza maana ya methali na matumizi, au atoe kisa moja kwa moja.
* Kisa kiweze kuthibitisha ukweli wa methali hii
* Aitimize kazi yake

(ii) Swali la TATU

* Aonyeshe pande zote za swali.

(iii). Swali la NNE

* Atumie lugha ya maelezo na aonyeshe hatua kwa hatua.

SEHEMU YA PILI
UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA .

(a) Kupambana na tatizo la kutanda kwa jangwa barani kabla halijapita kimo au kuchukua hatua za tahadhari mapema ili kuzuia jangwa kama kungali kunawezekana. ***(alama 3)***

(b) * Kuangalia miche / kutunza

* Kupalilia
* Kunyunyiziwa maji wakati wa ukame ***(hoja tatu 3x1 = 3)***

(c) * Serikali ya Kenya inahimiza upandaji miche.
* Australia imechimba visima katika sehemu zenye ukame. ***(2x2 = 4)***

(d) Yana chumvi ndani yake. ***(alama 2)***

(e) * Hawapandi mimea inayowapa vyakula
* Ukavu / ukame ambao unasambaa
(2 x $1^{1}/_{2}$ = 3)

(f) Kutanda - kuenea
Miche - Chipukizi, mimea inapoanza kutoa majani yake juu ya ardhi
Kunyunyizia - kumwagia maji
Hunawiri - Hung'aa / kufanya vizuri / vyema / kupendeza
Kustawi - Kukomaa

MUHTASARI

(a) * Kusafiri msituni
* Kupitia jangwa
* Hakukuwa na magari
* Farasi kuchoka na kufa / kukosa namna ya kusafiria
* Maji aliyokuwa nayo kwisha
* Kiu kumbana
* Kusafiri usiku, giza
* Kuwa hoi / mahtuti
* Kukatazwa maji na msafiri ***(hoja ozote tatu 6x1 = 6)***

(b) * Kukosa gari - kupata farasi
* Jua kali ya jangwa - kutembea usiku
* Kiu - Kutembea usiku / kupata mtu wa kumpa maji
* Msafiri kukataa mali ya mfanyi-biashara - kutoa lulu na almasi. ***(4 x $1^{1}/_{2}$ = 6)***

(c) * Mfanyi-biashara kuomba maji msafiri kwa kumuahidi mali
* Msafiri kukataa mali ya mfanyikazi na kutoona thamani yake
* Msafiri kumkataza mfanyi-biashara maji
* Mfanyi-biashara kumuonyesha lulu na almasi msafiri
* Msafiri kukubali kumpa maji mfanyi-biashara
(hoja ozote tatu 6x1 = 6)

a - 6
b - 6
c - 5

Utiririko - 3
Jumla 20

MATUMIZI YA LUGHA

(a)(i) Jitu linalotusumbua sharti liadhibiwe vikali
(ii) Mmea upandwao / ambao hupandwa katika msimu wa masika humea. ***(Alama 2)***

(b)(i) Juma alisema ya kuwa / kuwa / ya kwamba / kwamba angerudi tu ikiwa / kama _____ wangekubali kuomba msamaha. ***(Alama 2)***
(ii) Mwalimu Mkuu aliwataka / aliwaambia waeleze vile walivyoenda hapo na namna wangeenda / watakavyoenda. ***(Alama 3)***

c) (i) Simba aliyekula mzoga alimuogofya kwa hivyo hakumwangalia ***(Alama 2)***
(ii) Ni rahisi kukata mti wa zambarau ikiwa unatumia msumeno ***(Alama 2)***

(d) (i) Mtu mwenye shida ndiye ajuaye shida hizo. Kila mtu ana matatizo na hakuna haja ya kuwaeleza wengine. ***(Alama 2)***
(ii) Hakika kama mauti. ***(Alama 2)***

(e) (i) Hatungewalaki kama hatungejua hawaji ***(Alama 2)***
(ii) Tungalifanya kazi tungalikuwa matajiri *au* Tungefanya kazi tungekuwa tajiri. ***(Alama 2)***

(f) * Ki ya Masharti
* Ki ya udogo
* Ki ya kukanusha
* Ki ya lugha kwa *mfano* Kikamba
* Ki ya ngeli ya KI-VI
* Ki ya jinsi / namna kwa *mfano* tembea kijeshi na kadhalika ***(4x1 = 4)***

(g) (i) Jipya
(ii) Wangu
(iii) Mwingine
(iv) Mle ***(4x1 = 4)***

(h) (i) Safari / msafara / usafiri
(ii) Mzazi / Mzaliwa / Uzazi ***(2x2 = 4)***

(i) Yohana na Emanueli walifunga safari wakielekea Mashariki, Kusini na hatimaye Magharibi. Walifika huko Novemba mwaka jana. Walipokuwa wakirudi, walimkuta Mwalimu Mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale.
(Sehemu 12 = 12 x $^{1}/_{3}$ = 4)

(j) (i) Kijoka kile kirefu kilifukuzwa na vijitu vingi. ***(Alama 2)***
(ii) Figo - husafisha damu

Moyo - husambaza damu mwilini ***(2x1 = 2)***

4. Uvivu
   * Kulaza damu kwa Ame na zidi kumewaletea umaskini
   * Mwalimu anapolala darasani anasababisha elimu duni ambayo hatimaye inakuwa umaskini maana wanafunzi hawanufaishwi na elimu.
   * Utegemeaji wa misaada unaleta umaskini.

SEHEMU YA TATU
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
USHAIRI

9.(a) * Mtu hupanda cheo
   * Mtu huwanda hata ingawa anakula maganda
   * Moyo unamterema ***(Hoja 3 x 1 = 3)***

(b) * Ni johari
   * Ana furaha daima
   * Sana subira
   * Mwadilifu ***(Hoja 3 x1 = 3)***

(c) * Kutoa mawaidha kwa wanawake wawe wema
   * Kundodoa faida za mke mwema na hasara za mke mbaya
   * Kuntoa kile kinachotakikana kwa mke. ***(2 x1$^{1}/_{2}$ = 3)***

(d) * Tarbia - mishororo minne
   * Mtiririko
   * Urari wa mishororo 16 kila mshororo ***(3 x 2 = 6)***

e) (i) Chachu - hasira / kitu kikali au kichungu
   (ii) Johari - kitu cha thamani / kizuri / uzuri wa mke
   (iii) Saburi - Subira / ungojevu / uvumilivu
   (iv) Mbishi - anayebisha
   (v) Pishi - kipimo cha vibaba vinne cha ratili/ upishi/ vitu / vyakula vilivyopikwa
   (5 x 1 = 5)

10.(a) * Ushujaa wa moyo
   * Bidii ***(2 x1$^{1}/_{2}$ = 3)***

(b) * Mtu asipokaza moyo wake, atapata kuwa vitu / mambo yote ni magumu
   * Mtu hataweza kupata mazuri / matamu maishani
   * Lakini mtu akijitahidi kwa kadri awezavyo, atapata kufaulu. ***(Alama 4)***

(c) * Mtu hataonja matamu / yaliyo mema hutapata
   * Ataishi na kuoza
   * Unalotaka halitawezekana
   * Uadui
   * Kila kitu kitakuwa kigumu ***(Hoja 3 x 1 = 3)***

(d) Vina - Ubeti wa tano vina vya mwisho ni 'i' lakini mshororo wa tatu ni 'l'
Mizani - ni 8, lakini katika baadhi ya beti ni 7, 8 au 8, 7 ***(2 x 2 = 4)***

(e) * Hakuamini ufanisi wake
* Alikosa mtu mwingine wa kupigana naye ***($1\frac{1}{2}$ x 2 = 3)***

(f) Akadiriki - akaamua / akaweza / akapata
Kushawishi - kumvuta mtu kwa maneno / pembeleza akubali
Kulidhibiti - tia mkononi / weza / linda au tunza.

KISWAHILI III
SEHEMU YA KWANZA
INSHA

Andika insha mbili zisizopungua maneno 350 – 400. Insha ya kwanza ni ya lazima.

1. Umeteuliwa kuwa Mwanachama wa Kamati andalizi ya mkutano wa Harambee ya Kuwachangia vilema mkoani mwenu. Tayarisha ratiba itakayofuatwa katika mkutano huo.
2. Bahati ni judi
3. Nchi itaendelea ikiwa elimu itaimarishwa Jadili
4. Ndoto ya ajabu

KISWAHILI
SEHEMU YA PILI
UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA

Thamani ya shilingi ; tokea ibuniwe kama sarafu ya kuendesha biashara, inadunika kila kukicha. Tukirudisha nyuma gurudumu la wakati tutaweza kuchungulia na kujionea mengi ambayo yalikuwa yaweza kununuliwa kwa uwezo wa sarafu moja tu ya shilingi. Fungu la machungwa, au mkungu mzima wa ndizi au tita la kuni – haya yote yalikuwa yaweza kulipiwa shilingi tu kabla ya kumiliki kama mali yako. Kweli zama hizo, shilingi ingeweza kukushibisha na usilale na njaa.

Shilingi yenyewe ilikuwa na miujiza mingine. Thamani yake kwa miaka na miaka, ilikuwa ni ile ile na athara kama vile za kuanguka kwa thamani ya pesa ilikuwa ni jambo geni kabisa katika janibu hizi. Kwa wengi wa wakazi wa huku, athari hizo za kuanguka kwa thamani ya shilingi au Sarafu zozote zile za kilimwengu kama vile dola thabiti, yalikuwa ni matukio ambayo yalijulikana huku kama ndoto za vitabu vya historia tu. Ndoto hiyo leo ni ukweli mgumu usioaminika. Hali imewia kuwa ngumu zaidi na shilingi imekuwa chepechepe na ni shida kuitumainia kukunufaisha kwa chochote kile ila ukiwa na uraibu wa sigara moja mbili au ukiwa wataka kununua pipi tatu kwa kuondoshea ukakasi unaotokana na kuvuta sigara.

Shilingi 'haingiari ikaua' Enzi hizo zimepita na kamwe hazitarudi tena. Leo mifumo mbalimbali ya kiuchumi duniani imo katika gharika kweli kweli kwani adui 'inflesheni' amefaulu kuzizorotesha na kuziacha katika hali dhaifu viongozi mbali mbali kote duniani wakitawazwa, tamko lao la kwanza ni kupambana na adui huyu na kuingia katika utawala wao na kujitolea kupambana naye adui huyo kama yumo katika vita vya kufa na kupona.

Uchumi mwingi umenyauka. Fikira na wataalamu wengi wenye kufahamu sayari ya uchumi wangali wamekaukiwa na mbinu za kumwagusha adui huyo ili maisha yarudie ile hali ambayo ilikuwa yadumu

kila mahali ulimwenguni. Vitabu vya historia havisaidii kitu kwani fani yake adui huyu ilikuwa bado haija wakumba binadamu.

Usawazishaji wake 'inflesheni' wategemea mawimbi ya thamani za sarafu maalumu za kilimwengu. Wakati zinapokuwa makini na hazianguki kutokana na thamani zake, biashara na thamani ya shilingi zetu huwa pia shwari na zenye kurahisisha uendeshaji na upangaji wa biashara. Lakini mawimbi yake yakianza kugharikisha thamani za sarafu hizo, shilingi nayo huwa kama yalewalewa katika bahari ambayo haina upeo.

Maswali

a) Toa tofauti mbili baina ya shilingi ya zamani na ya sasa (alama 4)
b) Mwandishi wa taarifa hii alichochewa na nini hasa hadi akaandika ? (alama 3)
c) Kuna ithibati gani kutoka taarifa kuonyesha kuwa kuanguka kwa thamani ya shilingi ni tatizo kubwa duniani ? (alama 4)
d) Mwandishi ametumia jazanda nyingi ili kusisitiza unyeti wa swala hili; kwa mfano … tukirudisha nyuma gurudumu la wakati…… taja na uelezee jazanda nyingine zozote mbili na uelezee maana ya kila moja (alama 4)
e) Kuna faida gani thamani ya sarafu maalumu ulimwenguni inapokuwa thabiti ? Toa ithibati zako kutoka taarifa (alama 2)
f) Eleza maana ya maneno haya kulingana na muktadha wa taarifa hii (alama 3)
   i) Inflesheni
   ii) Janibu
   iii) Mawimbi

MUHTASARI.

Katika kila kiwango, wanafunzi huonekana kama wana shida kubwa sana katika kuyachambua mashairi. Hali hii ni matokeo ya mambo mengi. Yaweza kuwa mashairi waliyokutana nayo mara ya kwanza yalikuwa magumu, au yalikuwa yamechanganya kiswahili sanifu na lahaja zingine ambazo wasomi hawangezielewa moja kwa moja.

Jambo hili huwakatisha wanagenzi tamaa hasa wanapokosa kulipata katika kamusi msamiati uliotumika. Wanapotamauku, wao huwa hawataki kujishughulisha na mashairi. Huu ndio mwanzo wa kuanguka kwao katika mitihani kwa vile wengi wao hulazimika kukutana na mashairi kwa mara ya kwanza katika chumba cha mtihani. Hiki ni kinyume cha jinsi mambo yanavyostahili kuwa. Ukweli ni kuwa mashairi yanastahili kuwaburudisha wasomi pindi wakutanapo nayo.

Madai kuwa mashairi ya kiswahili ni magumu kufahamika isipokuwa kwa watu maalum wenye vipawa maalum hayafai. Mwanafunzi ambaye anataka kufanya vizuri katika swali la mashairi ni lazima aanze kuyapenda mapema iwezekanavyo. Ni muhimu aazimie kuyapenda hasa ajuapo kuwa atatahiniwa katika sehemu hii. Kwa vile hana njia ya kuyaepuka, azingatie msemo wa wazungu usemao kuwa kama hupati upendacho, anza kupenda kile ukipatacho. Ili kuchochea upendo ndani yake, asijishughulishe na yale mashairi ambayo anayaona kama ni magumu. Ajaribu kuyaelewa yale ambayo anayaelewa na kuudondoa ule ujumbe ambao yameumbeba na vile vile ajaribu kuufurahia utamu wa maneno yaliyotumika. Atalipata hili kwa kuyasoma kwa sauti. Kila mara, akumbuke kwamba kadili atakavyokutana na mashairi mengi ndivyo atakavyofurahia na kuyaelewa.

Pili, akikutana na shairi, asishtushwe na msamiati au lahaja iliyotumika. Hata kama haelewi msamiati uliotumika, ajaribu kuelewa ujumbe uliomo katika shairi. Hata hivyo, lazima ajihami na msamiati mwingi iwezekanavyo. Isitoshe, ni muhimu katika mazoezi yake kujaribu kuandika mashairi yake mwenyewe ili aelewe ni kwa nini waandishi huyaandika mashairi jinsi wanavyoandika; Atagundua kwa nini waandishi huyarefusha, huyafupisha au huyabadilisha maana ya maneno mbali mbali.

Maswali.

a) Ni mambo gani yanayochangia kuanguka kwa mwanafunzi katika swali la ushairi ? ***(alama 7) (maneno 40)***

Nakala Chafu.
Nakala Safi.

b) Mwandishi amependekeza hatua gani kuchukuliwa ili mwanafunzi afaulu katika maswali ya mashairi **?** ***(alama 8) (Maneno 50)***

Nakala Chafu
Nakala Safi

c) Mwanafunzi ahitajika kufanya nini ili kuyapenda mashairi ***(alama 5)*** ***(maneno 20)***

Nakala Chafu
Nakala Safi

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA.

a) Tumia kiulizi - pi katika kujaza sehemu zilizoachwa wazi. ***(alama 4)***

i) Ni tunda _____ ulililoleta ?
ii) Ni mayai _____ yaliyovunjwa ?
iii) Ni kiwete _____ aliyepata msaada ?
iv) Ni mitume _____ waliojilolea kufanya kazi ?

b) Andika sentensi zifuatazo katika kauli ya kufanyisha / za ***(alama 4)***

i) Alikifanya kijiti kiingie ndani ya kufuli.
ii) Mzazi alimfanya mwanawe alime siku nzima

c) Tumia virejeleo vifavyo katika sentensi hizi.

i) Mchezaji alipiga mpira kwa ustadi
ii) Simba alifukuza mtalii aliyetaka kupiga picha
iii) Umeokota wapi ndizi hizi zote ?
iv) Andrea alipanga vizuri maua mezani

d) Andika tena sentensi hizi ili zisiwe katika hali ya kukanusha ***(alama 4)***

i) Asiyekujua hakuthamini
ii) Asiyejua maana haambiwi maana
iii) Fimbo ya mbali haiui nyoka
iv) Amani haiji ila kwa ncha ya upanga

e) Ziandike sentensi hizi kwa kufuata maagizo

i) Mlete mtu mwenye akili (tumia ‘amba’)
ii) Walifungana bao moja kwa moja katika mchezo ule (tumia …… Sare)

f) Unda majina kutoka vitenzi hivi (alama 2)

i) Kulia _____ , Kudhani _____

ii) Ni nini maana ya : Amepata ahueni (alama 1)

Amekuwa buge (alama 1)

g) Andika sentensi ifuatayo katika udogo **(alama 2)**

i) Alishikwa na jipu ambalo lilivimbisha dole lake la mguu mithili ya pesa

ii) Akifisha sentensi hii: (Alama 2)

Ondiek aliita Maria Maria njoo hapa.

h) Eleza matumizi ya 'Ki' katika sentensi hizi:

i) Nitakapokuwa ni<u>ki</u>lala atakuwa a<u>ki</u>durusu

ii) <u>Ki</u>vulana hicho <u>ki</u>nawafurahisha wenzake

i) Andika maana mbili zinazojitokeza katika kila moja ya sentensi hizi

i) Mwalimu alimsomea mwanafunzi

ii) Alimlilia mwanawe

j) Ikiwa Mtondo ni Jumamosi

i.) Juzi ni siku gani _____ (alama 1)

ii) Leo ni siku gani _____ (alama 1)

iii) Tunga sentensi mbili ukutumia tashbihi zinazotokana na maneno haya:
(baidika, mkizi) (alama10)

SEHEMU YA TATU
USHAIRI.

1. Mabadiliko lazima kwa watu ulimwenguni,
Nalo lilianza zama hakika si neno geni,
Ni tabia ya daima kipya kuwa cha zamani,
Kwa watu ulimwenguni mabadiliko lazima.

Kama hili halikuwa jipya lingekuja lini ?
Mfano wetu maua na majani mitini
Hili linapofumua, lile huanguka chini
Jipya lingekuja lini kama hili halikuwa

Kuwapo na kutowapo tumo mabadilikoni
Nakuapia kiapo kwamba hii ni kanuni
Nawe linganisha pepo kaskazi na kusini
Tumo mabadilikoni kuwapo na kutowapo

Tukitaka tusitake ni sheria tumo ndani
Waume na wanawake roho zote za manani
Kubadili mwendo wake dunia si yamkini
Ni sheria tumo ndani tukitaka tusitake

Mwendo wa dunia mbio haimo usingizini
Kwa aliye na kilio na aliye furahani
Mara huona machweo na mara jua kichwani
Haimo usingizini mwendo wa dunia mbio

Mbio maisha ya watu, mfululizo mbioni
Hali hii kila kitu, kilicho maumbileni
Mbio haingoji mtu – tuo haijulikani
Mfululizo mbioni, mbio maisha ya watu

Hutuchukua kwa zamu katika matumaini
Na mchungu na matamu hututokea njiani
Na mara hatufahamu lilikuwa jambo gani
Katika matumaini hutuchukua kwa zamu.

Maswali.

a) Kuna mifano mingi ya kimaumbile iliyotolewa ili kudhihirisha dhana hii ya mabadiliko. Itaje mifano yoyote mitatu. (alama 3)
b) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari (alama 4)
c) Kuna ithibati kuwa mabadiliko hayabagui ? (alama 4)
d) Nakili mishororo minne inayoeleza kuwa mabadiliko ni sharti maishani (alama 4)
e) Katika shairi hili mwandishi ametaja maneno na vinyume vyao. Toa majozi manne ya maneno haya (neno na kinyume chake) (alama 2)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo:
   i) Linapofumua
   ii) Kiapo
   iii) Tuo (alama 3)

10. Nina machache muhimu, ambayo ni ya thamani,
Nataka kutakalamu, niyatoe hadharani,
Wayafahamu kaumu, marafiki ikhuwani,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Neno ‘UTU’ tufahamu, ni funzo kwetu soteni,
Nitawapa nidhamu, kwa mpango wa kanuni,
Na tena ni kwa nudhumu, kwa shauri kubaini,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Wema si mali ya mtu, hili tujue yakini,
Wala uzuri si kitu, wa umbo lako mwilini,
Kitu aula ni utu, kitu bora duniani,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Na kivazi na kitimo, kwa utu hakilingoni,
Nguo si kitu adhimu, na kiatu mguuni,
Kitu ni ubinadamu, kisokuwa na kifani,

Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Utu si kitu kujua, ujuzi wa akilini,
Ama alojaaliwa, kupata usultani,
Binadamu ni murua, ajuaye na hisani,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Utu ni adimu, kipawa chake manani,
Utu ni moyo rahimu, heshima yake insani,
Na tena ni ukarimu, na roho yenye imani,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Utu siyo ujabani, ushujaa wa vitani,
Mtu ni utu mzuri, wa tabia na makini,
Mwenye utu fahari, kwa wake na majirani,
Ewe kiumbe insani, kuwa mwenye utu.

Utu ni khulka njema, maumbile ya nyumbani,
Ni ubinadamu mwema, ni ya Mola yake shani,
Hima basi ndugu hima, utu ni wetu soteni,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Ya tisa ni kaditama, kalamu naweka chini,
Ikiwa niliyosema, nitakuwa makosani,
Tafadhali wa heshima, nawaomba samahani,
Ewe kiumbe insani, kuwa mja mwenye utu.

Maswali.

a) Hili ni shairi aina gani ? (alama 1)
b) Chambua shairi hili kwa kuzingatia:
   i) Mizani
   ii) Vina (alama 4)
c) Dondoa sifa halisi za utu kama zilivyotajwa katika shairi hili. (alama 5)
d) Andika ubeti wa saba katika lugha ya nathari (alama 4)
e) '…. Utu ni kitu adimu' ……. Kifungu hiki kinamaanisha nini hasa ? (alama 2)

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa (alama 4)
   i) Kaumu
   ii) Kubaini
   iii) Aula
   iv) Soteni

KISWAHILI III
SEHEMU YA KWANZA
<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA.</u>

i.) MTINDO (Kwa mfano swali la kwanza)

- Mtahiniwa aweza kuandika ratiba kwa kufuata mtindo mwafaka. Ataja saa halafu kitendo kinacho fuata. Atumie lugha ya moja kwa moja isiyo na maelezo au fafamusi nyingi. Katika maswali mengi tumia mtindo wa kawaida
- Sehemu zingine za usahihishaji yaani msamiati, maudhui, sarufi na hijai; tumia mtindo wa kawaida. Hapa chini ni mwongozo kama kielelezo tu. Tumia kielelezo hiki katika maswali yote.

ii) Msamiati (alama 5)

- Kadiria umbuji wake na kiwango cha lugha
- Uafaka wa maneno (sajili) kulingana na muktadha
- Kiwango cha kujitosheleza kimsamiati

iii) Maudhui (alama 5)

- Yaliyomo, yaani yale anayozungumzia katika insha yake yaweze kuoana na anwani.
- Mawazo au hoja ambazo zimetajwa

iv) Sarufi (alama 6)

- Sehemu hii husahihishwa kwa kinyume na i.,ii na iii kwa sababu tunakosoa mwanafunzi na alama atakazopata zitategemea idadi ya makosa aliyofanya. Jumla ya makosa ya kuadhibiwa ni kumi na mbili (12), kila kosa likiwa na thamani ya nusu (½) alama.
- Adhibu kila kosa la sarufi utakalopata kwa mara ya kwanza. Usirudie kuadhibu kosa lile lile mara mbili au zaidi ya moja.

v) Hijai (alama tatu za kuondolewa)

Kama ilivyo katika sarufi, sehemu hii hutegemea makosa yanayopatikana. Hukadiriwa kwa kutegemea idadi ya makosa sita (6) kila kosa likiwa na thamani ya nusu (½) alama.

KISWAHILI SEHEMU YA PILI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
UFAHAMU.

a) – Shilingi ya zamani ingeweza kununua vitu vingi (ilikuwa na thamani) lakini shilingi ya kisasa haiwezi kunua vitu hivyo vyote.
- Shilingi ya zamani thamani yake ilibaki hivyo hivyo lakini shilingi ya kisasa inabadilika kila wakati, inashuka ikipanda. (2 x 2 = 4)

b) Amesumbuliwa na thamani ya shilingi inayoendelea kuzorota siku baada ya siku. (alama 3)

c) – Uchumi mwingi kunyauka
- Mifumo mingi ya kiuchumi duniani imo katika gharika na imezoroteshwa na inflesheni. (2 x 2 = 4)

d) - Uchumi umo katika gharika – uchumi umo katika janga / tatizo
- Uchumi umenyauka – uchumi umezorota
- Mbinu za kumwangusha adui – njia za kutatua tatizo fulani
- Mawimbi ya thamani - hali ya mambo kuhusu thamani ya sarafu
- Shilingi kulewalewa – kuanguka na kuongeza thamani – kutopata uthabiti. (2 x 2 = 4)

e) Biashara na thamani ya shilingi huwa shwari na hurahisisha uendeshaji biashara (2)

f) i.) Kuanguka kwa thamani ya shilingi
ii) Eneo, mahali
iii) Mchafuko / kukosa ithabiti

MHUTASARI.

a) – Shida ya kuchambua mashairi
- Kuogopa mashairi baada ya kulikuta shairi gumu
- Itikadi kuwa mashairi ni magumu
- Kutofanya mazoezi na kukutana na mashairi kwa mara ya kwanza katika chumba cha mtihani
- Kupata msamiati usiopatikana katika kamusi 5 x 1 = 5

b) - Asivunjwe moyo anapokabiliana na mashairi magumu
- Atupilie mbali dhana kuwa ushairi ni ngumu
- Kuyapenda mapema na kufanya mazoezi
- Ajaribu kutunga mashairi
- Ajihami na msamiati 4 x 2 = 8
-

c) – Akubali maana hana njia ya kuepuka
- Ajaribu kufurahia utamu wa maneno
- Asome kwa sauti
- Apitie mashairi mengi 4 x 1 = 4

a + b + c = 17 (Utiririko = 3)

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA.

a) i.) lipi
ii) yapi
iii) yupi
iv) wapi 4 x 1 = 4

b) i.) Alikiingiza kijiti ndani ya kufuli (2)
ii) Mzazi alimlimisha mwanawe siku nzima (2)

c) i.) Aliupiga
ii) alimfukuza
iii) umeziokota
v) aliyapanga

d) i.) Anayekujua anakuthamini (1)
ii) Anayejua maana huambiwa maana (1)
iii) Fimbo ya mbali huua nyoka (1)
iv) Amani huja kwa ncha ya upanga (1)

e) i.) Mlete mtu ambaye ana akili (2)
ii) Walienda sare katika mchezo ule (2)

f) i.) Kilio / mlio , dhana (2 x 1 = 2)
ii) Amepata msaada / kupona kutoka ugonjwa (1)
Ameishiwa (1)

g) i.) Kilishikwa na kijipu ambacho kilivimbisha kidole chake cha kiguu cha pera(2)
ii) Ondiek aliita “Maria! Maria! Njoo hapa” (2)

h) i.) Hali ya kuendelea (2)
ii) Udongo / kiambishi cha ngeli ya Ki – Vi (2)

i.) i.) Mwalimu anasoma kwa niaba ya mwanafunzi
- Mwalimu anasoma ili mwanafunzi asikie / aandike

ii) Alilia kwa sababu ya mwanawe (huenda kwa sababu mwana amepatwa na janga
- Alimnyenyekea mwanawe ili ampe msaada

j) i.) Jumatatu (1)
ii) Jumatano (1)
iii) Kama ardhi na mbingu (1)
Mwenye hasira kama mkizi (1)

SEHEMU YA TATU
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
USHAIRI.

a) - Maana kufumua na kuanguka chini
- Pepo kaskazi na wa kusi
- Kilio na furaha
- Machweo na macheo (3 x 1 = 3)

b) - Maisha huenda yakibadilika, mara tunapatwa na machungu mara matamu, kila moja kwa wakati wake. (4 x 1 = 4)

c) - Watu ulimwenguni (wote)
- Waume kwa wanawake
- Roho zote za manani
- Aliye na kilio na aliye na furaha
- Kila kitu kilicho maumbileni (4 x 1 = 4)

d) i.) Kwa watu ulimwenguni mabadiliko ni lazima
ii) Ni sheria tumo ndani tukitaka tusitake

iii) Tukitaka tusitake sheria tumo ndani
iv) Nakuapia kiapo kuwa hii ni kanuni (4 x 1 = 4)

e) - Waume - Wanawake
- Kaskazi – Kusini
- Kilio - furaha
- Machungu - Matamu (4 x 1 = 4)

f) - Linapofumua - linapotoa ua
- Kiapo - kula yamini
- Tuo - kusita (sitama) (3 x 1 = 3)

KISWAHILI IV
SEHEMU YA KWANZA
INSHA

Andika Insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya lazima. Insha ya pili chagua kutoka 2, 3, na 4. Insha zako zisipungue maneno 400.
Kila insha ina alama 20

1. Toa maoni yako kuzishauri serikali za nchi za kiafrika jinsi ya kutumia vyema misaada wanayofadhiliwa na mataifa ya kigeni
2. Mawasiliano yatakavyokuwa mwaka 2100
3. Adui mpende
4. Si lazima kusoma ili kufaulu maishani. Jadili

KISWAHILI SEHEMU YA PILI
UFAHAMU, MUHTASARI, MATUMIZI YA LUGHA

Yaonekana watu hawajali usanifu wa Kiswahili katika Afrika Mashariki kwa sababu hakuna chombo chenye uwezo wa kutoa uamuzi kuhusu istilahi na matumizi ya lugha. Katika Mashairi na tungo zingine umepenya katika riwaya na unazusha tisho kubwa kwa Kiswahili sanifu. Maneno Kama vile kua, tua, sikia na lia huandikwa na wengi kana ‘kuwa, tuwa, sikiya na liya.’

Matumizi ya lugha isiyo sanifu kama haya yaweza kuvumilika yakiwa katika lugha ya mazungumzo au ya mashairi. Maandishi sanifu na wastani yanatakikana kusisitizwa. Kukosa kutumia mtindo mmoja wa kuandika maneno ya Kiswahili kunazusha mawazo kwamba kila moja yuko huru kuandika kiswahili vile apendavyo. Ikiwa tunafanya bidii kuandika maneno ya kiingereza kama vile ‘saw’, ‘sew’, ‘sow’ na ‘soul’ kwa kutumia irabu inayotakikana ni kitu gani kinachotushawishi kuandika ‘sikiya’ badala ya ‘sikia’? Tunahitaji chombo chenye uwezo katika eneo zima la ulimwengu wa kiswahili ili kusuluhisha masuala kama haya.

Baadhi ya watu wanaweza kuwa na hofu kwamba kuanzishwa kwa Kamati au Baraza kama hilo kutaweza kuhatarisha hali ya kiingereza katika Afrika Mashariki, hasa katika Uganda na Kenya. Hofu

kama hiyo haipaswi kuwepo kwa sababu kama nilivyoelezea, kusaidia matumizi ya kiswahili sanifu hakuizuii nchi kufuata sera ya lugha inayopendelea kiingereza vile vile ni wazi kwamba kiingereza si lugha ya Uganda, Kenya au Tanzania. Katika Afrika Mashariki kiingereza kitabaki kuwa lugha ya kigeni yenye umuhimu wa mawasiliano ya kimataifa na maandishi ya kitaaluma. Afrika Mashariki itaendelea kutumia kiingereza katika elimu ya juu na kuiwezesha kunufaika na maandishi ya kitaaluma na kiufundi.

MASWALI

(a) Pendekeza anwani mwafaka kwa taarifa hii? (alama 2)
(b) Kwa nini mwandishi anaona kuwa Kiswahili hakitiliwi maanani katika Afrika Mashariki? (alama 4)
(c) Kinachohitajika ili kiswahili kiweze kuimarika ni nini?
(c) Ni jambo gani hasa linalomshawishi mwandishi kuona kuwa Kiswahili sharti kiimarishwe? (alama 3)
(e) Unafikiri kilichochangia udunishaji huu wa kiswahili ni nini? (alama 4)
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yaliyotumika katika taarifa (alama 4)
  (i) Usanifu
  (ii) Umepenya
  (iii) Sera
  (iv) Kielelezo

MUHTASARI

Babu na nyaya zetu waliweza kifundisha vijana mambo mengi na watu walikuwa wamenyooka sawasawa. Ilikuwa ni wajibu wa kila mzee kupitisha hekima yake kwa vijana kila mara kwa njia ya methali, vitendawili, shirikina na hadithi zenye mafundisho maalum. Mambo yote haya yaliwafanya vijana kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo na watu wa marika yao. Watu walipokutana na wageni waliwaheshimu na waliheshimiwa. Ilieleweka kwamba neno ‘heshima’ lilikuwa la maana kwa kila binadamu na walijua kuwa heshima hainunuliki. Ilikuwa ni nadra sana kusikia zogo limetokea mahali popote.

Vijana wengi wa siku hizo walikuwa wakisifika kwa bidii, ushirikiano, uaminifu, utu, ukarimu, unyenyekevu, utiifu na upole. Wachache waliokosa sifa nyingi kati ya hizo walikosa wachumba. Hakuna aliyeweza kuficha tabia yake mbaya kwa muda mrefu kwa kuwa kila kijana pamoja na ndugu zake walifanya uchunguzi wa kutosha kabla ya kukubali posa. Upelelezi huu wa tabia ulianza tu mara mtu aliposema kuwa anataka jiko. Watu hawakujali ulemavu wa mtu na aghalabu waliokuwa na kasoro za kimwili waliweza kuoa ama kuolewa baada ya kuonekana kwamba wametimiza sifa nilizozitaja hapo awali.

Vijana walikubali kuelekezwa kutenda mambo mengi sana katika jamii bila ya maswali ama ubishi wowote. Hata walipoona mambo yamewawia magumu waliomba msaada kwa unyenyekevu mkubwa.

Hapo kale hapakuwa na mtindo wa vijana kupiga malapa mitaani. Waovu walikuwa wachache na waliweza kuadhibiwa na yeyote. Hakuna kijana aliyetoka kwao na kulala nje bila idhini ya wazazi wake na kama msichana angeweza kufanya hivyo, wazazi wangeweza kumlazimisha kurudi alipokuwa na arudi na huyo mtu aliyekuwa naye.

Maswali

(a) Kulingana na taarifa hii, unafikiri ni mambo gani hasa yaliyochangia kuimarika kwa nidhamu kwa upande wa vijana? (Maneno 40) (alama 8)

Nakala Chafu
Nakala Safi

(b) Eleza ujumbe unaojitokeza katika aya ya kwanza (maneno 40) (alama 6)
Nakala Chafu
Nakala Safi

(c) Fafanua aina za makosa na adhabu zilizotolewa hapo zamani kwa mujibu wa taarifa hii (maneno 30-35) (alama 6)
Nakala Chafu
Nakala Safi

C. <u>MATUMIZI YA LUGHA.</u>

(a) Andika sentensi hizi kwa wingi (alama 4)
(i) Buzi lililoibwa na jambazi lile limepatikana
(ii) Mwenye kelele usidhani kapoa

(b) Tunga sentensi ukitumia tashbihi zinazotokana na maneno yafuatayo
(i) Gundi
(ii) Chiriku
(iii) Lumbwi
(iv) Wali wa daku

(c) Kuna tofauti gani kati ya vyombo hivi
(i) Dira / saa
(ii) Tofautisha maneno haya
(iii) Sulubu / suluhu

(d) Sahihisha sentensi hizi (alama 4)
(i) Munyi alisanya vitabu yote siku ya Ijumaa
(ii) Fupa huu ulivunjwa na mpwakoko hii

(e) Andika sentensi ifuatayo bila kutumia neno ‘amba’
(i) Jembe ambalo lilinunuliwa jana limevunjika mpini (alama 2)
(iii) Mwizi ambaye amekuwa akitusumbua ameshikwa
(alama 2)

(f) Fuata maagizo uliyopewa katika kujibu yafuatayo
(i) Soma kwa bidii kijana. Utafaulu katika mitihani yako. (tumia …… nge) (alama 2)
(ii) Kisu kinachonolewa ndicho kinachopata (geuza hadi hali ya mazoea) (alama 2)

(g) Andika maneno mengine mawili yenye maana sawa na yafuatayo (alama 4)
(i) Daawa
(ii) Bughudha
(iv) Abadani
(v) Fitina

(h) Kanusha sentensi hizi
(i) Mwana yule alikuwa amekamilisha kuchimba mtaro alipojikata mguu
(ii) King'ora kililia kioo kilipovunjwa

(i) Weka viambisho vinavyofaa sentensi zifuatazo
(i) Walimu _____ li ____ ona mtoto _____ dogo _____ kianguka matopeni.
(ii) Mwavuli huu _____ eusi _____ a mzungu ame _____ nunua jana.

(j) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kufanyiza
(i) Mwalimu amefanya mwanafunzi wake ajue umuhimu wa bidii masomoni (alama 2)
(ii) Paka ameyanywa maziwa (geuza hadi kauli ya kufanywa) (alama 2)

SEHEMU TATU
USHAIRI

9. Tusitake kusimama, bila kwanza kutambaa,
Au dede kuwa hima, kabula hatuyakaa
Tutakapo kuchutama, kuinama kunafaa
Tujihimu kujinyima, makubwa kutoyauyaa

Tusitake kuenenda, guli lisipokomaa
Tujizonge na mikanda, inapochagiza njaa
Na mazuri tukipenda, ni lazima kuyaandaa
Tujiase kujipinda, kujepusha na balaa
Tusitake uvulana, au siga kuzagaa
Tushikaye nyonga sana, tunuiyapo kupaa
Kama uwezo hapana, tutoelee dagaa
Tujiase hicho kina, maji yajapokujaa

Tusitake vya wenzetu, walochuma kwa hadaa
Wanaofyatua vitu, na kisha vikasambaa
Uwezo hatuna katu, umaskini fazaa
Tujihimu kula vyetu, siendekeze tamaa

Mtaka kuiga watu, kufata kubwa rubaa
Vyao vijaile kwetu, vifaa vingi vifaa
Tunamezwa na machatu, tusibakishwe dhiraa
Tujihimu kilo chetu, hata kama twapagaa

<u>Maswali</u>

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)
(b) Chambua ubeti wa tatu na nne kwa upande wa vina na mizani (alama 4)
(c) Thibitihsha jinsi kunga ya inkisari na mazida inayojitokeza katika shairi hili

(alama 3)

(d) Mwandishi ana ujumbe gani katika shairi hili kwa wasomaji wake? (alama 2)
(e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari (alama 4)
(f) Taja misamiati yoyote minne ya hatua ya maisha ya binadamu na ueleze yake.
(alama 4)

2. Alikuwa mtu duni, alozongwa na shakawa
Hana alichoauni, wala alichoambuwa
Walikimwita mhuni, na thamani kumtewa
Utamwonea amani, jinsi ya alivyokuwa
Mwepesi wa kusahau

Alipita mtaani, kuomba kusaidiwa
Mtoto wa kimaskini, riziki haizumbuwa
Alizubaa njini, lake jua na mvuwa
Mwepesi wa kusahau

Ekosa kwenda chuoni, kwani alibaguliwa
Daima kawa mbooni, akitafuta afuwa
Chumia chungu mekoni, furaha kwake haiwa
Mwepesi wa kusahau

Wakati ukabaini, mjiuga akatambuwa
'Katoka usingizini, napo kwenye kukawa
Watu wakamuamini, kuwa mtu wa mvuwa
Kumbe vile atahuni, na ujeuri kuingiwa
Mwepesi wa kusahau

Leo kawa Sultani, mwingine katu hajawa
Hatamani na haoni, nyuma aliyochukuwa
Anga kwake limeguni, gubi amegubiliwa
Mwanadamu maalum, hakika ukichinguwa
Mwepesi wa kusahau

<u>Maswali</u>

(a) Eleza ujumbe unayojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili (alama 4)
(b) Fafanua maana ya kibwagizo katika shairi hili (alama 3)
(c) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu (alama 2)
(d) Je mwandishi amefaulu katika kuzingatia arudhi za utunzi? Fafanua (alama 6)
(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 5)
(i) Alichoauni
(ii) Alizubaa
(iii) Ukabaini
(iv) Sultani
(v) Maluum

KISWAHILI IV

SEHEMU YA KWANZA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
INSHA.

Mtindo **(alama 4)**
- Ni mpangilio wa insha kijumla: utangulizi, kiwiliwili na hitimisho
- Ni mpangilio wa aya na sentensi katika kutenganisha hoja au mawazo mbalimbali
- Ni unadhifu wa kazi

Msamiati **(alama 5)**
- Ni umbaji na uandishi na usanii wa lugha
- Matumizi ya msamiati kulingana na muktadha
- Uzito wa lugha

Maudhui **(alama 5)**
- Yaliyomo katika insha
- Mawazo/hoja zinazoshihirisha ukweli wa anwani au zinazofafanua anwani hiyo

Sarufi **(alama 6)**
- Usingatiaji wa kaida za lugha. Utumiaji wa lugha kitaalamu
- Uakifishaji n.k
- Kila unapopata kosa kwa mara ya kwanza liadhibu kwa kiondoa alama nusu (½) usiadhibu zaidi ya makosa kumi na mbili (12)

Hijai **(alama 3 za kuondolewa)**
- Ni uendelezaji wa maneno
- Kila kosa linapojitokeza kwa mara ya kwanza liadhibu kwa kuondoa alama nusu (½) usiadhibu zaidi ya makosa sita (6)

SEHEMU YA PILI
UFAHAMU, MUHTASARI, MATUMIZI YA LUGHA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

UFAHAMU

(a) Matumizi ya kiswahili
- Uimarishaji wa lugha zetu
- Utumiaji mbaya wa lugha ya kiswahili **(alama 2)**

(b) Kinatumiwa kiholela bila uzingativu
- Hakuna chombo chenye uwezo kutoa uamuzi juu ya matumizi ya lugha
  (alama 3)

(c) Kubuniwe chombo chenye uwezo wa kitoa uamuzi juu ya matumizi ya lugha hii
- Kuanzishwa kwa kamati au baraza ya kiswahili **(alama 3 X 1 = 3)**

(d) Kiingereza si lugha ya asili
- Kiswahili ni lugha ya kiasili inayoendelea kutumika kote duniani **(alama 3)**

(e) Imani kuwa kiswahili kinaweza kutumiwa kwa njia yoyote ile bila uzingativu
- Sera ya lugha ya nchi nyingi zinapendelea kiingereza **(alama 1½ X 2 = 3)**

(f) (i) Usanifu – Usahihi, utumiaji lugha kwa njia sawa
(ii) Umepenya – Umeingia/umesambaa
(iii) Sera – Mtindo wa kufuatwa
(iv) Kielelezo – Mfano **(alama 4 X 1 = 4)**

SEHEMU B: MUHTASARI

(a) Babu na nyanya walifundisha vijana mambo mengi
- Waliokosa kuwa na sifa nzuri walikosa wachumba
- Uchunguzi wa kutosha ulifanywa dhihi ya tabia ya mtu
- Vijana walikubali kuelekezwa
- Adhabu ilitolewa kwa wale waliokosa

(alama 4 X 2 = 8)

(b) Babu na nyanya kutunza vijana
- Watu kuwa wamenyooka
- Vijana waliwaheshimu wakubwa
- Wageni waliheshimiwa
- Ulikuwa nadra zogo kulokea

(alama 5 X 1 = 5)

(c) Aliyekosa sifa nzuri alikosa mchumba
- Kutoka kwao na kulala nje angerudishwa aende akalete huyo aliyekuwa naye **(alama 2 X 2 = 4)**

(a + b + c = 17, Utiririko = 3)

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) Mabuzi yaliyoibwa na majambazi yale yamepatikana **(alama 2)**
(ii) Wenye kelele msidhani kapoa **(alama 2)**

(b) (i) Hata kama fundi
(ii) Kuwa na maneno mengi kama chiriku
(iii) Kuwa kigeugeu kama lumbwi
(iv) Kuadimika kama wali wa daku

(c) (i) Dira – huonyesha upande/hutumiwa na wasafiri kujulia wanakoelekea
Saa – chombo kinachoonyesha saa **(alama 2 x 1 = 2)**

(ii) Sulubu – kazi ya kutumia nguvu/bidii/ushupavu
Suluhu – utatuzi, jibu **(alama 2 x 1 = 2)**

(d) (i) Munyi alikusanya vitabu vyote siku ya Ijumaa **(alama 2)**
(ii) Fupa hili lilivunjwa na mbwakoko huyu **(alama 2)**

(e) (i) Jembe lililonunuliwa jana limevinjika mpini **(alama 2)**
(ii) Mwizi aliyekuwa akitusumbua ameshikwa **(alama 2)**

(f) (i) Ungesoma kwa bidii kijana ungefaulu katika mitihani yako **(alama 2)**
(ii) Kisu kinolewacho ndicho hupata **(alama 2)**

(g) (i) Kesi/mashtaka
(ii) Hasina/mori/ghadhabu
(iii) Katu/Kamwe
(iv) Porojo

(h) (i) Mwana yule hakuwa amekamilisha kuchimba mtaro alipojikata mguu **(alama 2)**
(ii) Kingo'ra hakikulia kioo kilipovunjwa **(alama 2)**

(i) (i) Walimu walimuona mtoto mdogo akianguka matopeni **(alama 2)**
(ii) Mwavuli huu mweusi wa mzungu ameununua jana **(alama 2)**
(j) (i) Mwalimu amemjulisha mwanafunzi wake umuhimu wa bidii masomoni **(alama 2)**
(ii) Maziwa yamenywewa na paka **(alama 2)**

SEHEMU YA TATU
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
USHAIRI

(a) Kujinyima
- Kila jambo na wakati wake
(alama 1 x 2 = 2)

(b) Vina: Ubeti watatu vina vya kati ni <u>na</u>, vina vya mwisho ni <u>aa</u>
Ubeti wa nne: vina vya kati ni <u>tu</u> na vya mwisho ni <u>aa</u>
Mizani: Kila mshororo ina mizani kumi na sita
Ukwapi mizani nane na utao mizani nane –8, -8,
(Vina hoja mbili 2 x 1 = 2)
(Mizani hoja mbili 2 x 1 = 2)

(a) Inkisari – ufupishaji wa neno
Walochuma – waliochuma
Siendekeze – usiendekeze
Kilo – kilicho
Mazida – urefushaji wa maneno
Kabula – kabla
(inkisari 2 x 1 = 2)

(Mazida 1 x 1 = 1 Jumla alama 3)

(b) Tusijiinue/kujikaza kwa mambo ambayo hatujafikia

- Tufuate mambo hatua kwa hatua kwa taratibu nzuri ***(alama 3 x 1 = 3)***

(c) Mtu asiwe na tamaa ya kusimama kabla hajatambaa au atake kusimama dede kabla hajaweza kukaa kitako. Ni heri kuanzia hatua za mwanzo halafu hatua zingine zifuate wala sio kinyume chake ***(alama 4)***

(d) Kusimama – wima
Kutambaa – kutembea kwa magoti
Kusimama dede – kusimama bila kusaidiwa
Kukaa – kwa kitako
Kuchutama – chuchumaa, kaa kitako bila kugusa chini ***(alama 4 x 1 = 4)***

10.(a) Mtu fulani hakuwa na sifa zozote nzuri mwenye shaka. Hana lolote alichojupatia hata cha kupewa ikabidi kuona cha thamani kuwa duni. Afaa kuonewa huruma kwa namna alivyokuwa ***(alama 4)***

(b) Mtu aweza kusahau yaliyofanyika kwa haraka ***(alama 3)***

(c) Unne/tarbia – lina mishororo minne kila ubeti
Msuko –kibwagizo kimefupishwa ***(alama 2 x 1 = 2)***

(d) Ndio - idadi ya mishororo ni sawa kila ubeti (minne)
- Mizani 16 kila mshororo isipokuwa katika kibwagizo ni nane
- Vina vimetiririshwa (kuna urani) kina cha kati ni ‘ni’ cha mwisho ni ‘wa’ ***(alama 3 X 2 = 6)***

(e) (i) Alichosaidiwa
(ii) Kutokuwa makini/bila tahadhari
iv Kuelewa
v Kiongozi
(v) Binadamu ***5x1=5***

KISWAHILI V
SEHEMU YA KWANZA
INSHA

1. Wewe ni katibu wa chama cha wakulima cha kiteka: Tayarisha kumbukumbu za mkutano mliofanya hivi majuzi.

2. Andika insha juu ya: Maisha yangu ifikapo mwaka wa 2020.

3. Ndugu yako ameshtakiwa kwamba mnamo tarehe 12 Agosti mwaka jana, alipatikana na hatia ya ulanguzi wa dawa za kulevya. Amekutaja kuwa ulikuwa na yeye wakati huo nyumbani na umeitwa kutoa ushahidi juu ya:
alipokuwa wakati huo

Shughuli zake za kawaida
Historia yake
Maoni yako juu ya kesi hii.
Andika insha kuhusu vile utakavyomtetea mahakamani.

4. Andika insha juu ya methali hii; Mtenda jambo asishe ni kama asiyetenda.

SEHEMU YA PILI
UFAHAMU, MUHTASARI, MATUMIZI YA LUGHA

SEHEMU A – UFAHAMU

1. ***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:***

Miaka michache iliyopita, kila aliyekuwa amesoma alikuwa na bahati ya kupata kazi katika ofisi za humu nchini. Wote waliofika darasa la saba au pengine kidato cha pili na zaidi wale waliofuzu mtihani wa kidato cha nne, walinyakuliwa juu kwa juu na wizara mbalimbali za serikali au pengine waliandikwa kazi na makampuni. Kwa vile kila moja wao alipata kazi ya kuajiriwa, hakuna aliyejishughulisha na kazi za mtu binafsi kama useremala, uashi, ukulima, uvuvi na kadhalika- kazi kama hizo ziliachiwa wale tu ambao hawakupata fursa ya kuenda shule.

Siku hizi mambo yamebadilika. Licha ya kuwa na elimu ya darasa la saba au kidato cha pili na pengine cha nne, hata wale wenye shahada za vyuo vikuu nao pia wamezifungia shahada hizo mashubakani zikiota ukungu huku wenyewe wakijipurukusha kulima au kufuga; na wale ambao bado hawajakata shauri kama hili, wako barabarani wakipiga lami.

Wakoloni walifanya kosa moja kubwa sana ambalo tumeligundua tu baada ya kunyakua uhuru wetu. Kosa lenyewe ni lile la kuwafanya wananchi waliopata elimu wasipende kushika kazi zinazochafua mikono.Walijua tu kwamba mashamba yao na hata mitambo yao ingalifilisiwa na ile ya waafrika; kwa hivyo ingaliwabidi hata wao waje wawatumikie wenyeji. Ndipo walipokata shauri kutowaamsha waliolala ili wasije wakalala wao.

Katika karne hii, wataalamu wameshawishika kuitumia elimu yao kufanya kazi za mashamba, ujenzi na ufundi wa mitambo. Ijapokuwa baada ya kazi kama hizo mikono huwa imejaa tope au masizi, pato lake ni kubwa ajabu. Jambo la kuvutia zaidi katika makazi kama haya ni kwamba mwananchi huwa ni ‘bwana’ mwenyewe, hujitegemea mwenyewe bila kochokocho.

Kila moja wetu yuaelewa kinaganaga kwamba kazi kama ya ukulima huleta donge kubwa zaidi ya kazi zote; kwani kila mfanyikazi humwelekea mkulima baada ya kumaliza kazi yake. Mkulima naye hutoa jasho jingi wakati wa kulima shamba. Baadaye atapekua magugu na visiki aviweke katika matita ili aviteketeze moto. Baada ya muda kidogo atapanda na angoje hadi mbengu zake ziaanze kuchipuza. Mara maua huchanua na mazao kujionyesha. Baada ya kuvuna, kazi yake kubwa huwa ni kuanika na kuanua nafaka zake. Wakati huo, mazao yake huwa yatanga, mara yuapanga mara yuapangua mipango juu ya uuzaji. Mazao yafikapo nyumbani, pengine mkulima huipamba nyumba yake na akawaita marafiki zake ili awakirimu kwa vyakula na vinywaji. Karamu ikiisha hana budi kupambua mapambo yote. Huyoo, aenda kuuza bidhaa zake; akirudi yuakaa raha mstarehe akila na kuburudika pamoja na familia yake. Je kuna kazi yenye raha zaidi ya ukulima?

Watu wengi hufikiria maana ya neno ‘kulima' ni kushika jembe tu. Hiyo si kweli kwani kuna ukulima namna nyingi, kama vile ufugaji wa ng’ombe, mbuzi au kuku. Hata ufugaji wa samaki au utunzaji wa nyuki pia waweza kuitwa ukulima. Dhamira ya taifa letu changa ni kuwapatia mwangaza wananchi wake waliomo mashuleni, kwamba wangojewa kwa hamu wajiunge na wenzao katika kulijenga taifa lenye

nguvu, ili katika kujisaidia wenyewe pia waongeze pishi katika kulipa taifa maongozi mema yasiyokinai kazi zilizokuwa zikiitwa ‘chafu' lakini ambazo ndizo hasa kiini cha maendeleo na kujitegemea.

a) Kulingana na habari uliyosoma, ni mambo gani hasa yaliyochangia kupuuzwa kwa kazi za mtu binafsi? (alama 3)
b) Wakoloni walikuwa na lengo gani kwa kufanya waafrika waliosoma kuchukia kazi za mikono? (alama 2)
c) Unafikiri mwandishi wa taarifa hii alikuwa na dhamira gani kwa wasomaji wake? (alama 2)
d) ..‘Wamezifungia shahada hizo mashubakani zikiota ukungu huku wenyewe wakijipurukusha kulima au kufuga’ Mwandishi anamaanisha nini katika kauli hii? (alama2)
e) Kwa nini wasomaji wa kisasa wameanza kufanya kazi ya ukulima? (alama 3)
f) Eleza maana ya semi hizi kama zilivyotumiwa katika taarifa: (alama 4)
   i) Kata shauri
   ii) Kuwa bwana
g) Mwandishi ametumia maneno yenye maana ya kinyume kwa mfano ‘panga na pangua’; yataje maneno mengine mawili yaliyotajwa na vinyume vyao huku ukieleza maana ya kila moja ya maneno hayo. (alama 4)

2. **SEHEMU B MUHTASARI**

Wataalamu wengi wamelieleza neno hili fasihi. Kwa hivyo fafanuzi na nadharia juu yake ni nyingi. Lakini hata hivyo, karibu wote wamehusika zaidi ama na fasihi maandishi.

Ukitazama fasihi kwa umbo lake la nje na umbo lake la ndani utaona kuwa ni taaluma inayojengwa na maneno, na maneno yenyewe hutumia fani maalumu za aina mbali mbali kutolea makusudi au maudhui ambayo humzingatia binadamu maishani… Japokuwa sanaa hii ya fasihi mara nyingine huzungumzia vitu, lakini hilo ni umbo lake la nje tu. Umbo lake la ndani hasa hujishughulisha na binadamu na ndiye kiini cha fasihi; ndiye shabaha yake.

Fasihi simulizi ni masimulizi tunayopokea mdomo kwa mdomo. Si masimulizi yaliyoandikwa tangu awali. Kwa ajili hii basi tutaona kuwa katika fasihi hii mna utumiaji wa ulumbi (ufundi wa kusema). Kwa vile chombo cha kutongolea fasihi simulizi ni mdomo, hapana budi kuwepo na mwenye huo mdomo, yaani msimulizi. Msimulizi huyo, anaposimulia anachosimulia, huwa na nafasi si ya kutumia mdomo wake tu kujieleza, bali hali, uso, mikono na mwili wake mzima. Nafasi hii mwandishi wa fasihi maadishi hanayo kwa sababu yeye, kinyume na msimulizi wa fasihi simulizi, huwa hanao mbele zake watu wa kumsikiliza au kumtazama. Badala yake yeye hupambana na msomaji.

Msimulizi katika fasihi simulizi ana nafasi ya kutazama kama amefaulu au la, yaani wasikilizaji wake wanamsikiliza au hawamsikilizi. Kama hawamsikilizi, basi huwa na nafasi ya kubadilisha mbinu wakati huo huo asimuliapo ili wamsikilize. Na hapo ndipo aonyeshapo ufundi wake katika sanaa ya usimuliaji. Lakini nafasi hiyo mwandishi hanayo anapoandika.

Tena msimulizi ana nafasi ya kuwatumia wasikilizaji wake kama wahusika asimuliapo ayasimuayo. Hii ndiyo sababu msimulizi aweza kumfinya mtu, kuigiza jambo, au kuwafanya watu waimbe, au kufanya matendo mbalimbali mengine. Ufundi na nafasi hiyo ni waandishi wachache wanaoimudu na kuitumia maana huhitaji umahiri wa hali ya juu. Kwa njia hii msimulizi kwa upande mmoja huwa na wahakiki palepale, hali mwandishi ni mpaka andiko lisomwapo ndipo anapoweza kuwapata.

Kwa upande mwingine, fasihi simulizi ina wasikilizaji zaidi kuliko wasomaji; wasikilizaji ambao mara nyingi waweza kuwa wahusika wa jambo linalosimuliwa. Wao wana nafasi ya kuuliza maswali, kuonyesha hisi zao, kuhimiza, kukumbusha, na hata kujibizana na msimulizi. Msomaji hana nafasi ya aina hiyo asomapo andiko.

a) Pendekeza anwani mwafaka wa taarifa hii. (alama 2)
b) Kwa kutumia maneno yasiyopungua kumi(10) wala kuzidi ishirini(20), eleza maana na lengo la fasihi kama ilivyotolewa katika taarifa. (alama 4)
Nakala chafu
Nakala safi

c)Mpokezaji wa fasihi andishi ana vikwazo gani akilinganishwa na yule wa fasihi simulizi? (maneno 70-80) (alama10)
Nakala chafu
Nakala safi

d) Wapokeaji wa fasihi simulizi wanawezaje kuathiri uwasilishaji wa fasihi? (maneno 20) (alama 4)
Nakala chafu
Nakala safi.

3. **SEHEMU C: Matumizi ya lugha**:

a) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya umoja.
i) Mkitusaidia, nasi tutawanunulia zawadi nzuri. (alama 2)
ii) Waliposikia sauti hizo, waliwarushia mawe hadi wakafa. (alama 2)
b) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii.
i) Alifuatwa hadi akashikwa na mmeo dukani. (alama 2)
ii) Kuna tofauti gani kati ya sentensi hizi?
Ukirudi tena, nitakuadhibu vilivyo.
Ukirudi, tena nitakuadhibu vilivyo. (alama 2)

c) Sahihisha sentensi hii bila kubadilisha maana.
i) Mkutano ulihairishwa hati ijumaa. (alama 1)
ii) Fuata maagizo uliopewa katika kujibu swali hili.
Wananchi walimpokea mjumbe kwa shangwe na vigelegele. (Tumia.. pokelewa). (alama 2)
d) Igawe fungutenzi ifuatayo kwa kubainisha kila sehemu huku ukionyesha na kufafanua maana ya visehemu hivyo vinavyounganishwa ili vifanye sentensi kamili. (alama 6)

Alikiangusha

e) Tunga sentesi ukitumia maneno yafuatayo ili kudhirisha tofauti ya maana kati yao.
vi (alama 3)
(i) bovu (iii) bofu
(ii) pofu

f) Chagua neno ambalo haliambatani na mengine.
i) nyerere, ushanga, bangili, shimere. (alama 1)
ii) bunga, punguani, mkatili, baradhuli. (alama 1)
iii) Unganisha sentensi hizi ili ziweze kuwa sentensi moja.
1. Kelvin ni mwadilifu
2. Kelvin aliteuliwa kuwa kiongozi. (alama 2)

g) Eleza maana ya misemo hii
   i) Shika sikio. (alama 2)
   ii) enga enga mtoto. (alama 2)

h) Andika upya sentensi hii kwa kuandika neno lenye maana sawa na lile lililopigwa mstari.
   i) Mfalme yule alighadhabika alipofedheheshwa na watumishi wake katika karamu ile. (alama 1)
   ii) Andika upya sentensi hii kwa kuandika kinyume cha kila neno lililopigwa mstari
   Wifi alipovaa nguo na kusimama, ajuza yule alikaa. (alama 2)

i) Andika sentensi hii katika hali ya udogo .
   i) Mtoto mdogo alipatikana ndani ya nyumba ile. (alama 2)
   ii) Eleza maana ya PO kama ilivyotumiwa katika sentensi hizi. (alama 2)
   Wanafunzi wachelewapo, huchapwa viboko vinne.
   Wanafunzi wanapochelewa, huchapwa viboko vinne.

j) Andika sentensi ifuatayo kwa wakati uliopo.
   i) Yusuf hakulima shamba lake. (alama 1)
   ii) Andika sentensi hii katika msemo halisi.
   Mariam alimshukuru Edith na kutaka kujua wakati aliporudi kutoka nyumbani. (alama2)

1. SEHEMU TATU
USHAIRI

1. Siku moja itafika, nijifungie safari;
   Safari ndefu hakika, isiyotaka magari;
   Magari hayatafika, wala meli za fahari;
   Siku yangu!

2. Siyo nadhiri naweka, katu siyo ubashiri;
   Ni mwendo uliopangika, ni muhali kughairi;
   Kwenda nawajibika, kubeta sina hiari;
   Siku yangu!

3. Roho inanitutika, kila nikitafakari;

Ziara is'o shirika, hata akhi hujibari;
Wanabaki kuteseka, na kunipami kwaheri;
Siku yangu!

4. Siku itakapofika, zamani za kuabiri;
Kutazuka hekaheka, kibuhuti cha Suduri;
Na mwingi mno wahaka, kwa wendani na wambari;
Siku yangu!

5. Ziara itafanyika, na mola ndiye Sayari;
Ngia itanimulika, nifike pasi usiri;
Niwache mkitamka, mabayangu na mazuri;
Siku yangu!

6. Binadamu hutoweka, siku yake ikijiri;
Ugeni una mipaka, nami leo nahajiri;
Mipaka yangu yafika, mungu amenihitaji;
Siku yangu!

7. Sina budi kuitika, wito huu wa kahari;
Ziara kukamilika, moyoni sifanyi ari;
Nenda zangu haraka, moyoni sifanyi ari;
Siku yangu!

8. Haki sasa naondoka, ni mja sina hiari;
Huko nitasetirika, dahari hata dahari;
Buriani wahibaki, na maswahaba kwaheri;
Siku yangu!

Maswali:

a) Mtunzi wa shairi alikuwa na dhamira gani katika kutunga shairi hili? (alama 3)
b) Idhini ya ushairi/ mtunzi inajitokezaje katika shairi hili? (alama 4)
c) Kwa kutumia ithibati kemkem (kutoka katika shairi hili), eleza kwa undani muundo wa shairi hili. (alama 4)
d) Eleza ujumbe unaotolewa na mwandishi katika ubeti wa saba na nane. (alama 4)
e) Mafungu yafuatayo yametumiwa kumaanisha nini?
   i) ni muhali kughairi. (alama 1)
   ii) ziara is'o shirika. (alama 1)
f) Toa mifano miwili ya jazanda katika utunzi huu. (alama 3)

26. Mtu na awe na macho, kamili yote mawili,
Na kila kitu ambacho, alikiumba Jalali,
Kama hana kichwa kwacho, si mtu bali tumbili,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Wa kila kitu mwilini, ni yeye huwa wakili,
Na yeye ndiye mashini, ya kuendesha kauli'
Kito cha matumaini, usukani wa akili,

Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Wakili wa kila kitu, viungo vyote vya mwili,
Kichwa kinaleta utu, kwa sifa ya taamuli,
Ama ufanywe utu, kwa sifa ya taamuli,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Mtu huwa ni sanamu, hajaumbika kamili,
Kama hanayo fahamu, fahamu yake thakili,
Si kichwa cha binadamu, binadamu wa asili,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Tazama mwendawazimu, kichwa kilotanakali,
Huingiwa na zahamu, kukiuka ya awali,
Mfano wa marehemu, kila kiungo hajali,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Kichwa chenyewe si hoja, hoja ubongo mkali,
Kiwe kijua vioja, kwa kamili atikali,
Si kichwa chenye kuvuja, si kichwa chenye manzili,
Kichwa ni yeye wakali, wa kila kitu mwilini.

Kichwa kiwe peke, juu ya kiwiliwili,
Shingoni ukitungike, na nywele kama ulimi,
Moyo visiunganike, kichwa hakitahimili,
Kichwa ni yeye wakili, wa kila kitu mwilini.

Maswali:

a) Fafanua ujumbe unaobebwa na kiitikio cha utungo huu. (alama 3)
b) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)
c) Mja asiye na 'kichwa' amefananishwa na nini? Toa mifano miwili. (alama 2)
d) Ingawa kichwa ni muhimu, ni sharti kishirikishwe na viungo vipi ili kipate ukamilifu wake? (alama 3)
e) Shairi hili ni la bahari gani? Toa sababu. (alama 2)
f) Eleza mpangilio wa vina katika ubeti wa pili. (alama 2)
g) Taja na ueleze maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi.
   i) Neno la mwisho katika utao wa mleo ubeti wa kwanza. (alama 2)
   ii) Neno la mwisho katika ukwapi wa mwanzo ubeti wa tano. (alama 2)

SEHEMU YA KWANZA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
INSHA.

1. Kila insha ina alama 20-jumla-40
2. Tumia mtindo huu kukadiria alama
   a) Maudhui -5
   b) Mtindo -4
   c) Sarufi -6

d) Msamiati - 5 __
20
Tajilia -3

3. MAELEZO

a) Maudhui

- Ni mada au maelezo au vipengele ambavyo mtahiniwa anahitajiwa kutaja katika insha yake
- Mwanafunzi ataje mawazo au hoja zinazooana na anwani ya insha yake. Namna ya kutunza:-

Ikiwa ametaja hoja zote –5
Ametaja zaidi ya nusu -3½
Ametaja chini ya nusu -2
Hakutaja chochote -0

b) Mtindo

Ni mpangilio wa insha –Utangulizi, maelezo ya mwisho / hitimisho.
Namna anavyotoa mawazo yake na jinsi anavyotiririsha.
Namna anavyojenga insha yake na umbo lake kijmla

Tuzo: Hutegemea mambo yaliyotajwa hapo juu

Mtahiniwa hapewi 0

c) Sarufi

Ni matumizi ya lugha kulingana na kaida za kisanifu.
Namna inavyotoa mawazo yake na jinsi anavyotayarisha
Matumizi ya nyakati, minyambuliko, herufi kubwa na ndogo / nakifishaji, kutenganisha, au kukutanisha maneno, n.k.

Namna ya kutunza:

Kwa kila kosa la sarufi, ondoa alama ½, Usiondoe zaidi ya nusu 12 kwani insha moja yaani.
(alama 6)
Kosa moja likitokea, liadhibiwe au kutolewa alama ½ lakini kosa hilo likirudiwa, linakosolewa tu bali alama ½ haiondolewi.
Jumla ya alama za kisarufi zilizopatikana huhesabiwa na kuondolewa kutoka 6.

Mfano:- yaani ikiwa umepata makosa manne itakuwa ½ x 4 = 2

Tuzo itakuwa 6 – 2 = 4

d) Msamiati:

Ni utumiaji wa msamiati wa lugha ya kiswahili ipasavyo. Ni uzito wa lugha ya mwanafunzi
Tuzo: Huweza kukadiliwa kwa daraja tatu:-
Juu ya wastani.
Wastani.
Chini ya wastani.

Mtahiniwa hapewi 0

e) Tahajia au hijai

Makosa ya tahajia ni maendelezo mabaya ya maneno.

Tuzo:- Ondoa alama ½ kila unapopata kosa la tahajia. Kosa linaporudiwa, usiondoe alama kwa mara ya pili, kijumla usiondoe zaidi ya alama ½ (6) yaani alama 3 katika insha moja.

Mfano wa namna ya kutuza kijumla

Maudhui - Ametaja zaidi ya nusu -4
Mtindo - Juu ya wastani -3
Sarufi - Makosa 9 x ½ = 4 ½ - 6 – 4 ½ = 1 ½
Msamiati - Juu ya wastani -3
Tahajia - Makosa 3 = 3 x ½ = 1 ½

= Maudhui -4
Mtindo -3
Sanifu -1 ½
Msamiati -3
Jumla = 11 ½ - 1 ½ (Tahajia) = 10
Alama 10/20

Baada ya kujumlisha na kuondoa alama za tahajia, Iwapo kuna nusu yake, hujazwa kuwa alama kamili.
K.m. 10 ½ / 20 = 11/20

SEHEMU YA PILI
MATUMIZI YA LUGHA, UFAHAMU, MUHTASARI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

UFAHAMU.

1.(a) Kuajiriwa na wizara mbalimbali za serikali kwa urahisi (kwa wale waliopata elimu):
Kuandikwa kazi na makampuni
Wakoloni walifanya kosa la kufanya waliosoma kuchukia kazi za mikono.
Hoja zote tatu 3 x 1 = 3

(b) Walijua kwamba kama waafrika wangefanya kazi za binafsi / mikono, ingefilisha mashamba yao (ya wakoloni) kwani waafrika hao wenye elimu wangetumikia wenyeji. 1 x 2 = 2

(c) Anawatahadharisha wasomi dhidi ya kuchukia kazi za binafsi na kutarajia kuajiriwa. Anawataka wawe tayari kujitegemea baada ya kupata elimu. (alama 2)

(d) Anamaanisha kwamba watu waliopata shahada hawapati kazi za ofisi na hivyo huwajibika kufungia shahada hizo zao masandukuni na kuanza kufanya kazi za kibinafsi kama kulima, useremala n.k.
Shahada hizo haziwafaidi kwa vyovyote maana haziwasaidii kujipatia riziki.
Hoja moja 1 x 2 = 2

(e) Kazi ya ukulima ina pato kubwa – donge kubwa zaidi ya kazi zote.

Kazi za kuajiriwa zimekuwa nadra kupatikana.
(Hoja zote mbili alama 3)

(f) i.) Kata shauri – amua
ii) kuwa bwana – kuwa wa kuheshimiwa, wa kutegemewa na mwenye hadhi.
(2 x 2 = 4).

(g) - Kuanika na kuanua.
- Pamba na pambua.
- Kuanika – weka juani ili (nafaka) ikauke.
- Kuanua – kusanya (nafaka) ili ipelekwe ndani baada ya kukauka.
- Pamba – kuweka nyumba kuwa katika hali nzuri (kwa mapambo).
- Pambua – kuondoa mapambo yaliyokuwa yamewekwa nyumbani baada ya karamu. 1 x 4 = 4.
+ 4 + 4 = 20.

MUHTASARI.

a) Fasihi simulizi – au anwani yoyote mwafaka (alama 2)
b) Fasihi ni taaluma inayojengwa na maneno ambayo hutumia fani mbalimbali.
Hushughulikia binadamu na ubinadamu wake maishani
Hoja mbili = 2 x 2 = 4
Ondoa alama moja (1) anapozidisha maneno matano juu ya ishirini.

c) - Hana nafasi ya kutumia viungo vingine vya mwili au ishara kufaulisha mawasiliano
- Hana nafasi ya moja kwa moja ya kujifathrini kama amefaulu au la
- Hana nafasi ya kuwatumia wapokeaji wa kazi yake
- Hadhira au wapokeaji wa kazi yake ni ndogo.
Hoja zote nne = 2 x 4 = 8 ; Utiririko = 2 ; Jumla = 2 + 8 = 10
Ondoa alama moja (1) kwa maneno kumi yanayozidishwa usiondoe zaidi ya alama 3.

d) - waweza kuwa wahusika.
- wana nafasi ya kuuliza maswali.
- waweza kuonyesha hisia zao.
Hoja tatu – 1 x 3 = 3 ; Utiririko – alama 1 ; Jumla = 1 + 3 = 4
Ondoa alama 1 idadi ya maneno inapozidishwa kwa maneno tano juu ya ishirini.
Usiondoe zaidi ya alama mbili.
Jumla 2 + 4 + 10 + 4 = 20.

<u>MATUMIZI YA LUGHA.</u>

a) Ukinisaidia, nami nitakununulia / nitamnunulia zawadi nzuri. (alama 2)
b) Aliposikia sauti hiyo, alimrushia jiwe hadi akafa. (alama 2)
c) i) Mume wake ndiye aliyemshika huyo (bibi) dukani.
Aliyekuwa akifuatwa (bibi) alishikwa pamoja na mmewe dukani. *(1 x 2 = 2)*
ii) – Mtu anaonywa asirudi, maana akifanya hivyo (kurudi) ataadhibiwa.

Ya pili – Mtu anaonywa kuwa akirudi, ataadhibiwa mara nyingine (kama alivyoadhibiwa awali) – Tayari ameadhibiwa. (1 x 2 = 2).

d) i) Mkutano uliahirishwa hadi ijumaa. (alama 1)
ii) Mjumbe alipokelewa na wananchi kwa shangwe na vigelegele. *1 x 2 = 2*

e) i.) A/li/ki / angu/sha
A- kiwakilishi cha nafsi (ya tatu) – yeye.
Li –kiwakilishi cha wakati (uliopita)
Ki – kirejeleo cha ngeli ya KI – Vi (umoja) inarejelea
Kitu – kitendwa.
Angu – shina la kitenzi.
Sha – Hali ya kutendesha.
Kugawa vizuri sehemu zote – alama 1
Kueleza / kubainisha visehemu 1 x 5 = 5
Jumla 1 + 5 = 6.

e) (i) bovu – kilichooza, kisicho na thamani
(ii) bofu – mfuko wa mkojo tumboni
(iii) pofu – asiyeona.
*sentensi yoyote sahihi maadam maana zilizotajwa hapo juu zijitokeze waziwazi.
1 x 3 = 3

f) i) Shimere ii) mkatili

g) i) kukataza mtu jambo fulani – kama daktari anavyowakataza watu vyakula fulani kutengemea ugonjwa.
ii) enga enga mtoto – kumdekeza mtoto.
kutomuadhibu hata anapostahili kuadhibiwa.
Kumpatia vyovyote atakavyo. 2 x 2 = 4.

h) Mfalme yule alikasirika alipoaibishwa na watumishi wake katika karamu ile.
* Neno lingine lenye maana sawa (visawe) na lile lililotajwa likubaliwe.
Sahihisha ukamilifu wa sentensi – hakuna kupata nusu – (alama 1)
ii) Shemeji alipovua nguo na kukaa, buda yule alisimama (kama hapo (i.) alama

2.i) Kijitoto / kitoto kidogo kilipatikana ndani ya kijumba kile. (Alama 2)
Po – katika sentensi ya kwanza inaonyesha mazoea yaani kila wakati akifanya hivyo (kuchelewa).
Po – katika sentensi ya pili inaonyesha wakati maalum – pindi tendo hilo (kuchelewa) linapotokea. *1 x 1 = 2*
ii) Yusuf halimi shamba lake. *1 x 1 = 1*
iii) “Asante Edith” Miriam alimshukuru. “Na ulirudi lini kutoka nyumbani?” Miriam alimwuliza (Edith)
“Asante” Miriam alimshukuru Edith; Ulirudi lini kutoka nyumbani? Miriam alimwuliza Edith.
“Asante sana Edith; ulirudi lini kutoka nyumbani?” Miriam alimwuliza.
* Tazama jibu hili na upime kama itakubalika vilevile. *2 x 1 = 2*
Jumla 40

SEHEMU YA TATU
USHAIRI.

a) Mtunzi aeleza kuhusu siku yake ya kuondoka ulimwenguni siku ya kufa kwake. Kwamba siku hii ni sharti ije haiwezekani kuepukwa. (alama 3)

b Mtunzi anakutanisha maneno mawili.
Mabayangu – badala ya – Mabaya yangu.
Is'o amefupisha badala ya Isiyo. (2 x 2 = 4)

c) - Ni tarbia – Mishororo minne kila ubeti
umeumbwa kufuata mtindo wa msuko – mshororo wa mwisho umefupishwa.
Aina ya mtiririko, vina vya mwisho ni sawa toka mwanzo hadi mwisho 'ri', kina cha kati vile vile kimetiririshwa 'ka' isipokuwa katika ubeti wa nane / mwisho.
Hoja zozote mbili – 2 x 2 = 4.

d) Katika ubeti wa saba, mwandishi akiri kwamba anaungama na kukubali kuitwa na mungu maana maisha yake yamefikia mwisho hawezi kughairi. Ana enda zake yaani mapumzikoni ya milele.
Katika ubeti wa nane yeye asema kuwa kwa vile yeye ni binadamu, hana la kuchagua, kwa kufanya hivyo, huko aendako atahifadhiwa na kulindwa milele. Anahitimisha kwa kuwaaga wanaobaki.

e) i) Ni muhali kughairi – Haiwezekani kwenda kinyume au kupindua.
ii) Ziara is'o shirika – ni safari au mwendo ambao hakuna wa kukusindikiza au kuandama nawe. Ni safari ya mtu binafsi – pekee.

d) Siku ya kufunga safari ndefu – siku ya kuacha dunia.
Ziara is'o shirika – siku ya mauti hujia mtu pekee kila moja na wakati wake.
1 ½ x 2 = 3 *Jumla 3 + 4 + 4 +4 + 1 + 1 + 3 = 20*

10.a) Kichwa au hasa ubongo ndio unaoamua na kupanga kila kitu mwilini. Ubongo ndio unaoweka mizani na kutolea amri sehemu zingine za mwili. (alama 3)

b) Kilicho muhimu ni ubongo wala sio kichwa hasa. Sababu ni kwamba ubongo ndio ulio na uwezo wa kujua mambo mengi yaliyokamilika sio kiungo kichwa. Inatakikana kile ambacho hakivuji mambo.
(Alama 4)

c) Amefananishwa na: 1) Sanamu 2) tumbili (alama 2 1 x 2 = 2)

d) Kishirikisho na: - shingo.
nywele
moyo *1 x 3 = 3*

e) Tarbia / unne - Mishororo minne kila ubeti. (alama 2)

f) - Vina vya kati (ukwapi) katika mishororo mitatu ya mwanzo (mwanzo, mtoto, mleo) kina ni 'ni' katika kibwagizo kina ni li.
kina cha mwisho (utao) katika mishororo mitatu ya mwanzo (mwanzo, mtoto na mleo) ni 'li' isipokuwa katika kibwagizo kina ni 'ni'
Hivyo shairi katika ubeti huu unafuata mtindo wa ukara

Kielezo __ni, ___li.
___ni, ____li.
___ni, ____li.
___ni, ____li.

Maelezo ya kina cha ukwapi – alama 1 ; Utao – alama 1

g) i) Jalali – jina la Maulana, mwenyezi mungu.
ii) Mwendawazimu – Mtu aliye na matatizo ya akili asiye na akili timamu, anayeweza kuleta madhara. (1 x 2 = 2)
Kutaja maneno haya mawili kisahihi ni alama moja kila moja.
Maelezo sahahi ya maneno haya ni alama moja kila moja.
Jumla 1 + 1 + 1 + 1 = 4.
Jumla swali zima 3 + 4 + 2 + 3 + 2 + 2 + 4 =20

KISWAHILI VI
SEHEMU YA YA KWANZA
INSHA.

1. "Hamjambo wanafunzi . Ninamshukuru mwalimu mkuu kunialika kuja ili niwafahamishe kuhusu ukimwi ……." Endeleza hotuba hii mpaka mwisho .
2. Mti ukifa shinale na tanzuze hukauka .
   Toa hoja zitakazounga mkono usemi , 'Katika jamii za kiafrika mwanamke angali anadunishwa'
3. Eleza shida zinazoikumba nchi hii na upendekeze suluhisho zinazoweza kutolewa.

SEHEMU YA KWANZA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA,
INSHA.

Maudhui

Chanzo

(i) Kufanya mapenzi na mtu aliye na virusi vya H.I.V
(ii) Kwa kutumia vifaa kama sindano , wembe .
(iii) Kuongezwa damu iliyo na virusi vya H.I.V
(iv) Kubusiana .

Kinga

(i) Kuwa na mpenzi mmoja (asiye na virusi vya H.I.V) aliye mwaminifu kwako.
(ii) Kutumia mipira ikiwa ni lazima uwe na wapenzi wengi
(iii) Kutumia sindano , wembe mpya kila wakati .

C <u>Madhara</u>
(i) Umaskini
(ii) Vifo
(iii) Kutengana kwa familia

Hoja zozote 5

2. Mwanafunzi lazima atambue kuwa hii ni methali .
   Msamiati _____ Tanzu _____ matawi

Maelezo ⟶ Mti ukifa sehemu ya chini ni lazima pia ufe sehemu ya juu. Maana ya hapa ni kuwa kiongozi mwema akiondoka ni lazima aliokuwa akiwaongoza wakorogeke kwa mambo maana jamii isiyokuwa na uongozi huangamia .

Matumizi ⟶ Walioondokewa na kiongozi wao kisha wamekorogeka wanaweza kufarijiwa kwa methali hii.
TAZ: Insha ina sehemu mbili ambazo sharti zijitokeze katika insha .

(i) Kufa kwa shina ya mti (kuondokewa na anayetegemewa.
(ii) Tanzuze hukauka (waliomtegemea kuteseka) Eleza mateso

3. (i) Kidini - Hawaruhusiwi kuhubiri katika baadhi ya madhehebu .
(ii) Kielimu – Licha ya kuishi katika karne ya ishirini na moja, watu wengine hasa wazee) bado hawaoni haja ya kumwelimisha mtoto msichana.
(iii) Baadhi ya waajiri hubagua wanawake. Hawapendi kuwaajiri kwa sababu watakuwa wakienda likizoni kila mara kujifungua.
(iv) Kitamaduni - Baadhi ya watu bado hawakubali mwanamke arithi mali, ale baadhi ya vyakula kama mayai, kuku n.k.
(v) Nyumbani- Wanaume wengi huwadhulumu kutokana na imani kuwa mke lazima apigwe .
- Wanafanyishwa kazi ngumu (kulima , kupalilia kuvuna) wakati ambapo waume wao, wanapiga tu soga .

4.

SHIDA	**SULUHISHO**
(i) Ukosefu wa kazi	- Kujenga viwanda - Kupanua kilimo
(ii) Umaskini	- Serikali kuwapa watu mikopo ya - kuanzisha biashara ndogo ndogo .
SHIDA	**SULUHISHO**
(iii) Ukabila / ufisadi	- Sheria kali zitolewe/ hatua kali hukuliwe.
(iv) Watu wengi kuhamia mijini	- Kujenga viwanda mashambani .
(v) Barabara mbovu Ugonjwa wa ukimwi	- Barabara zitiliwe lami - Kuwafunza watu chanzo na madhara.

SEHEMU YA TATU
USHAIRI.

1. Wahenga waliyosema *Yamejiri* kwa hakika
   Yapotea yalo mema *Mawi* yamenawirika
   Wengi tunashika tama Maovu mengi yashika

Si hapa si Amerika Yawaka moto dunia

2. Yawaka moto dunia Si usiku si mchana
Ya Rabi tunaumia Kwa mengi ya kutatana
Wanja la fujo dunia Wataka *kukakawana*
Utunusuru Jalia Yawaka moto dunia

3. Yawaka moto dunia Yapandisha na kushusha
Magogo kuzidi mia Kuyatua na kutwisha
Ulimwengu wazuzua Wachache huwachekesha
Hutisha na kutuchusha. Yawaka moto dunia

4. Yawaka moto dunia Inayo mingi mijiza
Na wengi huwalemea Hupotosha na kujuza
Yataka kuyapimia Sije *kukudidimiza*
Yatesa kupindukia Yawaka moto dunia

5. Yawaka moto dunia Hubwaga zani sikiza
Bila taswira kutia Kujua inavyocheza
Huwa na mbuzi mkia Ukose ya kupendeza
Patupu kuangukia Yawaka moto dunia

6. Yawaka moto dunia Ni dungudungu dunia
Ya *mazigazi* julia Yatinga na kuchachia
Ghururi imejalia Na ya chumvi hutilia
Waza ukiyawazua Yawaka moto dunia

7. Ikikutaka dunia Tapaa wakulilie
Na *itakupalilia* ***Kofia wakuvulie***
Bali ikikuchukia Tatamani ujifie
Wabaki kujililia Yawaka moto dunia

8. Yawaka moto dunia Kuna mengi ya kuchama
Wivu wizi na tamaa Ubaguzi usokoma
Mafuriko nayo njaa Maonevu yasozama
Vita vingi vimejaa. Yawaka moto dunia.

9. Maswali.

a. Hili ni shairi la aina gani kimuundo? Tetea majibu yako. (alama3)
b. Ni wasia gani unaotolewa na mshairi?
c. Onyesha maana ya mstari toshelezi ukitoa mfano mstari wowote wa shairi. (alama 3)
d. Eleza maana ya kipokeo cha shairi hili (alama 3)
e. Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari (alama 3)
f. Kwa nini mwandishi anasema dunia inawaka moto? (alama 3)
g. Andika mbinu 2 za lugha katika shairi hili na mfano mmoja mmoja. (alama 3)
h. Andika maana ya (i) Kukakawana (alama 4)
i. Mazigazi (alama 2)

10. Mkusanyiko wa uma, ni mpango wa jalali,
Jalali mwenye huruma, aloumba kila mwili,
Mwili wa mtu na nyama, akatia na akili,
Akili yenye kupima, la haki na la batili,
Batili haina wema, iwapo japo kalili

Kalili huwa imara, iwapo na kiongozi,
Kiongozi ule busara, asiye na ubanguzi,
Ubaguzi ni hasara, isofaa siku hizi,
Siku hizi za fikara, za watu wanamaizi
Kumaizi yalo bora, yasiyo na pingamizi

Pingamizi kuzing'owa, baina yetu raia.
Raia tukateuwa, Serikali ya jamia
Jamia tukaridhiwa, kuwa haina udhia
Udhia tukiletewa, tusiridhi vumilia
Kuvumilia kwauwa, hasa kumwasi Jalia.

Jalia yake hukumu, ambayo kwetu lazima,
Lazima tumheshimu, kiongozi alomwema,
Mulema kula yake kaumu, iliompa kusimama
Kusimama muadhamu, kuitimiza kalima,
Kalima iliyotimu, nami nafunga nudhuma.

Maswali.

a. Lipe shairi hili kichwa mwafaka *(alama 2)*
b. Eleza muundo wa shairi hili *(alama 4)*
c. Eleza maudhui yanayojitokeza katika ubeti wa tatu *(alama 2)*
d. Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari *(alama 4)*
e. Mwandishi alikuwa na dhamira gani katika kuliandika shairi hili? *(alama 2)*
f. Hili ni shairi la aina gani? *(alama 2)*
g. Huku ukitoa mifano, eleza uhuru wa kishairi alioutumia mwandishi *(alama 4)*

SEHEMU YA PILI
UFAHAMU, MUHTASARI, MATUMIZI YA LUGHA

Kama kawaida yake , Faki alifika hospitali saa kumi na mbili asubuhi . Kawaida hii haikuanza zamani sana kwa hakika : Imeanza karibuni tu , toka kitoto chao chanajike kilipolazwa hospitali kwa tumbo la kuendesha.
Masika mama-mtu ikambidi akikimbie kitanda cha kinyumba kulalia kitanda cha hospitali karibu na mwanawe . Na Faki kwa upande wake ikamlazimu kutamba na jua na mvua kuizumbua riziki angalau ya kupeleka mkono kinywani.- angalau riziki hiyo! Na alipoipata riziki ya mchana kutwa alijifunga kibwebwe kuingia jikoni kuitayarisha ilike , kisha kudapia baiskeli yake au mwanapata kama watu wengine wanavyoita kuelekea hospitali kumpelekea mama mtoto aghalabu muhogo wa kupwaza na chai ya mkandaa; na kile kitoto chao , maziwa na uji
Asubuhi kila siku ilimbidi atoke mapema , kisha ashike njia kuelekea kibaruani .

Naam , kama kawaida yake , leo aliuwacha mparapata wake nje chini ya ngazi pale hospitali, akatoa mkoba wenye uji na maziwa ya mtoto pamoja na muhogo wa kupwaza na chai ya mkandaa ya mama -mtoto ,kwenye lile boksi kubwa analolifunga kibaoni nyuma ya baiskeli yake . Huyo Faki akawa anapanda ngazi taratibu kuelekea wadi ya watoto kumwuona mwele na muuguzi wake

Lakini leo , kabla hajamaliza kuipanda ngazi , alisikia ukwenzi wa mwanamke ambao ulimtuturisha moyo . Asingaliweza kuipotea sauti ya mwanamke huyo ingawaje ilitoka kwa ukwenzi . Bila shaka ilikuwa sauti ya Masika mkewe . Na sasa ukwenzi huo uwe wa nini ? Uwe wa nini enh, isipokuwa …….

Alitimka, akazipanda ngazi kwa vidato vitatu vitatu. Macho yakamtoka na moyo ukamhaha . Joto la ghafla likamjia. Na hofu ikamjaa. Huyo kufumba na kufumbua, alijkuta katika mbele ya Masika mkewe aliyekuwa kashikiliwa vyema na wauguzi ; wengine kulia na wengine kushoto huku akiwawa na kupiga makambi na mayowe .

"Nini ?" Alibwata Faki pale alipokuwa kasimama kama shujaa aliyechomwa sime na kuyasikiliza maumivu. " Mwanangu ……." Alipayukwa Masika, " maskini damu yangu … mume wangu ewe mwenzangu…… nguvu zetu, jasho letu, mtoto …….aaaa mama! Uchungu wa mwana unauma! Tumbo linanikeketa !" Aliendelea kulalama Masika.

Lugha hiyo ilitosha kujibu swala la Faki lililomwenda akilini. Kila kitu kilikuwa wazi. Faki sasa alikwisha maizi nini kimetokea. Hima alipiga goti chini kufikia kimwili kilichozongwa shiti jeupe na kulazwa kigodononi sakafuni. Huku mwili mzima ukitetema, taratibu alinyoosha mikono kukiteka hicho kijimwili kisha aliinuka na kwenda nacho kwa mkewe.

" Mume wangu, haaikuwa riziki yetu ….." aliendelea kulia Masika
"Nyamaza Masika", alitamka Faki kwa upole huku akijaribu kuyazuia machozi yaliyokuwa njiani . " Kila liandikwalo halina budi kuwa, lazima …."
alishindwa kuyamaliza aliyotaka kuendelea kuyasema .

Maswali.

(a) Eleza kwa nini Faki alikuwa akienda hospitali kila siku *(alama 2)*
(b) Taja jina lingine lililotumiwa katika taarifa kurejelea baiskeli *(alama 1)*
c) Kwa nini Faki alilazimika kutafuta kibarua kila asubuhi *(alama 3)*
(d) Eleza sababu iliyomfanya Masika kupigwa ukwenzi *(alama 2)*
(e) Unadhani mwandishi ana maana gani anaposema, "……ilitosha kujibu swala la Faki lililomwenda akilini kila kitu kilikuwa *wazi"* (alama 3)
(f) Fafanua maana ya, " mume wangu haikuwa riziki yetu ……" *(alama 3)*
Taja maneno yoyote mawili kutoka kwa taarifa ambayo yamefanyiwa utohozi kutoka lugha ya kiingereza *(alama 2)*
(h) Eleza maana ya ; *(alama 4)*
Alijifunga kibwebwe
Machozi yaliyokuwa njiani

UFUPISHO.

2. Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Ninashukuru wanafunzi wote wa dasara langu kwa kuhudhuria mkutano huu nilioitisha dakika ya mwisho. Najua walimu washaanza kukata vipindi vyote baada ya kumaliza

mambo yaliyohitajika kufunza toka juzi. Na sasa mmepewa nafasi kubwa ya kujitayarisha vizuri zaidi kwa ajili ya mtihani wenu wa mwisho, lakini mimi nimeona kwamba upo muhimu wa kuzungumza na nyinyi katika dakika hii ya mwisho. Madhumuni si kufunza zaidi, maana hakuna tulichosaza kwa mujibu wa muhtasari wa masomo lakini ninataka kuwapeni maoni yangu ya mwisho kabisa . Hasa nitawaeleza yale ya kuzibia nyufa ndogondogo zilizobaki na pia kuwafunulia kunga za maisha ambayo wengine mtalazimika kuyakabili kwani ingawa sote tunawatakia heri mufaulu mtihani na hatuna shaka mtafaulu, yawezekana kwamba mtapata bahati mbaya katika mtihani na mlazimike kujiunga na maisha moja kwa moja.

Kwa kuwa tumefika ukingoni mwa safari yetu tuliyoianza miaka minne iliyopita, ninataka kuwapigia kengele ya mwisho. Hapa ninazo karatasi zenu za majaribio mliyoyafanya juma lililopita. Nina furaha kusema ya kuwa nyote mmejaribu maswali kama ilivyostahili. Hata hivyo msivimbishe vichwa mkaja mkachafua mambo dakika ya mwisho katika mitihani yenu. Wahenga wamesema, mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Kumbuka hilo jaribio si mtihani wa mwisho, kazi bado ingalipo na inakukodoleeni macho .Pengine si vizuri kwa wakati huu kusoma sana na kukesha, lakini ni wakati wa kuzipiga brashi na kuzisafisha zile sehemu ambazo kila moja wenu anaziona hajazipitia vizuri , au hazijui vizuri au hajaziwekelea uzito. Zidini kujitayarisha vyema, zaidi na zaidi. Mkifanya hivyo, kila kitu kitakuwa wazi kwenu na mtaiona faida ya kazi na uvumilizi wenu.

Ningependa kusema kwamba sasa ninaosha mikono yangu kabisa sina ambacho ni cha lazima sijawafunza. Baadhi ya mengi mjuayo yatatahiniwa lakini mengine hayatatahiniwa kwani kutunga mtihani si kuandika kitabu , bali ni kutunga maswali ya kupima kama unajua mengi uliyofundishwa . Hata hivyo, kwa kuzijua nyanja zote za kiswahili zilizopendekezwa kwenye muhtasari wa masomo, hakuna kitakacho kushindeni.

Naomba myakumbuke maaso yote niliyowapa na jinsi ya kukabiliana na mitihani na hata ulimwengu wenu . Endeleeni na bidii yenu. Na hili la ulimwengu wenu ndilo la muhimu sana. Maana ya kufanikiwa katika mtihani si kufanikiwa na maisha. Maisha yanataka mbinu zake. Mnakokwenda nje ya kuta za darasa kuna ulimwengu, na wazee wamesema, asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Ulimwengu msiuingie kwa hamu na pupa na kutaka kuyavamia yale yote ambayo mlikuwa mkiyakosa mlipokuwa shule. Mkitaka kufikisha kisugudi kabla vidole havijafika, mjuwe huenda mkavunja mikono yenu.
Ulimwengu una mengi ya kuvutia, lakini si kila zuri na la kuvutia ni zuri katika hakika yake. Vyengine vinang'ara, lakini si dhahabu. Na isitoshe si kila mtu miongoni mwenu ana uwezo wa kupata kila anachokitaka. Lazima wengine miongoni mwetu tujikune tujipatiapo. Tusiwaige watu ambao tunajua ukunjufu wao wa matumizi ulivyo. Hakika mwiga tembo kumeza boga, huchanika msamba.

Lazima katika dunia ya leo uishi pamoja na watu - yaani usijitenge, bali shirikiana na wenzako kwani ulimwengu wa siku hizi ni ulimwengu wa mtu kumtegemea mwenzake, hata ikawaje. Mheshimu anayekuheshimu, mfundishe heshima asiyekuheshimu . Wapende wazee wako, majirani zako, na zaidi ipe nchi yako nafsi yako.Ukipata kazi ithamini kazi yako, maana siku hizi kazi si kitu cha kuchezea .Kama hukupata kazi ya kuajiriwa,tumia akili ,busara na maarifa yako kujitegemea .Mengi mmefundishwa katika mfumo wa elimu wa 8 : 4 : 4 ili mjitegemee. Si rahisi tena serikali kumpa kila mtu kazi. Usitahimilivu ni msingi wa maendeleo. Jengo halisimami kwa siku moja, lataka idili ya mchwa.

Hii sasa ndio hatima ya mimi kuwa nanyi kama mwalimu wenu wa kidato hiki na nyinyi ndio mwisho kuwa wanafunzi wangu. Tuna mengi ya kukumbuka. Tusisahau uhusiano wetu. Zaidi na watakia kila la heri katika mitihani yenu na maisha kwa ujumla .

(a) Eleza mambo muhimu katika aya ya pili (maneno 50- 60) *(alama 7)*

(b) Eleza maaso ambayo wanafunzi walipewa katika aya ya nne. (maneno 65-75)
(alama 9)

(c) Mwalimu alitoa maaso gani kwa wanafunzi iwapo hawangebahatika kuajiriwa ?
(maneno 35-40) *(alama 4)*

MATUMIZI YA LUGHA .

A. (a) **Ainisha sentensi hizi** *(alama 4)*

Maji ukiyavulia nguo yaoge
Twende kwetu sasa hivi

(b) **Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi ; kisha eleza ni vielezi vya aina gani.** (alama 4)

(i) Anafanya kazi kwa mwajiri wake .
(ii) Alifanya mambo kisirisiri.

(c) **Toa jibu moja sahihi linalooana na tungo ulizopewa** *(alama 2)*

(i) Mabaki ya jengo lililobomoka au mtu aliyekonda kupita kiasi
(ii) Sehemu ya pwani ambayo meli hufungwa ili kupakia shehena

(d) **Sahihisha sentensi zifuatazo** *(alama 4)*

(i) Uko na pesa yoyote unikopee ili niweze kukidhi mahitaji yangu ?
(ii) Yule msichana anijiringa tu bila kujua kuna kuringa hiyo haitamsaidia sana .

(e) **Taja kinyume cha kila mojawapo ya maneno yafuatayo** *(alama 4)*

(i) Kudai
(ii) Unganisha

(f) **Unda majina mawili kutokana na kila kitenzi ulichopewa** (*alama 4)*

(i) Tatua
(ii) Kunja

(g) **Eleza maana ya semi hizi** *(alama 4)*

(i) Kata kalima
(ii) Kuzua maneno

(h) **Andika upya sentensi hizi bila kutumia neno <u>amba</u>** *(alama 4)*

(i) Ugonjwa ambao ni hatari sana ni ukimwi .
(ii) Nilimwona simba akinyemelea banda la ng'ombe nilipokuwa nikishika zamu

Kanusha sentensi hizi . *(alama 2)*

(i) Nitaenda bungeni alasiri kuhudhuria kikao .
Tumesimama hapa sana .

(k) **Andika maneno haya katika hali ya kufanyiana** *(alama 2)*

(i) Soma
(ii) Iba

(l) **Huyu ni nani?** *(alama 1)*
(i) Mwamu
(ii) Kamilisha methali ifuatayo *(alama 1) .*
(iii) Mkataa wengi _____

SEHEMU YA PILI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
UFAHAMU, MUHTASARI, MATUMIZI YA LUGHA

1. UFAHAMU

a. Alikuwa akienda hospitali kila siku kwa sababu mtoto wake msichana alikuwa amelazwa huko .
(b) Mparapata
(c) Alilazimika kutafuta kibarua ili apate pesa ya kununua chakula chake mwenyewe pamoja na mkewe na mtoto.
(d) Masika alipiga ukwenzi kwa sababu mtoto wake aliyelazwa hospitalini aliaga dunia
(e) Ina maana kuwa Faki alifahamu sababu ya mkewe kulia ilikuwa kifo cha mtoto wao.
(f) Masika alimaanisha kuwa mungu hakuwa amepanga mtoto huyo angeishi .
(g) Wadi
Shiti
(h) (i) Alifanya kazi kwa bidii
ii) Alikuwa karibu kulia .

2. UFUPISHO

(a)

(i) Wanafunzi wasivimbishe vichwa , wakaja wakachafua mambo dakika ya mwisho.
(ii) Jaribio si mtihani wa mwisho , bado kazi ingalipo na inakukodoleeni macho.
(iii) Si vizuri wakati huu kusoma sana na kukesha lakini ni wakati wa ; Kuzipiga brashi na kuzisafisha
sehemu ambazo kila mmoja wenu anaziona hajazipitia vizuri.
(v) Zidini kujitayarisha vyema zaidi wa zaidi .

(b)

(i) Endeleeni na bidii yenu
(ii) Kufanikiwa katika mtihani si kufanikiwa katika maisha.
(iii) Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu .
Msiuingie ulimwenguni kwa hamu na pupa na kutaka kuyavamia yale yote ambayo mlikuwa mkiyakosa mlipokuwa shule.
(v) Ulimwengu una mengi na kuvutia , lakini si kila zuri na la kuvutia, ni zuri kwa hakika yake
(vi) Si kila mtu miongoni mwenu ana uwezo wa kupata anachokitaka.
(vii) Tusiwaige watu ambao tunajua ukunjufu wao wa matumizi ulivyo.

{m------ 7}
{u--------2}

9

c) (i) Tumia akili, busara na maarifa yako kwa kujitegemea.
(ii) Mengi mmefundishwa katika mfumo wa elimu wa 8: 4: 4 ili mjitegemee
(iii) Si rahisi tena serikali kumpa kazi kila mtu.
{m------3}
{u ------1}
4

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a)

(i) Maji	ukiyavulia	nguo	yaoge
Kiima	Kitenzi	Kitendewa	Kitenzi

(ii) Twende	Kwetu		Sasa hivi
Kitenzi	Kivumishi		Kielezi
	Kimilikishi		

(b)(i) Kwa - kielezi cha mahali
(ii) Kisirisiri - kielezi jinsi / namna

c) (i) Gofu
(ii) Gati
(d) (i) Una pesa zozote unikopeshe ili niweze kukidhi mahitaji yangu ?
(ii) Yule msichana anaringa tu bila kujua ya kuwa maringo hayo hayatamsaidia sana
(e) (i) Kudai - Kulipa
(ii) Unganisha - tenganisha
(f) (i) Tatua - utata , tatizo , kutatana , mtatizi *(yoyote mawili)*
(ii) Kunja - Mkunjo , ukunjaji, kukunja , *(yoyote mawili)*
(g) (i) Kata kalima - Acha kusema ghafla
(ii) Kuzua maneno – kusema uwongo .
(h) (i) Ugonjwa ulio hatari sana ni ukimwi .
(ii) Mtumwe aliyepigwa na mawe alikuwa Stefano .
(I) (i) <u>Ka</u> imetumika kuonyesha matendo yanayofuatana kwa kutendeka kwa wakati uliopita
(ii) <u>Ki</u> imetumika kuonyesha kuwa ,kitendo kilikuwa kikiendelea wakati ambapo kingine kilikuwa kikitendeka.

(j) (i) Sitaenda bungeni alasiri kuhudhuria kikao.
(ii) Hatujasimama hapa sana .
(k) (i) Soma - Someana
(ii) Iba - Ibiana
(l) (i) Mwamu - Shemeji wa kiume .
(ii) Mkataa wengi <u>ni mchawi</u>

KISWAHILI KARATASI 9

102/2

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

1.

UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Msemo “Ya kale hayako” unatukuzwa sana na vijana na hata wazee ambao wanathamini usasa. Msemo huu umetishia kuumeza na kuutema utamaduni wa Mwafrika. Utamsikia kijana akiambiwa na mzazi wake, “Jamani itabidi ujifunze lugha yako ya mama, hivi hatuwezi kuwasiliana na mababu zako kijijini”. Naye kijana huyu hujibu, huku macho kayatunga kwenye runinga, kidhibiti mbali mkononi. “Hayo ni yako. Lugha inahitajika kutumiwa pale mtu anapoishi. Mimi kijijini humo nitaishi lini? Na huyu babu, si anajua Kiingereza?”

Huyu ni mfano mmoja tu unaoonyesha mabadiliko ambayo yamezikumba jamii zetu. Watoto na hata watu wa umri wa makamo wamerithi desturi mchafukoge ambazo hazijulikani kama ni za Kiafrika au Kizungu. Mitindo ya mavazi ya kushangaza imezuka. Kuna wale wanaopendelea kutembea mabega wazi. Hawa huvaa vizibau vilivyoning’inizwa kwenye fito za nyuzi. Kuna baadhi ambao huvaa suruali ndefu ambazo zimening’inia kiasi cha kuvifanya viuno kuwa kwenye miundi. Huu nao ni usasa ati. Unapouliza unazomewa na kuambiwa umechelewa kutambua hii ni karne ya ishirini na ngapi.

Tofauti za umri zimeanza kuwa finyu mno siku hizi. Si bura kumpata kijana akimpita mzee kama kwamba hajamwona. Anangoja mzee amsalimu yeye. Vijana wengine hudiriki kujibizana na wazee wao kama kwamba ni wa rika moja. Hawawapi wazee fursa ya kuzungumza, badala yake huwakata kauli kila

mara wanapozungumza na kuwaudhi. Anapoulizwa kwa nini anamjibu vibaya mzee huyo, anasema nyakati za 'kuhubiriwa' bila kuuliza maswali zimepita na kuzikwa.

Teknolojia mpya imewapunguzia udhia baadhi ya vijana ambao hawapendi kufanya kazi. Katika baadhi ya familia, utapata kwamba kuna mashine za kufulia nguo na kupangusia sakafu. Vijana wengi wanaoinuka hawawezi hata kujifulia nguo. Wale ambao kwao hakuna mashine, wana vijakazi ambao huwafanyia kila kitu. Lao ni kulala tu na kusoma. Mafunzo ya kazi ambayo vijana walipata siku za mababu yameanza kuzikwa kwenye kaburi la sahau. Hata katika familia ambazo utapata wazazi wana ari ya kuwafunza wanao umuhimu wa kutenda kazi za nyumbani, utapata kwamba watoto wenyewe hawazipendi kazi hizi. Wanahiari kucheza michezo ya kompyuta na kutazama kupigana mierekani na masumbwi katika runinga. Si ajabu kwamba wengi wa vijana wanakua wakidhani njia ya kutatua migogoro ni kupitia kwa makonde migoto vichwani.

Suala unasaba lilikuwa na umuhimu mkubwa katika siku za kisogoni. Neno ndugu lilikuwa na maana pana katika jamii ya Mwafrika. Watoto wa ami, mjomba na shangazi walihifadhiana na kulindana kama ndugu. Siku hizi neno ndugu limejikita tu katika uhusiano wa karibu tu; mtoto wa mama au baba yako. Vijana wengi hawajui hata mabinamu zao. Jambo hii limewafanya wengine kuoa watu wa ukoo wao bila kujua. Baadhi ya vijana wamezaliwa na kukulia mijini, hawana wakati wa kutangamana na jamaa zao vijijini. Kwa hivyo, hata inapofika wakati wa kuoa, hao hukutana na wachumba wao mijini.

Ingawa tunapasa kutambua kuwa wakati umebadilika, ni vyema kuwajibika. Hata pale tunapoiga mitindo ya kisasa kama vile ya mavazi, tuige kwa tahadhari. Mavazi tunayovaa yasikinzane na maadili ya jamii zetu. Elimu ya kisasa isiwe kisingizio cha kusahau kitovu chetu. Tukumbuke methali isemayo "Usiache mbachao kwa mswala upitao".

(a) Mwandishi amedhamiria kichwa mwafaka cha taarifa hii kuwa ya kale hayako. Eleza. (alama 2)

(b) Tofauti za umri zimeanza kuwa finyu mno siku hizi. Fafanua kauli hii. (alama 2)

(c) Mabadiliko yaliyokithiri katika jamii ni kutokana na vijana wasiowajibika. Toa ithibati. (alama 5)

(d) Eleza chanzo cha mabadiliko ya vijana kulingana na taarifa. (alama 4)

(e) Eleza matumizi ya methali usiache mbachao kwa mswala upitao kulingana na taarifa. (alama 2)

2. **MUKHTASARI**

Soma taarifa ufuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au mchoro unaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, video, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, wavuti, DVD, n.k.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea ulimwenguni kote mithili ya moto katika mbuga wakati wa kiangazi. Uenezi umechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Matumizi ya tarakilishi, mdahilishi na viungambali vya picha yamesambaza ponografia ilivyoanza. Hata hivyo, hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbali mbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la ama kuvuruga maadili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Hivi sasa, kundi kubwa ni lile la wanotumia matusi haya kama njia ya kuchuma. Kwa mfano, wanamziki ambao hutumia ponografia kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji ponografia kuna athari kubwa kwa jamii na hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kuwa kinachoonekana na jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama masomo watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera. Hivyo basi huanza kuiga wanayoyaona na kusikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Kutokana na uchafu huu, watu wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni mengi. Haya ni pamoja na ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa. Wengine nao huambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo huwaletea mauti.

Inasemekana kuwa akili za binadamu hunata zaidi mambo yanayowasilishwa kwa picha. Si ajabu vijana huyadumisha matusi haya katika kumbukumbu zao na kuyasanya sehemu ya maisha yao. Wengi huanza kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagaji. Kuna wale ambao huanza kujichua. Kujichua ni hali ya mwanamke au mwanaume kumaliza haja za kimaumbile bila kufanya mapenzi na mtu mwingine. Ponografia imechangia pakubwa kuenea kwa haya.
Jambo hili limegeuza mielekeo ya vijana. Wanaiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Halikadhalika, huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono. Yote haya yanapingana na desturi za Mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kila kukuchapo.

Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama unywaji wa pombe, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochea uchu wa ngono. Mambo haya huwapa vijana tabia za unyama.

Jambo hatari ni kuwa kuendelea kutazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, yaani huondoa makali. Hata katika utu uzima, mtu atapoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na maenezi haya yasio na kizuizi.

Jambo la kwanza ni kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi. Kwa namna hii itawezekana kupunguza mahitaji na uuzaji wa pnografia. Aidha ni vizuri watu wazima wawajibike ile wawalinde hasa vijana kutokana na athari hizi. Inapasa wenye midahilishi, video na sinema wasiwaruhusu vijana kutazama uchafu huu.

Tatizo la kuenea kwa ponografia limeendelea kuwepo kwa sababu ya udhaifu wa sheria. Kilichoko basi ni kuweka sheria za kuzuia utengenezaji na usambazaji wa upujufu huu. Kuambatana na haya, hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria hizi. Hali kadhalika, ushirikiano wa karibu baina ya wadau uimarishwe katika ulimwengu mzima. Serikali na wanaohusika wakabiliwe ipasavyo. Jamii ingependa kuona michakato ya kuharamisha utengenezaji, usambazaji na utangazaji wa ponografia ikiwekwa.

Wazazi nao wasijipweteke tu bali nao wasaidie. Ni muhimu washikilie kwa shati juhudi zao za kuwaelekeza na kuwashauri watoto kuzingatia uongofu na kukwepa picha hizi najisi. Watoto lazima waeleweshwe kuwa haifai kutazama picha au michoro michafu. Itikadi na imani za kidini na utamaduni wa Kiafrika unakataza vikali mtu kuona uchi wa mtu mwingine. Matokeo ya kuasi makatazo haya yana madhara makubwa kwa watu na jamii.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, fanya muhtasari wa aya ya pili naya tatu. (maneno 20 – 25) (alama 6, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya nne hadi ya tisa. (Maneno 55-60) (aama 9, 1 ya utiririrko)

Matayarisho

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Andika kwa maneno. (alama 2)

(i) 11,001

(ii) 10,001

b) Eleza sifa zinazofananisha na kutofautisha sauti zifuatazo. b na d. (alama 3)

c) Eleza matumizi ya viambishi VITATU vya ngeli ya MAHALI huku ukivitungia sentensi mwafaka. (alama 3)

(d) **Tunga sentensi ukitumia neno 'kuja' kama:** (alama 2)

(i) Nomino

(ii) Kitenzi

(e) **Tunga sentensi ukitumia vielezi vinavyotokana na maneno uliyopewa.** (alama 3)

(i) Soko

(ii) Zidisha

(iii) Mtoto

(f) **Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.** (alama 3)

Wazazi wanalipia watoto karo kwa hundi.

(g) **Tunga sentensi sahili yenye viungo vya sarufi vifuatavyo.** (alama 3)

(i) Shina la kitenzi cha silabi moja

(ii) Kauli ya kufanyia

(iii) Kikanushi

(iv) wakati uliopita

(v) Mtendewa nafsi ya tatu umoja

(vi) Kiima nafsi ya pili wingi.

h) Neno 'tikiti' hupatikana katika NGELI mbili tofauti. Taja NGELI hizo huku ukitunga sentensi mbili kubainisha matumizi tofauti. (alama 3)

(i) **Tunga sentensi sahihi ukitumia viunganishi vyenye dhana ya:**

(i) Kinyume (alama 2)

(ii) Kutowezekana kuwili.

(j) **Andika kwa wakati ujao** (alama 2)

Ungalifanya kazi kwa bidii usingaliishi maisha ya dhiki.

(k) **Tumia neno 'mpaka' kama kihusishi cha:** (alama 3)

(i) Kiwango

(ii) wakati

(iii) Mahali

(l) **Kamilisha sentensi kwa kutumia vivumishi kama ulivyoagizwa.** (alama 3)

(i) Rehema ni bibi ……. bezo . (umilikaji)

(ii) Naomba kinywaji …… (ziada)

(iii) Muonye bawabu …….. kwa kutofika mapema. (kusisitiza- mbali kidogo)

(m) **Tofautisha kimaana** (alama 2)

(i) Aliuawa mnyama.

(ii) Mnyama aliuliwa

n) Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi tofautiya ‘po’. (alama 2)

o) Andika kwa msemo halisi. (alama 2)

Askari alisema angemuona siku hiyo jioni dukanimwe.

p) Tunga sentensi ukitumia ulivyopewa katika kauli ya kutendewa. (alama 2)

(i) Pa

(ii) La

4. **ISIMU JAMII**

(a) Tofautisha kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. (alama 2)

(b) Taja mambo mawili yanayoonyesha udhaifu katika mazungumzo na huchangia katika uhamishaji wa msimbo. (alama 2)

c) Taja kaida mbili zinazotawala matumizi ya maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka. (alama 2)

d) Fananisha sifa zozote nne za sajili za maabadini na mahakamani. (alama 4)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA 9
KISWAHILI 102/2

1. UFAHAMU

a) - La

- Mwandishi analalamika kuhusu vile mambo ya kale yanayofaa yamepuuzwa na kutukuza usasa usio na madili. (2 x1=2)

b) Heshima kati ya vijana kwa wazee imeondolewa. (1x 2 = 2)

- Vijana kutukuza lugha ya kiingereza kuliko lugha yao asili.

Vijana kupapia mavazi ya kisasa ya kushangaza.

Vijana kukosa heshima kwa wazee.

Vijana kutopenda kufanya kazi.

Vijana kupuuza unasaba au undugu. (5 x 1 = 5)

- Urithi wa desturi mchafukoge

– Teknolojia mpya

Kuweko vijakazi nyumbani.

Athari za miji. (4 x 1 = 4)

e) Taarifa inahimiza watu wasiache tamaduni na desturi zao za kiafrika ambazo zimewasaidia sana kwa muda mrefu na kukimbilia mambo mageni ambayo hayana faida katika jamii ila madhara mengi. (1 x 2 = 2)

JINSI YA KUTUZA.

Ondoa nusu (½) alama kwa kila kosa la hijai hadi makosa sita (6) yaani alama tatu (3)

Usiondoe zaidi ya nusu ya alama ulizotuza kwa makosa ya sarufi.

MUHTASARI

- Ponografia imekuwepo tangu jadi.

Tatizo sugu ulimwenguni sasa.

Imeenezwa na vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Chanzo hakijulikani.

Huundwa na makundi mbalimbali ya watu wenye nia tofauti. (Hoja 5 x 1 =5)

- Ponografia huharibu akili.

Hufanya vijana kuingilia shughuli za ngono mapema.

Huchangia ukahaba.

Utendaji mbaya shuleni.

Mahudhurio mabaya darasani.

Mimba zisizotarajiwa.

Kuacha shule.

Magonjwa ya zinaa.

Mauti

Kuandama ushoga, ubasha na usagaji.

Kujichua

Kuiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono.

Ubakaji

Kushiriki ulevi/ pombe, dawa za kulevya, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochea uchu wa ngono.

Hufanya nishai na hisi za watu kuwa butu/ huondoa makali.

Hupoteza mhemko wa kawaida.

Hufanya mtu kuwa mtegemezi wa ponografia. (Hoja zo zote 16 x ½ = 8)

JINSI YA KUTUZA

Ondoa nusu (½) alama kwa kwa kilakosa la hijai hadi makosa sita (6) yaani alama tatu (3).

Ondoa nusu (½) alama kwa kila kosa la hijai hadi makosa sita (6) yaani alama tatu (3).

Ondoa alama (1) kwa maneno ya kwanza kumi (10) ya ziada halafu nusu (½) alama kwa kila maneno matano (5) yanayofutia.

3. MATUMIZI YA LUGHA

a i) Kumi na moja elfu na moja/ Elfu kumi na moja na moja.

ii) Kumi elfu na moja/ Elfu kumi na moja. (2x1= 2)

b) - Ni vipasuo/ sauti za kuzuiwa. (1 x 1 = 2)

- b hutamkiwa kwa midomo.

- d hutamkiwa kwa ufizi. (2 x 1 = 2)

c) PO/PA – huonyesha pahali panapodhihirika/ dhahiri/ maalum.

KO/KU – hupoyesha mahali kusikodhihirika / si dhahiri/ si maalum.

MO/MU – huonyesha mahali ndani. (3 x ½ = 1 ½)

Mifano- Pahali hapa panapendeza.

Mahali huku kunapendeza.

Mahali humu mnapendeza. (3 x ½ = 1 ½)

d) i) Kuja kwake kulitufurahisha sana.

ii) Alikuja jana usiku. (2 x 1 = 2)

e) i) Mama ameenda kununua matunda sokoni.

ii) Wanafunzi walitembea zaidi.

iii) Mzee yule anaongea kitoto. (3 x 1 = 3)

f) Shamirisho kitondo - watoto

Shamirisho kipozi – karo

Shamirisho ala – kwa hundi. (3 x 1 = 3)

g) Sentensi yoyote yenye viungo vilivyotajwa kwa mfano: Hamkumfia. ((6 x ½ =3)

h) - LI - YA

- I – ZI (2 X ½ =1)

- Tikiti hili limeiva sana.

- Tikiti yangu ya kusafiria imeraruka. (Setensi zo zote sahihi (2 x1 = 2)

i) i) Lakini, ila, ingawa, ijapokuwa, isipokuwa, n.k.

kwa mfano: Hassan ni mrefu lakini Juma ni mfupi

Wala. Kwa mfano:

Mwanafunzi hakupewa kitabu wala kalamu. (2 x 1 = 2)

p) i) Mtoto alipewa chakula cha kutosha hadi akashiba.

ii) Chakula chote kililiwa na mtoto. (2 x 1 = 2)

JINSI YA KUTUZA.

Ondoa nusu (½) alama kwa kila kosa hijai hadi makosa sita (6) yaani alama tatu (3).

Usiondoe zaidi ya nusu ya alama ulizotuza kwa makosa ya sarufi.

j) Utakapofanya kazi kwa bidii hautaishi maisha ya dhiki. (2 x 1 = 2)

K) i) Nitasoma mpaka chuo kikuu.
ii) Nitasoma mpaka saa tano.
iii) Mwalimu alitembea mpaka kwake. (3 x 1 = 3)

L) i) Mwenye
ii) kinginecho
iii) yuyo huyo. (3 x 1 = 3)

M)i) Mnyama alitolewa uhai kwa sababu yake.
ii) Mnyama alitolewa uhai. (2 x 1 = 2)

N) - po ya wakati
- po ya mahali
- kwa mfano: Bibi aliponitembelea alinipata palipo na kichuguu.

O) Askari alisema, " Nitakuona leo jioni dukanimwo."
" Nitakuona leo jioni dukanimwo." Askari alisema.

Vitahiniwa 7 alama 2
Vitahini 4-6 alama 1
Vitahini 2-3 alama ½

4. ISIMU JAMII

a) - Kuhamisha msimbo ni kutumia lugha Fulani katika mazungumzo kisha ukaanza kutumia lugha nyingine tofauti na ile ya kwanza.
- Kuchanganya msimbo ni matumizi ya maneno au msamiati wa lugha zaidi ya moja katika mazungumzo. (2 x 1 = 2)

b) - Ukosefu wa msamiati unaofaa katika lugha hiyo.
- Wazungumzaji kutojua lugha hiyo husika vizuri. (2 x 1 = 2)

c) - Wakati. Kwa mfano kuna maamkizi ya asubuhi kama vile subalkheri, naya jioni kama vile masalkheri.

- Umri. Kwa mfano mtu mdogo kwa umri humuamkua mkubwa wake, shikamoo, naye hujibu, marahaba.

- Mazingira. Kwa mfano katika mazingira ya shida kama kifo, maneno kama makiwa hutumiwa.

Hoja zo zote 2 x 1= 2

Hoja bila mifano 2 x ½ = 1

d) - Mtu mmoja hutawala mazungumzo kama vile hakimu, wakili, shehe, kasisi, n.k.

- Mazungumzo hurejelea kanuni zilizoandikwa kama vile sheria za nchi, Koran au Biblia.

- Lugha sanifu hutumiwa ili ieleweke vizuri.

- Lugha ya heshima hutumiwa kama vile ndio mheshimiwa, ndugu na dada, n.k.

- Mazungumzo hutolewa mahali maalum kam vile mahakamani, msikitini au kanisani.

- Mazungumzo huweza kueleweka tu na wahusika wenyewe. (Hoja zo zote 4 x 1 =4)

JINSI YA KUTUZA.

Ondoa nusu (½) alama kwa kila kosa la hijai hadi makosa sita (6) yaani alama tatu (3)

Usiondoe zaidi ya nusu ya alama ulizotuza kwa makosa ya sarufi.

MAKOSA YA SARUFI.

Kuakifisha vibaya matumizi mabaya ya vikomo, vituo n.k

Kutumia herufi ndogo na kubwa mahali si pake.

Matumizi mabaya y ngeli na viambashi, nyakati, vihusiano, muundo mbaya wa sentensi na mnyambuliko mbaya wa vitenzi na majina.

Kuacha au kuongeza neno katika sentensi.

Matumizi mabaya ya herufi kubwa.

Mwanzoni mwa sentensi

Majina ya pekee

Majina ya mahali, miji, nchi.

Siku za juma na miezi.

Mashirika, masomo, vitabu, n.k

Makabila, lugha, n.k

Majina ya Mungu.

Majina ya kutambulisha kama majina ya mbwa kama Tom, Jim n.k

MAKOSA YA HIJAI/ TAHAJIA

Kutenganisha neno kama vile asiye kuwa.

Kuunganisha maneno kama vile kwasababu.

Kukata silabi vibaya kama vile karib-u.

Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama “mahari” badala ya “mahali”

Kuacha heerufi katika neno kama vile ‘aliekuja’ badal ya ‘aliyekuja’

Kuongeza herufi isiyofaa katika neno kama vile ‘piya’ badala ya ‘pia’

Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika herufi kama vile i, j.

Kutoandika kistari cha kuunganisha neno au kukiandika mahali si pake.

Kuacha ritifaa au kuiweka pasipofaa kama ‘Ngombe’ N’gombe badala ya ‘ Ng’ombe’

Kuandika maneneo kwa kifupi – k.m, n.k, k.v, mf.

102/2
(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu Jamii)

UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Siku moja , mtu ambaye alijulikana kwa jina la Moto , alikuwa Ameketi chini ya kivuli cha mbuyu. Alikuwa akifanya hivyo kwa kungojea kulungu kunaswa na mtego wake. Hapo mbuyuni, ndipo palikuwa na njia ya kulungu ya kwenda mtoni kunywa maji. Kupitia mbuyuni, iliwabidi kwanza wapitie pale mtegoni. Lakini kwa kuwa kwa siku hii ya leo wakati wao wa kunywa maji ulikuwa bado kuwadia, naye Moto, badala ya kurudi ili aje baadaye, akaonelea heri angojee hapo.

Haikuwa mara yake ya kwanza kutega kulungu. Alikuwa amewanasa wengi na kwa muda mrefu sana. Na ingawaje alifurahia nyama yao laini, ni kuwachuna ndiko alikokuzira. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya vifaa butu vya mawe ya kuchonga alivyokuwa akitumia. Kwa sababu hii basi, haikuwa rahisi kuwachuna. Pia, alikuwa akiwala wabichi. Ili kujipa kazi akisubiri, akaonelea amtengenezee utunda mpenzi mkewe. Hakuwa na shida kuamua utunda huo ungekuwa wa namna gani. Nyakati hizo, shanga zilikuwa bado hazijavumbuliwa. Ni jiwe na mti tu ndivyo vilivyokuwapo, navyo ndivyo vilivyokuwa mali ghafi.

Kwa ala yake, jiwe la kuchonga, Moto akakata vijiti viwili. Kikubwa akakiita 'mama' na kidogo, 'baba'. Dhamira yake ilikuwa kumtengenezea mkewe ushanga na tembe zikiwa za mti. Akiweka kijiti mama chini, alitumia kijiti baba kupekejea tundu. Alifanya hivi kwa nguvu zake zote, Haja ilikuwa ni atoboe matundu mengi, halafu ayakate na kuyaviringisha na baadaye ayaunge na uzi wa muaa ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha, na jasho kumtoka, na huku mawazo yake yote yakiwa juu ya uso wa mkewe, hakuwa ameona cheche zikianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake. Alichokisikia kwa ghafla, kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika. Alishtuka na akaruka kwa woga. Hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani!

Huku akitetemeka kwa hofu, cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Sasa ikawa imepata nguvu na kuwa tsanzala ambayo ilienea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kuangalia hivi, akajiona amesimama peupe! Kutoka kwa upande wa mtegoni, kukaja harufu nzuri ya kunukia. Alifuata na alipofika, akaona kulungu ambaye alikuwa ameshikwa na mtego, ameokwa vizuri sana na nguvu hizo ngeni. Hakujua zinaitwaje wala hakujua aziiteje. Kwa hivyo, hakuwa ameshawahi kuona ama kuonja kitu cha kuchoma sembuse cha kupikwa!

Ni harufu ya kuiva ya kulungu na kudondoka kwa mafuta ya kunona ndivyo vilimtia ujasiri. Naye kwa hatua za woga, akanyatanyata akanyakua kinofu na kukionja. Si utamu huo aliousikia! Sasa akanyafua jinofu. Halafu akaingilia maini, moyo na mafigo. Kulungu akamshinda ingawaje alimla maradufu ya kawaida yake. Aliyebaki, akamfunga ndani ya majani ya mgomba na kuwapelekea watu wake. Pamoja na kulungu, akawa amechukua pia kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili ambavyo baadaye kijiti mama alikuja kukiita "wimbombo" na kijiti baba, " ulindi"...

Ilikuwa alfajiri asubuhi watu waliposhitukia "tatata" za kualika kwa kuni na kulipuka kwa moshi kutoka nyumbani kwa Moto. Nyumba yenyewe ilionekana ikiwa na nuru nyekundu ya ajabu na ya kutisha. Walinyatanyata kuelekea kwenye kioja hicho. Kiliwavutia zaidi kwani walivyozidi kulisongelea, ndivyo ile baridi ya asubuhi ilivyozidi kuwatoka. Mvuto huo ukawapumbaza. Lakini walipumbazika zaidi walipoona - nyuma ya kioja hicho na kupita pazia la moshi, Moto ameketi.

Macho yake yalionekana mekundu mno. Hii ilikuwa sababu ya moshi; lakini hawakuwa wakijua hivyo. Kiwiliwili chake kilionekana kikiyumbayumba nyuma ya miale. Haya yote yakamfanya kutisha. Wenzake wasijue la kufanya kwa sababu ya bambuazi, wakawa wamesimama tuli wameduwaa. Hapo

ndipo waliposikia sauti ikinena: "Mimi ndimo Moootoo...; naivisha na kuunguza, natokeza na naoteka. Anitakaye nitakuja kwake nimpe huu uwezo wangu..."

Ili kuwaogofya zaidi, akaupulizia nao ukaalika kwa moshi na cheche nyingi zilizowafanya wenzake kurudi nyuma kwa hofu. Kuona hivi, akaendelea kuwatia woga kwa kusema, "Hizi ndizo nguvu za Moootoo... mimi ndimi Moootoo...nijieni niwageuzie maisha yenu..."

Akiwa bado ana sehemu ya nyama ya kulungu, akawagawia na kuwaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo aliwaambia siri ya kioja. Hakuwaambia ule ukweli wa mambo, badala yake, aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao, kwa kukosa jina la kufaa, wakaliita "Moto".

Punde si punde, watu wakawa wamezoea moto na wengi wakawa wanakuja kwake tu. Hakutaka uenee vivi hivi tu. Kwa hivyo, akaweka masharti: moto ulipatikana kwake tu kila jioni, na uzimwe mara moja baada ya matumizi. Ni hapo kwake tu ambapo "moto mpya" ungeweza kupatikana. Moto hauibiki wala haufichiki, akawakanya. Na ambaye angefanya ujasiri wa kuuiba ama kuuficha, basi asije kulia kwake baadaye, akawaeleza.

Masharti haya yalifuatwa, naye akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa - na punde si punde, za utukufu pia! Sasa watu wakawa, bila moto, hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi. Hapa ndipo aliwageukia na kuwaambia:

“Ili kuulinda huu Moto Mtakatifu usife, imenibidi kuacha kazi zangu. Lakini siko radhi kuendelea kufa njaa na familia yangu."

" Tutakugawia chakula chetu ili uzidi kuuchunga huo Moto Mtakatifu ili usife," wakamkatiza.

Basi, kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Siku si nyingi, mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto", ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha na kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "Utukufu wa Moto".

Maswali

Ipe makala uliyoisoma anwani mwafaka (alama 1)

Moto alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu kwa sababu gani? (alama 2)

Ala za pekee za wakati huo zilikuwa zipi**?** (alama 2)

Uvumbuzi wa Moto ulikuwa na athari zipi katika maisha ya jamii? (alama 2)

Kwa kutotaka Moto uenee hivi hivi tu, Bwana Moto aliuwekea masharti. Taja mawili (alama 2)

Moto na Aila yake walifaidikaje baada ya ufumbuzi huu? (alama 2)

Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 4)

Kioja

Alikokuzira

meza kichaka

wimbombo

UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha uiibu maswali yanavofuata.

UGONJWA wa utando wa ubongo ambao kwa kiingereza unafahamika kama *meningitis* huzua hofu miongoni mwa watu wengi. Ugonjwa huo pia hujulikana kama homa ya uti wa mgongo.

Hofu kama hizo zinaeleweka kwa sababu utando wa ubongo ni ugonjwa unaoathiri ngozi inayofunika ubongo na uti wa mgongo na kwa hivyo ni rahisi mno kusababisha kifo ikiwa mgonjwa hatahudumiwa haraka iwezekanavyo.

Utando wa ubongo ni ugonjwa unaosababishwa na virusi na bakteria, Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, utando wa ubongo unaosababishwa na virusi sio hatari sana kwa uhai wa mtu ikilinganishwa na bakteria. Japo watu wengi wanaougua utando wa ubongo hutibiwa na kupona, baadhi yao huachwa wakiwa bubu au vipofu na wengine kufariki.

Shida kubwa ya ugonjwa huu ni kwamba unatokea bila kutarajiwa. Kwa mfano mtoto au mtu wa umri mkubwa anaweza kuwa mzima kwa muda wa dakika kadha ila baadaye kuwa mgonjwa mahututi baada ya kukumbwa na ugonjwa huo. Shida nyingine ya ugonjwa huu ni kwamba huwa vigumu kutenganisha dalili za ugonjwa huu na dalili za magonjwa mengine ya kawaida kama vile maumivu ya kichwa. Kwa hivyo kuna baadhi ya watu wanaomeza dawa za kupunguza maumivu ya kichwa bila kujua wanaugua utando wa ubongo.

Dalili za watoto wanaougua utando wa ubongo ni homa, kutapika, mtoto kukataa kula na kulia kwa uchungu. Mtoto anayeugua ugonjwa huu kadhalika huwa anaonyesha dalili za kufura kichwa, kupumua kwa haraka na kutupatupa miguu huku mwili wake ukiwa umejikunyata. Watu walio na umri mkubwa nao huonyesha dalili za maumivu makali ya kichwa, kuwa na shingo nzito (stiff neck) na mgonjwa kuepukana na mwangaza. Kadhalika mgonjwa hushikwa na homa na pia kutapika kando na kukosa ufahamu.

Utafiti umeonyesha kwamba watu walio na umri mkubwa kadhalika huonyesha dalili za kuwa na mikono au miguu baridi, maumivu ya misuli na tumbo hasa kutokana na damu kuwa na sumu. Ni muhimu kufahamu kwamba sio kila mtu anahisi dalili hizi, ikiwa yeyote atashuhudia baadhi ya dalili hizi itakuwa bora kufika hospitalini haraka kupata usaidizi wa daktari kabla ya ugonjwa huo kuzidi sana.

Yeyote anayeshuku kwamba anaugua utando wa ubongo anapaswa kupelekwa hospitalini mara moja. Hii ni kwa sababu ni rahisi mno kwa madaktari kutibu mgonjwa anayepelekwa hospitalini punde tu anapoonyesha dalili ikilinganishwa na yule anayepelekwa huko kama amechelewa.

Maswali

Bila kubadilisha maana <u>fupisha</u> aya nne za mwanzo (Maneno 70-80)

(alama 7, 1 ya utiririko)

<u>Matayarisho</u>

Nakala safi

b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, eleza dalili za ugonjwa wa utando wa ubongo na huduma kwa mhasiriwa (Maneno 55-65) (alama 6, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

.MATUMIZI YA LUGHA

(a) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli zipi**?**

i) neno ……

ii) mate ……. (alama 2)

(b) Eleza matumizi mbalimbali ya 'ni' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Nendeni mkamwite Kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani

(c) Taja ala zinazotumika katika kutamka sauti zifuatazo

i)/dh/ ……

ii)/gh/ …….. (alama 2)

(d) Ainisha matumizi ya –ema katika sentensi ifuatayo (alama 3)

Mwanafunzi mwema ametunzwa vyema kwa wema wake

(e)Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)

"Atamkuta papa hapa akija kesho".Alisema.

(f) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi na kiambishi ngeli (alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(g) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa.

i) Tano ondoa tatu matokeo ni mbili (anza: Mbili……) (alama 1)

ii) Mwalimu huyu anafunza Kiswahili

(Maliza kwa kiashiria kisisitizi) (alama 1)

iii)Ng'ombe aliyekuwa nyuma ya ua alichechemea kwa vile aliumia ukwato wake.(andika kwa wingi) (alama 2)

(h) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno lifuatalo (alama 2)

Ndwele

(i) Ainisha sentensi hii (alama 3)

Aliyenichokoza

(j) Geuza sentensi hizi ziwe katika kauli ya kutendewa (alama 4)

i) Muktubi amempa mwanafunzi jarida.

ii) Bate alivua samaki wengi.

(k) Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo (alama 4)

i) Uhusiano wa zaidi ya hayo

ii) Kuonyesha chanzo

(l) Changanua sentensi ifuatayo kwa vistari/vishale (alama 4)

Kandanda ni mchezo maarufu duniani

(m)Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Wanafunzi ambao waliokuwa wakarimu walimpenda Bi Keti

(n) Yakinisha sentensi hizi (alama 2)

i) Asingeenda safari asingepata ajali

ii)Usije

o) Andika kwa wastani (alama 2)

Magoma hayo yatachezewa mawanjani

4 ISIMU JAMII

“Bwana mdogo,” alisema kwa sauti ya kite.
‘Naam Doctor,’ Nikajibu.
‘Leo wasikiaje?’
‘Nafeel poa’
‘Unafanya kazi gani?’
‘Nasukuma rukwama’

‘Eeh! Bwana, kama watakwa kuishi,acha hiyo kazi ya suruba, unasikia?’
‘Ndiyo Doctor”(kisha akanipimapima kwa kifaa alichokuwa nacho…..)
‘Leo!’ Aliniambia huku akisimama wima na kuchezeshachezesha kifaa chake mkononi,
“N’takuruhusu kwenda nyumbani.Wapaswa kupumzika kwa mwezi mzima pasi kufanya lolote zito.”
‘N`takupa vidonge vya kumeza.’
‘Asante Doctor ,’ Nikamshukuru.

Maswali

a) Mazungumzo haya yako katika rigista gani? (alama 1)

b) Taja lugha zilizotumika katika mazungumzo haya (alama 2)

c) Fafanua sifa za sajili hii (alama 3)

d) Eleza dhima za lugha ya Taifa (alama 2)

e)Taja na ueleze matatizo mawili yanayoikumba lugha ya Kiswahili. (alama 2)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KARATASI YA 10
KISWAHILI 102/2

1. UFAHAMU

(a).Moto / uvumbuzi wa moto (alama 1)

(*Yasizidi maneno manne ikiwa methali*)

(b).-Akingojea kulungu kunaswa na mtego wake

- Ilikuwa mapema hakuona haja ya kwenda nyumbani na kurudi (alama 2)

(c) .mawe / jiwe vijiti / kijiti (alama 2)

(d).Athari za moto

Faida	Hasara
-kuunguza	-kuteketeza (kuweza vyote)
-kuoteka	- uharibifu mkubwa usipodhibitiwa
-kuchoma	- kujenga utabaka
- mwangaza nk	(zozote 2x1)

(e).Mashariti ya kuenea kwa moto:

-moto ulipatikana kwake tu

-uzimwe mara tu baada ya kutumiwa

-usiibiwe wala kufichwa (zozote 2x1=2)

(f).Faida zote za moto

-chakula cha bure

-utajiri au ubwanyenye (kufaidi bila kufanya kazi)

-kupata utukufu (zozote2x1=2)

(g).

i) Kioja – ajabu / shairi

ii) Wimbombo – kijiti mama kilichopekechwa na kuwaka moto

iii) Alikokuzira – alikokuchukia / dharau

iv) Meza kichaka – kuteketeza / kuunguza (4x1=4)

2. UFUPISHO

a)

utando wa ubongo (meningitis) huzua hofu

huathiri ngozi inayofunika ubongo na uti wa mgongo

bakteria huwa hatari kuliko virusi kwa kusababisha meningitis

wagonjwa wengi watibiwapo haraka hupona lakini wengine huachwa wakiwa bubu au vipovu na wengine hufariki

ugonjwa huu hutokea bila kutarajiwa, aidha kwa ghafla

ni vigumu kutenganisha dalili za ugonjwa huu na magonjwa mengine ya kawaida

ripoti hii ni kwa mujibu wa wataalamu wa afya (Hoja 7x1 =7 mtiririko = 1)

b) Dalili

watoto hupatwa na homa, hutapika, kukataa kula na kulia kwa uchungu

aidha kufura kichwa , kupumua kwa haraka, kutupatupa miguu na mwili kujikunyata

watu wakubwa hupatwa na maumivu makali ya kichwa na shingo nzito

wao hutapika na kukosa ufahamu

aidha hupatwa na mikono na miguu baridi, maumivu ya misuli kwa damu kuwa na sumu

Hatua:

Mhasiriwa yeyote anayeshukiwa apelekwe hospitalini mara moja.

hoja 5 za dalili

hoja 1 ya hatua 6x1=6 1 mtiririko

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) i) neno li-ya

ii) mate ya –ya (2x1=2)

b) Nendeni – hali ya amri / rai

ni – kitenzi kishirikishi kipungufu

kitenzi kishirikishi

kitenzi

niliyemwacha – nafsi / nafsi ya kwanza umoja

nafsi ya kwanza / nafsi ambata

maktabani - kielezi mahali (4x ½ =2)

c) i) /d h/ - meno na ulimi

ii) /gh/ - kaakaa laini na ulimi

d)mwema – kivumishi (v)

vyema - kielezi (E)

wema – nomino (N)

e) – Alisema angemkuta papo hapo ikiwa angeenda keshoye.

- Alisema angemkuta papo hapo angeenda keshoye / siku iliyofuata (4x ½ =2)

f) aliyetumwa

hajaipata karo (2x1=2)

g)i) –Mbili ni matokeo ya tano kuondoa tatu.

- Mbili ni matokea ya tatu kuondolewa kwa tano. (alama 1)

ii) Mwalimu anayefunza Kiswahili ni yuyu huyu. (alama 1)

iii) Ng'ombe waliokuwa nyuma ya nyua walichechemea kwa vile waliumia kwato zao.

(4x ½ =2)

h) ndwele – ugonjwa

- maradhi *kutambua –alama 1* *sentensi - alama 1*

a-kiwakilishi nafsi cha tatu umoja

li- kiwakilishi cha wakati uliopita

ye- kirejeshi

ni- kitendewa / shamirisho / nafsi ya kwanza umoja

chokoza- shina / mzizi wa kitenzi

a – kimalizio

- kiishio
- hali ya kutenda (6x ½ =3)

j)i) Mwanafunzi amepewa jarida na muktubi.

ii) Samaki wengi walivuliwa na Bate. (2x1=)

k)i)Uhusiano zaidi ya hayo

-tena / pia / vilevile / aidha

ii) kuonyesha chanzo

tangu, toka. *kutaja 2x1=2* *kutunga 2x1=2* (alama 4)

l)Kandanda ni mchezo maarufu duniani.

S → KN + KT
KN → N
N → Kandanda
KT → T + N +V + E
T → ni
N → Mchezo
V → Maarufu
E → duniani (8x ½)

m)-ambao / waliokuwa

- karimu (2x1=2)

n) i) Angeenda ½

Angepata ½

ii) usije – njoo / uje (alama 2)

o) Ngoma hizo zitachezwa nyanjani

4. **ISIMU JAMII**

-Hospitali

- Zahanati (2x1=2)

- Kiingereza

-Kiswahili (2x1=2)

c)- maswali na majibu

-mahojiano

-maelezo

-ushauri / wosia / mawaidha

-shughuli (kupimapima)

-masharti

-usiri *(Hoja za mwanzo 3x1=3)* *(kutaja ½)* *(kufafanua / maelezo ½* *(6 x ½ =3)*

d)

-umoja na utangamano

-mawasiliano miongoni mwa wananchi

-hutambulisha utamanduni

-huziba mipaka ya kikabila

-hurahisisha utawala / uongozi

-huleta ajira (2x1=1*)* *(Hoja za mwanzo mbili)*

e) Matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili

-dhana ya sheng

-lugha ya kwanza

-kiingereza kupewa hadhi zaidi ya Kiswahili

-kiswahili kama lugha ya ujanja

-uhaba wa walimu *(Hoja za mwanzo mbili 2x1=2)*